Kikao cha Sita - Tarehe 18 Oktoba, 2013,

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika. (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha Mezani Hotuba ya Uwasilishaji wa Taarifa ya Serikali juu ya Hoja mbali mbali za Kamati ya PAC ya Baraza la Wawakilishi kuhusu Shirika la Umeme (ZECO). Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 27
Ujenzi wa Nyumba ya Spika

Mhe. Salim Abdalla Hamad - Aliuliza:-

Ninavyohisi ile nyumba nzuri iliyojengwa kwa ajili ya Mhe. Spika, Baraza la Wawakilishi aishi katika nyumba hiyo imekamilika na iko tayari kuhamiwa.

a) Nyumba ile imegharimu kiasi gani cha fedha na fedha hizo zimetoka wapi?

b) Vigezo vilivyohitajika katika ujenzi huo vimefikiwa vilivyo?

c) Kuna mpango wowote wa Mhe. Naibu Spika, na wenyeviti wa Baraza kujengewa nyumba za kuishi kama ilivyofanywa kwa Mhe. Spika?

d) Nyumba ile inao mpango gani wa kuhamiwa na Mhe. Spika wa Baraza la Wawakilishi?

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam 27 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, kwa kiasi kikubwa nyumba iliyojengwa kwa ajili ya makaazi ya Mhe. Spika, wa Baraza la Wawakilishi hapo Migombani imekamilika. Nyumba hiyo imegharimu kiasi cha Tshs. 1,204,215,269/= ambazo asilimia 82 ni msaada kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na asilimia 18 ni fedha zilizotolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

b) Mhe. Spika, nyumba hiyo ilijengwa na Kampuni ya Ujenzi ya *Quality Building Contractors Ltd* na kusimamiwa na Mshauri wa majengo maarufu (Ndugu Ramadhan Bakar) (Rama China) na ujenzi huo umekidhi viwango vilivyowekwa.

c) Mhe. Spika, kwa sasa serikali kupitia Ofisi ya Baraza la Wawakilishi, haijapanga kujenga nyumba za makaazi kwa ajili ya Naibu Spika na wenyeviti wa Baraza.

d) Mhe. Spika, ilitarajiwa kuwa Mhe. Spika, ahamie katika nyumba hiyo itakapomalizika kujengwa pamoja na kuwekwa fanicha, hayo yote sasa yamekamilika lakini kumejitokeza upungufu wa maji katika jengo hilo ambalo linaendelea kufanyiwa kazi, na kuanzia sasa wakati wowote Mhe. Spika, atahamia katika jengo hilo.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya mdogo wangu hapa Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, naomba niulize swali dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, kwa kuwa Spika ni miongoni mwa viongozi wakubwa wanaoongoza mihimili mitatu mikubwa ya nchi, na kwa kuwa Maspika wana kazi kubwa za kuongoza vikao vikubwa kama hichi, na kwa kuwa kuongoza kikao kama hichi ni kazi kubwa mno, wanahitaji maspika wetu kupata mahali patulivu pale ambapo wanapomaliza kazi zao na kujipumzisha kama vile sehemu za pembezoni mwa mji au karibu na fukwe za bahari ili kusudi waweze kupata upepo mzuri kutuliza mawazo yao kuweza kuendesha kikao kikubwa kama hichi.

Je, kumuweka Spika, wetu barabarani kama vile mahali ambapo magari yanafanya zogo, walevi wanapita wanafanya zogo si kumdhalilisha Spika wetu katika hili?

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza nataka nikubaliane naye kwamba Mhe. Spika, ni mmoja katika viongozi wakuu wa nchi yetu ambaye anaongoza muhimili huu mzito kabisa wa Baraza la Wawakilishi. Kwa dhana hiyo ndio maana Mhe. Spika, anahitaji kupewa kila fursa zinazostahiki ili aweze kufanya kazi zake vizuri na ndio maana tukaamua kumjengea Mhe. Spika, nyumba mahala pazuri.

Kuhusu kuwa barabarani si kumdhalilisha hata kidogo, maana hata Mhe. Rais wetu nyumba yake ipo barabarani, yote haya ni katika mapenzi tu, ya kuona kwamba ni mahala gani katika maeneo yetu ni mazuri ili viongozi wetu hawa wakuu wakae ili sio tu wakae mahali pazuri lakini pia waone vinavyopita nje pale ili wazidi kuridhika. Ahsante.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika nakushukuru kwa dhati kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mimi nataka kujua tu nyumba ambayo imejengwa ya Mhe. Spika, ambayo anatarajia kuingia ina uwezo wa kukaa familia ngapi kwa wakati mmoja. *(Makofi) (Vicheko)*

Mhe. Spika: Mheshimiwa hili litafutie mahali pengine pa kuuliza. Hii imekuwa nzuri kwa chai ya asubuhi (*Kicheko*) (*Makofi)*

Nam. 94
Baa Kuanzishwa Katika Makaazi ya Watu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Kumekuwepo na wimbi kubwa la baa kuanzishwa katika makaazi ya watu hasa katika mitaa ya Mbweni, Kiembesamaki, Amani na maeneo mengine na kusababisha uchafuzi wa mazingira na kero ya muziki kwa wananchi.

(a) Kwa nini serikali imekuwa ikitoa leseni za biashara kuanzisha miradi hiyo bila ya kuzingatia athari zake kwa wananchi wa maeneo husika?

(b) Kuna maana gani ya kukataza vilabu vya michezo kutangaza pombe ili kulinda mila na utamaduni wakati serikali hiyo hiyo inatoa leseni za kuuza pombe hadi katika makaazi ya watu?

(c) Je, tunatengeneza taifa la vijana wa aina gani kama kila mtaa tunaruhusu kuanzishwa vilabu vya pombe Zanzibar?

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwanza napenda niwapongeze sana Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa imani yao ya kutaka Mhe. Spika, aweze kuishi vizuri pamoja na familia yake.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 94 lenye kifungu (a), (b) na (c) kabla ya kumjibu naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, biashara ya vileo ambayo hufanyika katika mabaa hufanyika baada ya wahusika kupata leseni ya kuendesha

biashara hiyo chini ya Sheria ya Vileo sura ya 163 ya mwaka 1928 chini ya usimamizi wa Bodi ya Vileo. Ili mwenye baa apate leseni inabidi awasilishe maombi ya leseni katika Bodi ya Vileo na baada ya Mahakama ya Vileo kupokea maombi, hufanya ukaguzi wa maeneo husika na hutangazwa tarehe za vikao vya kujadili maombi pamoja na pingamizi za wananchi kama zipo kuhusu kuwepo kwa baa katika maeneo husika na kutolea maamuzi. Baada ya Bodi ya Vileo kutoa orodha ya baa zilizoruhusiwa kukata leseni hutolewa muda wa siku 14 kwa ajili ya kusikiliza rufaa za maamuzi kabla ya kutolewa leseni.
Pamoja na kuendelea kutumika kwa sheria hiyo lakini ni sheria ya muda mrefu na Ofisi yangu itaifanyia mapitio na kuangalia uwezekano wa kutunga sheria mpya itakayoendana na wakati tulionao. Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake.

(a) Mhe. Spika, utoaji wa leseni za biashara za vileo imekuwa ikiwashirikisha wananchi wa maeneo husika na inafanya hivyo kwa kuzingatia utekelezaji wa Sheria ya Vileo sura ya 163 ya mwaka 1928.

(b) Mhe. Spika, serikali kupitia bodi ya vileo huwa inaweka mbele kulinda mila na Utamaduni wa watu wake wakati wa utoaji wa leseni kwa baa na kuzingatia sheria, kanuni na miongozo mbali mbali ya uuzaji na utangazaji wa vileo.

(c) Mhe. Spika, ni kweli kwamba uanzishwaji wa vilabu vya pombe au baa katika makaazi ya watu kunaweza kwa kiasi kikubwa kuporomosha maadili na hatimaye kuathiri mila na utamaduni wetu kwa vijana na jamii kwa ujumla.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri kutokuwa muafaka na majibu yenyewe kwa wananchi naomba nimuulize maswali mawili ya nyongeza.

a) Wakati gani mila na utamaduni unalindwa na wakati gani mila na utamaduni unavunjwa ukizingatia serikali hii imepiga

marufuku kwa vilabu kutangaza pombe wakati serikali hii inatoa leseni kwa ajili ya baa?

b) Serikali inatambua kuwa wananchi wamekuwa wakilalamika sana katika mahakama za vileo na hakuna hatua zinazochukuliwa?

c) Je, utakuwa tayari nikuletee hao wananchi wanaolalamika ili uchukue uamuzi muafaka kwa vile limekuwa likiudhi wananchi hata watoto kutopata nafasi ya kusoma kwa wakati?

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, kwanza ijulikane kwamba utoaji wa leseni za baa (vileo) upo kwa mujibu wa sheria niliyoitaja, ndio maana serikali hivi sasa inazingatia namna ya kuipitia sheria hiyo, kwa sababu hiyo sheria ni ya zamani sana. Baada ya kukamilisha utaratibu wa kuweza kutunga sheria mpya mambo mengi sana yatazingatiwa katika kulinda mila na utamaduni na silka ya Wazanzibari.

a) Sio sahihi kusema kwamba hakuna mazingatio yoyote kwa serikali juu ya kero za wananchi hilo si kweli. Pale ambapo wananchi wamekuwa wakilalamikia jambo hilo serikali hufika katika eneo hilo na kama ikibidi hushauriwa mwenye baa ili aondoke katika eneo hilo. Kama nilivyosema kwamba unapotoa leseni ya vileo unatoa siku 14 kwa wananchi wa eneo lile waweze kuleta pingamizi kama lile jambo linalofanywa hawalipendelei au wanalipendelea, kwa mujibu wa sheria hiyo ipo. Kwa hiyo si kweli kama serikali pengine haijali mila na silka na tamaduni zetu.

b) Hakuna sababu yoyote iliyofanya kuweza kupiga marufuku kwa pombe kutumikia vilabu. Kwanza ieleweke leseni za vileo zinatoka kwa mujibu wa sheria, upigaji wa marufuku ilikuwa ni amri na wala sio sheria. Kwa hiyo ni busara za serikali ndio ilipokea wazo la kuweza kusema ni vizuri vilabu na wakati ule wakati wa utawala wa Serikali ya awamu ya tano, chini ya mshauri Mohammed Raza ndio alikuja na wazo hilo serikalini.

Sasa ni busara tu ya kiongozi aliyekuwepo wakati ule akalikubali hilo suala lakini halipo kwa mujibu wa sheria. Utoaji wa leseni za vileo huu unaofanyika upo kwa mujibu wa sheria, na sheria inapokuwa na tatizo serikali kazi yake kutafuta namna ya kuweza kurekebisha au kuiandika upya ili kuweza kuondokana na hayo matatizo ambayo yamejitokeza katika utekelezaji wa sheria.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, katika maneno yake Mhe. Waziri amesema kuwa sheria hii inayoruhusu kuweka vileo ni sheria ya 163 ya mwaka 1928 yaani ni miaka isiyopungua 85 iliyopita, wakati Mhe. Waziri na kila mtu anajua kuwa kutumia ulevi si jambo jema, na kwa sababu swali mama linaeleza kuwa hivi vilabu vya pombe vimewekwa katika maeneo ya watu na athari ya pombe na kunywa pombe tunaielewa, na hawa hawa watu wanaofanya maasi makubwa ni wale wanaokunywa pombe. Kwa nini Mhe. Waziri wakati anajua hii kulewa si vizuri pamoja na kuwa kuna sheria ya kuweka pombe kwa miaka yote hiyo 85 hajafikiria kubadilisha sheria hii ikawa bado inaendelea tu na kuudhi?

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, mimi Haji Omar Kheri naelewa kwamba kunywa pombe ni jambo ambalo sio zuri kwangu mimi hasa nikiwa Muislamu, nimetoka katika mifupa ya Kiislamu nalielewa hilo, lakini wapo ambao wanaona kwamba kunywa pombe ni kama jambo la kawaida.

Kwa hivyo serikali kwa kutambua kwamba hili jambo sio zuri katika kufanyika hasa katika makaazi ya watu, ndio maana Wizara yangu ilichukua hatua ya kulipeleka suala hili pamoja na sheria hiyo ya zamani katika Tume ya Kurekebisha Sheria; na Tume ya Kurekebisha Sheria imefanya kazi hiyo kwa uadilifu, imepita katika maeneo yote ya Unguja na Pemba katika kutaka

maoni ya wananchi juu ya marekebisho na utungaji wa sheria hii ya vileo.

Kwa hiyo Tume ya Kurekebisha sheria imeshakamilisha kazi hiyo, ni hivi punde tu Tume ya kurekebisha sheria itawasilisha mapendekezo yake kwa Wizara ili tuweze kuingia katika mchakato wa kuitunga hiyo sheria na halafu tuilete hapa Baraza la Wawakilishi ili Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi muweze kuamua.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza nichukue nafasi hii nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametufikisha katika hali ya usalama na hasa kusherehekea Sikukuku yetu ya Eid el Haj.

Mhe. Spika, nitamuuliza Mhe. Waziri atakubalina na mimi kwamba nchi yoyote inaendeshwa kwa mujibu wa taratibu na sheria za nchi, lakini haiendeshwi nchi kwa matakwa ya mtu au kwa watu wambao wanasababisha baadhi ya mambo. Je, Mhe. Waziri atakubaliana nami suala hilo?

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Asha Bakari Makame, kwamba nchi huendeshwa kwa mujibu wa sheria za nchi na taratibu za nchi na sio kwa matakwa ya mtu au utashi wa mtu binafsi.

Nam. 17
Mpango wa Kudhibiti Ukataji Miti Kwenye Bonde la Chaani – Masingini

Mhe. Ussi Jecha Simai - Aliuliza:-
Wizara ya Kilimo kupitia Idara ya Misitu inaendeleza upandaji wa miti katika bonde la Chaani Masingini Wila ya Kaskazini "A". Kwa bahati mbaya wananchi hasa wakulima wanaolitumia bonde hili wamekuwa wakikata miti pamoja na kuing'oa hivyo kuitia serikali hasara.

a) Je, Wizara yako ina mpango gani wa kuwaelimisha wananchi wanaolitumia bonde hilo juu ya umuhimu wa misiti hiyo katika maisha ya binaadamu na viumbe wengine?

b) Je, Wizara imepanda miche mingapi kwa mwaka 2013 na miche mingapi imeng'olewa au kukatwa na wananchi?

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili - Alijibu:-

Ahsante Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam 17 lenye vifungu (a) na (b). Kwanza naomba kutoa maelezo mafupi kuhusiana na shamba la miti la Chaani Masingini kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Shamba la Miti Chaani Masingini lilianzishwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mwanzoni mwa miaka ya 1980. Shamba hili lilitangazwa rasmi kuwa msitu wa hifadhi ya serikali mwaka 1987 na wananchi waliokuwa wakimiliki maeneo hayo walilipwa haki zao kwa mujibu wa sheria. Kabla ya kutangazwa rasmi wakulima wa maeneo hayo walitoa malalamiko yao kwa serikali ya kutaka kumegewa sehemu ya eneo hilo. Jumla ya hekta 200 zilitolewa ili wakulima wa bonde hilo waendeshe shughuli zao za kilimo. Eneo lilobakia lenye ukubwa wa hekta 456 likatangazwa rasmi katika gazeti la serikali kuwa ni hifadhi.

Mhe. Spika, madhumuni ya kuanzishwa kwa shamba hilo yalikuwa ni kuhifadhi udongo kutokana na mmong'onyoko wa ardhi, kurejesha rutba na kuhifadhi vyanzo vya maji ambavyo vilikuwa vimeanza kupotea kutokana na ukame na upungufu wa miti katika eneo hilo. Kusudio jengine la upandaji wa miti katika eneo hilo ni kupata mazao ya misitu yakiwemo kuni na majengo ili kukidhi mahitaji ya wananchi wa Kaskazini ya kisiwa cha Unguja ambako kuna upungufu mkubwa wa mazao hayo.

Mhe. Spika, sasa naomba kujibu maswali ya Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, Wizara yangu inaamini kwamba umuhimu wa shamba la miti la Chaani unafahamika na wananchi wengi

wanaoishi katika maeneo hayo, pengine hata Mkoa wote wa Kaskazini. Kwani wananchi wengi wa Mkoa huo walikuwa wakipata mahitaji yao ya miti, kuni, majengo na hata ajira kutoka katika shamba hilo.

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo na Maliasili bado inaendelea na mpango wake wa kutoa elimu kwa wananchi hao kupitia vyombo vya habari kuhusu umuhimu wa miti pamoja na kulihifadhi shamba hilo kwa faida ya vizazi vya sasa na vijavyo. Aidha wizara imeshaanza kukutana na uongozi wa Wilaya ya Kaskazini "A" na "B" pamoja na Masheha wa Wilaya hizo, ili kuwahamasisha na kuzungumza na wananchi wao kuhusu utunzaji wa shamba hilo pamoja na faida ziliopo.

Wizara pia inashirikiana na vikundi vya uhifadhi wa mazingira vya Kikobweni (HIMAKI), Chaani kubwa (JUMACHA) na Chaani Masingini (HIMACHA) katika kutoa elimu, na pia kushiriki kuliimarisha shamba hilo.

Mhe. Spika, kuiharibu miti kwa makusudi katika shamba hilo ambalo ni mali ya serikali ni kwenda kinyume na utaratibu wa sheria ya nchi. Hivyo basi Wizara ingawa haipendi sana kuchukua sheria za kuwafungulia mashtaka pamoja na kuwaadhibu wahalifu hao waliovunja sheria, hata hivyo lisilo budi hutendwa. Hivyo basi wizara yangu haitoacha kuchukua hatua kali kwa wale watakaobainika wanaharibu kwa makusudi miti au mali nyengine za serikali katika shamba hilo.

b) Mhe. Spika, kuanzia mwaka 2012 Wizara hii iliweka lengo la kupanda misitu hekta 50 sawa na wastani wa miti 100000 kwa mwaka, hata hivyo kwa mwaka huu 2013, jumla ya hekta 55 sawa na miti 100500 ilipandwa. Kwa mwaka wa fedha 2013 jumla ya hekta 69 sawa na miche 128500 imeshapandwa.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu swali langu la msingi alisema kwamba wananchi wengi hasa wa Mkoa wa Kaskazini wanaelewa umuhimu wa miti, lakini vile vile alisema pia kwamba kukata miti kinyume na utaratibu ni kosa kisheria. Nataka anieleze kwa kuwa hilo ni kosa je, Wizara yake imewachukulia hatua za kisheria watu wangapi kutokana na uharibifu wa mazingira tukizingatia kwamba mazingira ndio maisha ya viumbe hai?

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, baada ya kupata taarifa hii ya uharibifu wa miti kuna matukio sita ambayo tuliyapeleka kituo cha Polisi ili wahalifu hawa wachukuliwe hatua, lakini baada ya muda mrefu kuona bado hatua hizi hazijachukuliwa sisi kama Wizara, mimi na watendaji wangu tulikwenda kwa Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya tukakaa na Kamati ya Ulinzi ili kujua matukio haya bado hayajachukuliwa hatua na ilikuwa ni muda mrefu. Tukakaa nao pamoja na tukazungumza nao, tulichokifanya Wizara ya Kilimo ilitoa wito kwa Jeshi la polisi kuharakisha kukamilisha, kulikuwa bado haujakamilishwa utaratibu wa kisheria ili kukamilisha utaratibu wa kisheria na uchunguzi wa ziada ili hatua za Mahakama zichukue nafasi yake.

Mheshimiwa mpaka sasa hivi huu wito tuliutoa katika jeshi la Polisi na bado hatua hizi hazijachukuliwa. Tunatarajia kwamba wahalifu hawa watachukuliwa hatua.

Mhe. Kazija Khamis Kona: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza.
Mhe. Naibu Waziri, alitueleza katika jibu la msingi ya kwamba kuanzia 2012 hadi 2013 kuna miti ilipandwa lakini nataka kujua kati ya miti iliyopandwa ni mingapi iliyoharibiwa na mingapi bado haijaharibika kwa mwaka 2012 hadi 2013.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, mwaka 2012 nilisema kwamba tulipanda miti 100,500 lakini miti

iliyoharibiwa ni miti 50,000, kwa hivyo miti 100,500 ukitoa miti 50,000 iliyoharibiwa, iliyobakia haikuharibiwa. Mwaka 2013 tulipanda miti 128,500 hii tulipanda, lakini jumla ya miti iliyoharibiwa ilikuwa ni miti 38,000 iliyobaki haikuharibiwa.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kuna suala ambalo Mheshimiwa sasa iko haja katika sehemu ambazo ni za wananchi waliokuwa karibu na misitu kuwafanyia semina ya kuwapa faida na hasara zake.

Lakini pili, huoni Mheshimiwa sheria yako ya misitu imeshapitwa na wakati?

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, ninachukua ushauri wake juu ya kuwafanyia semina watu hawa waliokuwa karibu na misitu suala hili tutalichukua na kulizingatia ili kuwapa semina wajue umuhimu wa misitu.

Suala la sheria hii ya misitu kwamba imeshapitwa na wakati pia tunachukua ushauri wake ili kuja kuitizama kuifanyia mapitio tena sheria hii.

Nam. 25

Baadhi ya Wananchi Kunyimwa Mikopo PBZ

(Mhe. Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hilo ameliondoa)

Nam. 48

Msimamo Kuhusu Wajumbe Kuchangia Maendeleo

Mhe. Salim Abdalla Hamad - Aliuliza:

Kumekuwa na mtindo Waheshimiwa Wawakilishi wanapoomba huduma ya umeme au maji kwa vile vijiji ambavyo havina huduma hiyo hupata maelekezo ya kuwa wagharamie wenyewe upatikanaji huduma hizo.

Je, huu ni msimamo wa Wizara au ni utashi wa baadhi wa watendaji wa Wizara hii tu?

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake nambari 48 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, sera ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuwasogezea karibu huduma za umeme na maji wananchi wote wa Visiwa hivi vya Unguja na Pemba hasa wanaoishi vijijini ili kuwapunguzia gharama kubwa ya kujisogezea huduma hizo. Katika utekelezaji wa sera hii Serikali hutenga fedha katika bajeti yake ya mwaka kwa lengo la kupeleka umeme vijijini kwa utaratibu wa awamu.

Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa fedha baadhi ya wakati Waheshimiwa Wawakilishi kupitia mifuko yao ya majimboni huombwa kusaidia kuchangia baadhi ya gharama kwa vijiji ambavyo huduma hiyo bado haijafika na havijaingizwa kwenye bajeti.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, kwa sababu Mfuko wa Jimbo tunaopewa hautoshelezi kupeleka huduma kwa wananchi kutokana na baadhi ya majimbo yetu yalivyo. Na

unapopeleka msaada katika sehemu moja ya huduma hii huwa ni lawama kwa sehemu nyengine. Sasa kwa vile tunapokwenda Wizarani kuomba msaada wa kupewa hizi huduma, ninashukuru Wizara kazi kubwa inayofanya ni kufanya vipimo, kuandika vifaa na makisio ugharamie ili kazi ile itekelezwe. Je Mheshimiwa kutokana na mfuko wetu wa Jimbo ulivyo na mahitaji yanayohitajika ni makubwa sana, haoni kuwa Mheshimiwa sasa ni lazima aone kuwa mfuko huu usiwe ni sababu ya kutopatiwa huduma katika maeneo kadhaa?

Pili kwa vile katika Shehia ya Mtambwe Kusini kuna kijiji cha Makongeni, Tondooni, Mitambuuni na hata Kinazini wote hawana huduma hii, maji na ni muhimu sana na hasa pale Makongeni penye skuli pamoja na hospitali. Sijui Mheshimiwa atatoa uzito gani kwa sehemu hizi kupatiwa maji haraka iwezekanavyo na kuwafanya wananchi wangu waondokane na dhiki kubwa sana ya kuchota maji chini kabisa katika milima?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kama nilivyoeleza hapo awali Serikali kupitia wizara yangu huwasogezea wananchi huduma ya umeme na maji katika vijiji vyao isipokuwa kwa kile kijiji ambacho hakijaingizwa kwenye bajeti, basi litakapotokea ombi hilo huombwa Waheshimiwa Wawakilishi wachangie lakini bado wizara yangu iko makini katika kulitekeleza hili kupitia Shirika la Umeme na Mamlaka ya Maji. Kwa hivyo vijiji ambavyo havijafikia huduma hiyo si kama vimesahauliwa au tu kwamba vimeachwa kwa makusudi, isipokuwa tunaangalia utaratibu wa bajeti yetu, na uwezo wa kifedha unaporuhusu basi tutaendelea kuvipelekea huduma hiyo vijiji vyote ambavyo havijapata huduma hiyo.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Kutokana na kuwa mfuko wa Jimbo hautoshelezi kupeleka huduma hii muhimu katika majimbo yetu kutokana na mazingira ya jimbo lenyewe lilivyo, ni lini Mheshimiwa atafanya huruma ya kusaidia kuona kuwa

vijiji vya Makongeni, Tondooni, Mitambuni na Kinazini vyote vikiwa Mtambwe ya Kusini lakini nilisema na hasa kijiji cha Makongeni ambacho ni cha kuanzia chenye hospitali pamoja na Kituo cha Afya watapelekewa huduma hii?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji basi italiangalia suala hilo na hali ya fedha itakaporuhusu basi kijiji chako kitashughulikiwa na kitapelekewa huduma hiyo.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ahsante sana Mhe. Spika, kunipa fursa hii kumuuliza Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati swali la nyongeza. Kwa sababu kumekuwa na usumbufu mkubwa wa kutosha katika kijiji cha Jitenge Maziwani Jimbo la Kojani na jitihada zilizofanywa na mimi mwenyewe Mwakilishi na Mbunge pamoja na Halmashauri ya Wilaya lakini mpaka leo hii maji wananchi wa kijiji hicho hawajapata. Hivyo utakubaliana na mimi kwamba iko haja Wizara kuingia kati katika kushughulikia suala hilo?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Spika, ni kweli baadhi ya kasoro zimejitokeza hususan katika vijiji vingi tu si kijiji hicho kutokana na hili suala zito la maji hususan kutokana na baadhi ya miundombinu yetu kuharibika mara kwa mara. Lakini hilo lieleweke ni jambo la kawaida kwa sababu miundombinu ni kitu ambacho kinatengenezwa kwa hivyo kutokezea uharibufu ni kitu cha kawaida.

Lakini vile vile niseme kwamba Mheshimiwa Mwakilishi naomba uelewe kuwa Serikali imejitahidi katika kusambaza maji kwa sababu sasa hivi tumeshafika asilimia 80 ya kuwasambazia wananchi wa mjini na vijijini likiwemo jimbo lako la Kojani. Si muda mrefu tumefungua mradi mkubwa tu wa maji ndani ya jimbo la Kojani, kwa hivyo ningekuomba Mhe. Mwakilishi uendelee na subra, wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji

itapitia katika eneo la Kijiji hicho na kuchunguza na kujua nini tatizo ili tulipatie ufumbuzi wananchi hao wapate huduma hiyo ya maji safi na salama.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa mujibu wa Katiba ya wananchi kusogezewa huduma ya maji, umeme ni wajibu wa serikali kwa mujibu wa katiba ya mwaka 1984, vijiji vingi vimekuwa vina matatizo na hasa ZECO ikipeleka huduma ile inaonekana imefanya kitu kama hisani. Je serikali itakuwa tayari kuleta wawekezaji wengine ili wananchi wanufaike na ukitizama kuwa biashara ya ushindani na ushindani huwaneemesha wananchi je, serikali iko tayari kufanya hivyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwanza nataka Mhe. Mwakilishi ajue kwamba suala la maji Zanzibar si biashara isipokuwa suala linalohusiana na maji ni kwamba wananchi wanachangia, wanatakiwa wachangie kwa mujibu wa utaratibu tuliokuwa nao lakini si suala la biashara. Bado Serikali ya Mapinduzi Zanzibar iko makini na iko tayari kuwahudumia wananchi wake hususan kupitia suala hili la maji na umeme.

Nam. 42

Haja ya Kuweka Muda Mwengine wa Kufanyika Tamasha la Mzanzibari

Mhe. Nassor Salim Ali - Aliuliza:

Kwa mwaka wa pili sasa Tamasha la Utamaduni wa Mzazibari linaloanza Juni, 19 kila mwaka halifanyiki kwa kuwa linaangukia mwezi wa Ramadhani.

Je, Wizara haioni kwamba ipo haja kuweka tarehe nyengine na mwezi wa kufanyika tamasha hilo?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Rahaleo swali lake Nam. 42 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa miaka miwili mfululizo tamasha la utamaduni wa Mzanzibari linaloanza Juni 19 kila mwaka halifanyiki kwa sababu linaingiliana na mwezi mtukufu wa Ramadhani, Wizara yangu imezingatia suala hilo na kuona pia ipo haja ya kulipangia muda mwengine tamasha hilo ili liweze kutoa mafunzo kwa jamii zijazo kwa kuhakikisha kwamba tamasha hili linaendelea.

Mhe. Spika, katika kuuthamini utamaduni wetu, Wizara yangu inahakikisha suala hili linapatiwa ufumbuzi.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, mbali na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, wizara imeona kuwa hilo tatizo wameliona lakini Mhe. Spika, Tamasha hili huwa linaitangaza Zanzibar katika masuala ya utalii, na Tamasha hili limekuwa kivutio kikubwa kwa watalii. Je, ni lini hasa Wizara itaona kwamba ni mwezi gani na tarehe gani ya kuliendesha Tamasha hili ili kuitangaza Zanzibar katika masuala haya ya utalii?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, Mhe. Mwakilishi nakubaliana na wewe kwa hoja zako hizo lakini kama nilivyoeleza Tamasha liliingiliana na mwezi mtukufu wa Ramadhani, lakini Wizara kwa kushirikiana na Serikali tuna mpango wa kuweza kuweka mwezi mwengine ili lisiambatane na Ramadhani. Mhe. Mwakilishi mwezi wa nane tulikuwa na tamasha la Mangapwani, kwa kweli nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi kwa kushirikiana na wizara tuweze kufanya matamasha kwenye Wilaya zetu.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, naomba kuuliza swali dogo la nyongeza lenye vifungu (a) na (b). Nilitaka kujua tu sababu gani za msingi zilizopelekea tamasha hilo lisifanyike mwezi wa Ramadhani, wakati lengo la tamasha ni kuitangaza Zanzibar?

(b) Hayo mambo yaliyopelekea kutofanyika tamasha hilo mwezi wa Ramadhani mwezi wa kula mchana inakuwa halali?

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, ninakushukuru, sababu za msingi ambazo Wizara imeamua kutolifanya tamasha hili katika mwezi mtukufu wa Ramadhani ni kuzingatia hali halisi ya mwezi, mafundisho ya dini yetu na mambo ambayo yanafanyika hasa mchana katika mwezi mtukufu wa Ramadhani ambao kwa kweli huwa ni makuruhu sana kwa watu walio na ibada hiyo. Sasa kwa sababu asilimia karibu 98, 99 ya Wazanzibari huwa wamo katika ibada nzito Wizara yangu imeona si busara kufanya mambo ambayo yangeweza kwa njia moja au nyengine kupelekea vishawishi vya kutengua ibada yao.

Sasa suala la kwamba je ni halali kufanyika wakati mwengine, si halali lakini ni tofauti wakati mtu akiwa na ibada wakati ambapo hayumo katika ibada. Kwa kuzingatia hilo sasa Wizara yangu imeamua hivyo, na kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri kwamba tunaangalia mambo mawili. Kwanza mwezi wa Juni ujao utakuwaje, kama utaangukia mwezi mtukufu wa Ramadhani basi tutapanga mwezi mwengine, lakini kwa sababu miezi hii ya Juni inakwenda mzunguko na tunapofanya utaratibu na utafiti mwengine inawezekana kwamba mwaka huu hali ikawa nzuri zaidi.

Kwa hivyo Mhe, Spika, hiyo ndio sababu ya msingi ambayo tumefanya kuangalia suala hilo kwamba tulisitishe katika mwezi mtukufu wa Ramadhani kwa kuzingatia ibada ya wananchi na mila na utamaduni wetu.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ahsante sana Mhe. Spika, kunipa fursa hii kumuuliza Mhe.Naibu Waziri swali la nyongeza. Mhe. Spika, kwa sababu kuna haja ya kufufua michezo ya asili katika Visiwa hivi vya Zanzibar na tayari kumetayarishwa Tamasha ndani ya Wilaya ya Wete Jimbo la Kojani, tamasha la michezo ya asili ikiwemo mchezo wa ng'ombe, mchezo wa kareti pamoja na michezo ya mashindano ya ngalawa na madau, na mashindano ya mbio za magunia na mambo mbali mbali yanayohusiana na michezo. Yalitarajiwa kufanyika tarehe 16 mwezi huu tulionao na mpaka sasa hivi wananchi wameshahamasika na jambo hili ndani ya Wilaya ya Wete, na sasa hivi tarehe imepita ni lini Mhe. Naibu Waziri Tamasha hili litafanyika tarehe itayopangwa tena baada ya kupita tarehe hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Ahsante Mhe. Spika, Mhe. Mwakilishi ninakubaliana na wewe yote hayo kwa sababu tulikaa pamoja na wewe tukapanga lakini tu ninakuhakikishia Mhe. Mwakilishi swali lako lipo na tutalikamilisha tukiwa pamoja na wewe, lakini tukikosa mwezi huu mwezi ujao tutafanya tamasha hilo.

Nam. 52

Sababu za Ongezeko la Maradhi Nchini

Mhe. Salim Abdalla Hamad - Aliuliza:

Katika miaka ya karibuni kumejitokeza wimbi la maradhi mbali mbali yanayoathiri afya za wananchi wengi Zanzibar hali inayopelekea kudhoofisha nguvu ya rasilimali watu.

Ni sababu zipi hasa zilizopelekea wananchi kupata maradhi mbali mbali kwa wingi kama vile sindikizo la damu, kansa, kupoteza nguvu za kiume, kisukari n.k.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake nam. 52 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla sijajibu nilikuwa kidogo nataka nitoe indhari kwa Waheshimiwa Wawakilishi. Waheshimiwa mawaziri huwa mara nyingi tunapokuwa na shughuli za Baraza tunakuwa na shughuli nyengine katika mawizara. Na huwa tunapaswa kwenda inapobidi, lakini tukiwa hatupo Waheshimiwa Wawakilishi wanakuwa wanafanya zogo jingi wanasema sisi hatukai. Lakini wakati huo huo na wao sisi tunapokuwa tunajibu wao huwa hawakai wanatoka na baada kurudia masuala hayo kwa hayo.

Swali hili nilijibu Baraza lililopita nilimjibu Mhe. Mwanajuma Mdachi na leo suala hili limejirudia tena mara ya pili, hata nikilijibu mara 20 jawabu itakuwa ndio hiyo hiyo haitobadilika. Kwa hivyo naomba Waheshimiwa Wawakilishi wasitoke tunapojibu ili waweze kusikiliza kuepuka kwamba tusirudie masuala haya.

Baada ya utangulizi huo naomba kumjibu Mheshimiwa.

Mhe. Spika, magonjwa sugu yasiyoambukiza (*chronic non-communicable diseases*) yanachangiwa kwa kiasi kikubwa na mtindo ya maisha na ndio maana wataalamu husema ni "*life style diseases*", ambapo mtu mwenyewe binafsi anapelekea kwa kiasi kikubwa kupata maradhi kama Kisukari, Maradhi ya moyo, shinikizo la damu na saratani na sababu zake zimegawika makundi mawili kama zifuatazo:-

(a) Sababu ambazo mtu anaweza kujiepusha nazo
- kula mlo usio kamili
- Matumizi ya pombe
- Matumizi ya tumbaku
- Kutofanya mazoezi

- Uzito uliozidi au kupindukia
- Msongo wa mawazo
- Matumizi makubwa ya chumvi

(b) Sababu ambazo hazikwepeki
- Umri mkubwa
- Urithi

Hii inamaanisha mfumo wa maisha na tabia ya mtu katika maisha au urithi. Na umri huwa yanaambatana na athari nyingi ikiwemo ile ya kupoteza nguvu za kiume, hivyo katika kuendeleza na kudumisha afya ya mtu na kuzuia maradhi hususan magonjwa sugu yasioambukiza tunashauriwa kufuata mtindo bora wa maisha ambao unazingatia ulaji bora kufanya mazoezi ya mwili, kuepuka matumizi ya sigara na bidhaa zinazotokana na tumbaku, kuepuka matumizi ya pombe na kuepuka kuwa na msongo wa mawazo.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, pamoja na kuwa Mhe. Naibu Waziri sikumsikia vizuri sana kutokana na sauti yake, lakini alizungumza kuwa moja katika mambo ambayo Waheshimiwa hawazingatii yanapotolewa majibu ni kufanya zogo katika Baraza lako tukufu. Mhe. Spika, naomba niseme kuwa sote tunajua kuwa hiki chombo ni kitukufu na tunakuja hapa kusikiliza kwa makini yanayozungumzwa na tukapata maswali ya nyongeza, lakini kurejea swali la mtu mwengine lililojibiwa haina maana kuwa yule mtu hakusikia jibu lakini hakuridhika na jibu ifahamike hivyo.

Pili, ninamuomba Mhe. Waziri kuwa hapa anazungumza na Waheshimiwa kuambiwa kwamba tunafanya zogo ni kuvunja heshima ya Baraza lako Tukufu, naomba suala kama hili asiombe radhi lakini asirudie tena kwa heshima ya Baraza lako na wanaotusikiliza.

Swali langu la nyongeza ni kwamba hii dunia imeanza zamani, na wazee wapo mpaka wa miaka 100 hivi sasa walioanza zamani na bado ni wazima lakini haya mambo ya haya maradhi yamekuja hivi karibuni watu wengi wana presha, watu wana upungufu wa damu, watu wengi wana maradhi ya *cancer*, nguvu za kiume zimepotea. Ninaamini lazima kuna sababu zilizosababisha hivyo kwa nini zamani ilikuwa hakuna hivi sasa imeenea na hasa Zanzibar naomba anipe sababu ni kitu gani kilichosababisha tukapata maradhi haya?

Mhe. Spika: Labda niseme moja dogo lile alilosema Mhe. Naibu Waziri la wakati wa vikao na wakati shughuli zinaendelea kwamba Waheshimiwa tubaki ndani hilo amenisaidia na kwa kweli ni wajibu wetu kuona kwamba tunabaki ndani humu kufanya kazi tuliyotumwa na wananchi. Kwa hivyo hilo wala hakuna haja ya kumwambia asirudie. Mimi nilipaswa nisisitize zaidi hiyo kwa hivyo ninamshukuru kunisaidia.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, mimi naona Mhe. Salim kilichomshughulisha zaidi ni huko kupoteza nguvu zaidi za kiume kuliko hayo mengine. Sidhani hayo mengine kwake kama ni *issue.* Sasa nasema hivi.

Utaratibu

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, mimi sijasikia lolote naona watu wanapiga meza tu naomba azungumze tusikie vizuri ili na sisi tufaidike. Pili, sikukusudia nguvu za kiume pekee ni pamoja na maradhi mengine.

Mhe. Spika: Tuwe watulivu tusikilize majibu na yeye atajitahidi kunyanyua sauti ili aelezee kuhusu matatizo ya nguvu za kiume pamoja na maradhi mengine.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba niendelee. Sababu za msingi ni maendeleo ya nchi, maradhi haya zamani

yalikuwa ya nchi zilizoendelea na kadiri nchi itakavyoendelea maradhi yanahama kutoka nchi moja kwenda nchi nyengine, wao kwao ni tatizo kubwa, na sisi sasa nchi inaendelea. Matumizi ya vitu ambavyo vinakatazwa ni mengi, moshi wa magari mabovu ni mengi, uharibufu wa mazingira ni mkubwa. Kwa hivyo, kuna kila sababu na sisi kufikia hayo. Nchi zilizoendelea zilipitia katika njia hii ambayo sasa hivi sisi tunapitia, kwa hivyo kwa njia moja au nyengine. Zamani sababu zetu zilikuwa ni mbili, aidha uwe umerithi au umri mkubwa, waliokuwa umri mkubwa walikuwa si wengi, *life span* ilikuwa ni ndogo, kwa hiyo watu wengi walikuwa hawafikii hivyo.

Lakini urithi hilo mpaka mtoto mchanga anaanza nalo. Kwa hiyo ni kiwango kile tu cha watu ambao zamani ndio walikuwa wakipata matatizo hayo. Lakini sasa hivi watu wote umri unafika mbali mno kutokana na maendeleo, kutokana na kwamba watu wanaishi vizuri, tumetoka hatua moja kwenda hatua nyengine ya maisha. Tanzania inakwenda katika nchi ambazo zinatakiwa ziwe na maslahi ya kati katika ulimwengu. Kwa hiyo kuna mambo mengi yatakayotokea na yakasababisha ugonjwa huu hatuna jinsi ya kuyaepuka isipokuwa tu, yale ambayo yanasababishwa na sisi binafsi hayo lazima tuyafanyie kazi. Mazoezi tufanye kama tunataka, sigara tusivute, na mengine yale ambayo nimeyashauri. Tukifanya hivyo tutapunguza kwa kiwango fulani, haimaanishi kwamba hutougua kwa sababu mengine hayako kwenye uwezo wetu, moshi *ozone* kuchafuka, uchafuzi wa mazingira, yale yako nje ya uwezo wetu, kwa hivyo tutaugua tu.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa sababu hivi sasa upotezaji wa nguvu za kiume umekuwa ni gumzo kubwa, sasa naomba nijue serikali imefanya utafiti wowote kuhusu hili. Kama umefanya ni wanaume wangapi Zanzibar walioathirika na jambo hilo?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kama maradhi yako mengi mpaka ukasikia watu wanalalamika basi ujue tatizo ni kubwa, lakini bahati mbaya mimi mwanamke, wanaume si mara nyingi kukubali kwamba wakatoe siri zao kuwa mimi sifai. Kwa hivyo, hatuwezi tukapata takwimu kwa sababu hawajitokezi, jitokezeni tukuhesabuni mliokuwa mnapoteza nguvu za kiume tupate takwimu.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, kunipa nafasi hii na mimi nikauliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba tatizo hili ni kubwa sana na anaelewa kuwa kuna sababu ambazo zimejitokeza na kuna sababu ambazo zinalifanya tatizo hili litokezee.

Namuuliza Mhe. Naibu Waziri je, atachukua hatua gani ya kuwapitia wananchi au kufanya mikutano akawaeleza wananchi wale kufahamu tatizo hili kama alivyotuelezea sisi na tukafahamu jinsi ya tatizo hili lilivyotokea.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, utaratibu wetu tunatumia vyombo vya habari; magazeti na redio, kupita kwa wananchi kutahitaji gharama ambazo sitokuwa nazo.

Nam. 107

Ujenzi wa Njia ya Mashine ya Maji

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk – Aliuliza:-

Naipongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara yake ya Miundombinu na Mawasiliano kwa jitihada zake za kuzijenga njia za ndani katika maeneo mengi ya Unguja na Pemba.

(a) Je, Mhe. Waziri huoni kuwa ni jambo la busara kuwaambia wananchi wa maeneo hayo ni nani aliyejenga njia hiyo?

(b) Lakini pia kutokana na umuhimu wa njia ile atakubaliana nami kuwa muda umefika sasa kwa njia ile kuwekwa lami ili kuwapunguzia vumbi wananchi wa maeneo hayo?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nam. 107 lenye vifungu (a) na (b). Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi ambaye ni Mwakilishi wa Jimbo la Kitope lakini ni mkaazi mwenzangu katika Jimbo la Fuoni naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mhe. Spika, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano imepewa jukumu kwa mujibu wa Sheria ya kujenga na kutunza barabara ambazo zimetajwa kwenye Sheria husika. Barabara hizo ni Barabara Kuu (*Trunk Roads*) Barabara za Vijijini *(Rural Roads)* na barabara zinazounganisha ama barabara kuu na za vijijini (*Feeder Roads*).

Aidha, Sheria ya Tawala za Mikoa pia imeainisha majukumu ya kuzijenga na kuzitunza Barabara za Mitaa za Miji na barabara za ndani kupitia Manispaa, Mabaraza ya Miji na Halmashauri za Wilaya barabara nyenginezo za *unclassified roads.*

Kwa kuwa Manispaa, Mabaraza ya Miji na Halmashauri za Wilaya hazina wataalamu wa barabara na huwa hazitengi bajeti ya kuzifanya matengenezo barabara zao, zimekuwa zikiharibika na kusababisha usumbufu mkubwa wa usafiri wa wananchi kwenye maeneo husika. Hivyo wizara yetu imekuwa ikisaidiana

na taasisi hizo katika kuwaondoshea usumbufu wananchi wa maeneo kadhaa.

Baada ya maelezo hayo, sasa napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

(a) Kama nilivyoainisha kwenye maelezo yangu ya utangulizi, barabara ya Mashine ya Maji – Nyarugusu ni miongoni mwa barabara za ndani zinazopaswa kujengwa na Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi, lakini kutokana na Halmashauri hiyo kuwa na upungufu wa fedha za ujenzi wa barabara, pamoja na umuhimu wa barabara hiyo ambayo ilikuwa na hali mbaya, ndipo uongozi wa Jimbo la Fuoni ukiongozwa na Mhe. Mwakilishi wa Jimbo hilo walivyowasilisha malalamiko yao wizarani. Mwakilishi wa jimbo hilo waliowasilisha malalamiko wizarani, wizara yangu iliona ni vyema kuifanyia matengenezo makubwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara (*ZRF*) angalau kwa kiwango cha kifusi ili iweze kupitika kwa urahisi na wakati wote, na hivyo kuondosha usumbufu kwa wananchi hao.

    Sababu nyengine ilikuwa ni kwamba katika barabara hiyo tayari wizara yetu tulikwisha kuandaa *route* maalum kwa ajili ya daladala ambazo zimewaondoshea usumbufu wananchi waliokuwa wakikaa katika maeneo hayo.

(b) Nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa kuna umuhimu wa barabara hiyo kuiwekea lami ili kupunguza vumbi, lakini la msingi zaidi ni kuiwezesha kudumu kwa miaka mingi ni pamoja na barabara zote kama hizo tunazozijenga kwa kiwango cha kifusi. Wizara yangu na Mfuko wa Barabara hatuna fedha za kuzijenga kwa kiwango cha lami barabara hizo kutokana na ufinyu wa bajeti.

Namuomba Mhe. Mwakilishi awasiliane na Halmashauri yake ya Wilaya ya Magharibi ili watenge fedha kwa ajili ya kuiwekea lami barabara hiyo na wizara yangu itachangia wataalamu na vifaa vya ujenzi.

Mhe. Spika, wizara yangu inatoa shukurani za dhati na inaendelea kutoa wito kwa uongozi wa Jimbo la Fuoni hasa Mhe. Mwakilishi pamoja na wananchi wake wote kwa ushirikiano na ustahamilivu mkubwa waliotupatia kabla na wakati wa utekelezaji wa mradi huo kwa kipindi chote ambacho umeweza kukamilika.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kuweza kunipa nafasi kuweza kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Pamoja na majibu yake mazuri ambayo yamenifurahisha hapa. Mhe. Naibu Waziri hivi sasa ni kipindi ambacho karibu watu wataanza kufanya kampeni za kutaka kuingia kwenye majimbo. Na kwa kuwa ni hivyo kama ulivyosema kuwa suala hili limeshirikishwa na Mhe. Mwakilishi pamoja na uongozi mzima wa jimbo.

Mhe. Naibu Waziri je, watu kama hawa wanaopita wakaeleza kauli ya kusema wamejenga wao barabara ile huoni watu hawa wanaidhalilisha wizara yako pamoja na Mhe. Mwakilishi na wananchi wa jimbo lake?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, inawezekana kwamba kila mmoja akasema mradi ule ameukamilisha yeye, lakini jambo la msingi sisi kama serikali ni wajibu wetu kutekeleza miradi ya maendeleo kwa wananchi tunaowaongoza na jambo ambalo halina shaka, mwanzo wa barabara ile kuna bango ambalo linaelezea nani mfadhili na nani mjenzi, na mwisho wa barabara ile kuna bango la pili linaloelezea nani mfadhili na nani mjenzi. Kwa hivyo, kama kutakuwa kuna mtu ambaye anapotosha mimi naamini atakuwa anajipotosha yeye mwenyewe, miradi ya serikali inajulikana

wazi, utaratibu wa serikali uko wazi na siamini kama kuna mwananchi atakayeamini kwamba mradi ule haukutekelezwa na serikali kwa kupitia malalamiko yaliyoletwa na viongozi husika wa jimbo linalohusika.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kunipa fursa na mimi nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza. Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanya jitihada kubwa kujenga barabara kuwaondoshea wananchi usumbufu ili waweze kujiletea maendeleo katika nchi yao. Kwa bahati nzuri Serikali ya Awamu ya Sita iliyokuwa ikiongozwa na Mhe. Amani Abeid Karume alijenga kwa kiwango cha lami barabara ya Kilindini Micheweni, lakini kwa bahati mbaya mno katika ujenzi wa barabara zinazojengwa hivi sasa, Kampuni ya *H Young* na Kampuni ya *MECCO* imepitisha magari mazito na imeharibu barabara ya Micheweni vibaya mno kiasi cha kuwa sasa hivi haitamaniki na haipitiki.

Je, Mhe. Waziri ana mpango gani wa kuirudisha barabara ile ili irudi katika kiwango chake wananchi wa Micheweni wapate kufaidika?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, barabara anayoizungumza Mhe. Mwakilishi ni barabara ambayo imejengwa kwa kiwango cha lami, lakini bahati nzuri kwamba katika maeneo hayo hayo jirani tuna miradi miwili inayofanyika katika maeneo ya Kaskazini Pemba. Sote tunafahamu kwamba mali ghafi kubwa ya utengenezaji wa barabara ni kifusi na kwa bahati kwa upande wa Kaskazini Pemba eneo pekee ambalo lina kifusi ni katika Jimbo la Micheweni. Sasa namuomba Mhe. Mwakilishi akubaliane na rai ambayo tumezungumza nje ya Baraza hili, kwamba tuache wenzetu wakamilishe miradi ile na wenzetu nao wapate barabara za lami ikiwemo ya Konde, Mtambwe, Kojani baadae mazungumzo yetu sisi na wajenzi kuona barabara ile

tunairejeshea uhalisia wake kwa kiwango cha lami kama ilivyokuwa kabla.

Ni kweli kwamba kuna eneo ambalo limeharibika lakini tulichokiona kwa kipindi hiki ambapo yataendelea kutumika magari mazito tukisema tufanye ukarabati wa barabara ya eneo lile tutakuwa tumepoteza nguvu za wananchi, kwa maana kwamba tukiendelea kutengeneza itaharibika tena. Sasa busara tu, nimuombe Mhe. Mwakilishi kwamba tukubaliane tuvute subira, tukamilishe miradi miwili ile ikikamilika tutarudi kuja kutengeneza barabara yetu irudi katika uasili wake wa lami kama mgongo wa ngisi.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Ni lini wananchi wa Jumbi - Mkorogo watapatiwa barabara angalau ya jasi kwa vile hivi sasa kwa muda mrefu kijiji hicho hakina barabara ya aina yoyote.

Mhe. Spika: Hajakusikia sawa sawa rudia swali.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Mhe. Spika, namuuliza Mhe. Naibu Waziri kwamba wananchi wa Mkorogo ni muda mrefu hawajapatiwa barabara ya lami ama ya jasi, ni lini wananchi wa kijiji hicho watapatiwa barabara ya kufika kijijini kwao?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, wizara yetu kwa kipindi hiki tunatekeleza miradi miwili ya barabara kwa kiwango cha lami. Barabara ambazo zinajengwa na Kampuni ya Shapriya barabara moja inatoka Jendele – Ungujaukuu ambapo Ungujaukuu ni eneo la Jimbo la Koani. Na barabara ya pili inatoka Mwera – Pongwe – Jumbi ambayo pia ni Jimbo la Koani na inajengwa kwa kiwango cha lami. Mimi naamini kwamba Jumbi anayoikusudia Mhe. Mwakilishi ya Mkorogo barabara hii ndipo inapopita. Kwa hiyo Mhe. Mwakilishi kama utakuwa umepita siku mbili tatu utaona

kwamba Kampuni ya Shapriya imeshaanza kazi ya *mobilization*, kuna nyumba tayari zimeshaanza kuvunjwa, minazi tayari ishaanza kung'olewa na miti imeanza kukatwa, ile ni ishara kwamba utekelezaji wa mradi wa barabara ya lami unaanza kazi.

TAARIFA YA SERIKALI

Taarifa ya Serikali juu ya Hoja mbali mbali za Kamati ya PAC ya Baraza la Wawakilishi kuhusu Shirika la Umeme (*ZECO*)

UTARATIBU

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Spika, mimi kidogo nilikuwa nataka kupata maelezo juu ya hii Hoja ya Serikali iliyoletwa kuwa inaelezwa kwamba ni Hoja ya Kamati ya *PAC*. Lakini ninavyofahamu mimi Mhe. Spika, hoja hii kutoka kwenye Kamati ya *PAC* ilishawasilishwa Barazani na inapotoka hapa Barazani inakuwa si hoja ya Kamati ya *PAC* inakuwa ni Hoja ya Baraza. Naomba muongozo wako katika hili.

Mhe. Spika: Sasa tatizo ni nini?

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Tatizo ni kwamba hii hoja inaonekana imeandikwa katika haya maandishi yote ni hoja ya *PAC*, yaani kama ni kamati ndio imekuja kujibiwa wakati hii hoja ni ya Baraza. Kwa sababu kamati iliwasilisha Barazani na Baraza ndio likaichukua ile hoja hivyo inakuwa ni ya Baraza. Sasa kama serikali inajibu maana yake iwe inalijibu Baraza moja kwa moja badala ya kuijibu Kamati ya *PAC*. Sasa nilikuwa nataka ufafanuzi kidogo kama ni sawa hivyo basi ningeomba Mhe. Waziri arekebishe haya maelezo yake katika kuwasilisha hii hoja kwamba majibu haya yatakuwa ni hoja ya Baraza analijibu Baraza badala ya kamati.

Mhe. Spika: Kwa hivyo, unakusudia labda iwe ni Taarifa ya Serikali juu ya Baraza, hebu tusaidie iko kwa jina gani.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Spika, nakusudia kwamba hii ni Taarifa ya Serikali juu ya hoja zilizotolewa na Baraza, maana yake ile hoja ilipoteuliwa Kamati ya *PAC* kwenda kufanya ule uchunguzi ilitakiwa iwasilishe Barazani, Kamati ya *PAC* ikaja ikawasilisha Barazani na Baraza likaridhia, kama kulikuwa na mapendekezo mengine yalitolewa na Wajumbe hapa yaliingizwa kwamba sasa serikali nakupeni haya mkayafanyie kazi Baraza ndio linaiagiza serikali, sasa nafikiri inapojibu serikali ijibu kwamba inalijibu Baraza sasa isiwe inaijibu Kamati ya *PAC*. Maana yake haya maandishi ambayo yalitolewa inaonekana kama ni majibu kwa kamati, nilikuwa nataka atusaidie Mhe. Waziri kama ni hivyo basi labda amekosea katika kuandika tu. Sijazungumzia ile hoja yenyewe iliyoko ndani ni hivi vichwa vya habari kwenye maandiko yake yote mawili. Ningeshauri kwamba akayaelekeza kwamba analijibu Baraza kwa sababu hiyo hoja ni ya Baraza.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri wasilisha taarifa ya Serikali juu ya hoja ya Baraza kuhusu Shirika la Umeme.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, Ahsante naupokea ushauri wa Mhe. Mbarouk Wadi nakubaliana naye. Kwa hiyo, Mhe. Spika, maelezo yetu yatakuwa ni ya serikali juu ya hoja mbali mbali zilizotolewa na Baraza la Wawakkilishi kuhusu Shirika la Umeme la Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kwa niaba ya serikali niwasilishe hoja za serikali juu ya mambo mbali mbali yaliyotolewa na Baraza la Wawakilishi kuhusu Shirika la Umeme la Zanzibar (*ZECO*).

Kwanza Mhe. Spika, nichukue fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipa ruhusa hii, lakini vile vile kwa namna unavyoliongoza

Baraza letu kwa uadilifu na umakini mkubwa. Aidha, niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kuwa wakati wote hutoa michango sahihi yenye maelezo ya kina, yenye nia ya kuwatumikia wananchi wetu na kuleta maendeleo katika nchi yetu. Aidha, niwashukuru pia na Kamati ya *PAC* kutokana na kazi yao nzuri waliyoifanya wakaweza kuwasilisha hoja hii mbele ya Baraza hili na Baraza kuipokea na ikawa hoja ya Baraza.

Mhe. Spika, pia naomba nitoe shukurani maalumu kwa viongozi wetu wa Serikali hususan Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili wa Rais, Waheshimiwa Mawaziri, Mhe. Mwanasheria Mkuu na watendaji wote ambao waliifanyia kazi kwa kina na leo hii kwa heshima naomba niiwasilishe katika Baraza letu tukufu.

Mhe. Spika, taarifa yetu hii iko katika Makabrasha mawili; kabrasha moja ni hili ambalo liko kwenye mfumo wa *matrix* unaoonesha tuhuma, maelezo ya kamati, mapendekezo ya serikali. Na kabrasha la pili ambalo nitalisoma hili ni hotuba ninayoiwasilisha ambayo sawa kabisa na *matrix* yenyewe isipokuwa ni utaratibu tu wa uwasilishaji ambao utanirahisishia mimi kuwasilisha katika Baraza lako hili tukufu Mhe. Spika.

Baada ya maelezo haya Mhe. Spika, naomba niisome taarifa hii.

Mhe. Spika, itakumbukwa kwamba katika Mkutano wa Saba wa Baraza la Nane la Wawakilishi Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi wa kuchaguliwa na Wananchi wa Jimbo la Kiwani Mhe. Hija Hassan Hija kwa kutumia haki yake chini ya Kanuni za Baraza za kifungu cha 27(1)(m), 27(3), 48(1) na 49(1) ya Toleo la Mwaka 2012 aliwasilisha hoja binafsi kwa mujibu wa Kanuni ya 117 ya Kanuni za Baraza na kulitaka Baraza liridhie kuundwa kwa Kamati Teule kwa ajili ya kulichunguza Shirika la Umeme la Zanzibar (*ZECO*).

Mhe. Spika, vile vile itakumbukwa kwamba Baraza lako tukufu lilikubaliana kwamba hoja hiyo ya Mhe. Hija Hassan ifanyiwe kazi kupitia Kamati ya Kudumu ya Baraza ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika ya Umma (*PAC*), na Mhe. Hija mwenyewe kuingizwa katika kamati hiyo ili kusaidia katika uchunguzi huo.

Mhe. Spika, kufuatia uamuzi huo wa Baraza, Kamati ya *PAC* ikimjumuisha Mhe. Hija ilianza kazi ya kufanya kazi hiyo tarehe 30 Aprili, 2012 na kuwasilisha ripoti yake Barazani katika Kikao cha Baraza kilichofanyika mwezi Machi, 2013 na baada ya kuwasilishwa serikali iliahidi kulifanyia kazi ipasavyo ripoti hiyo ya *PAC* na baadae kuwasilishwa rasmi katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imepokea Ripoti ya Baraza la Wawakilishi kuhusu Shirika la Umeme la Zanzibar (*ZECO)* kwa moyo mkunjufu na kuifanyia kazi kwa umakini mkubwa na uadilifu wa hali ya juu ili kuona mapungufu yaliyooneshwa katika ripoti hiyo yanafanyiwa kazi kwa maslahi ya nchi yetu. Vile vile wale walioguswa wanafanyiwa haki na uadilifu kufuatana na matakwa na sheria na kanuni za nchi yetu ili haki itendeke kwa wahusika wote.

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kukushukuru kwa dhati wewe mwenyewe binafsi kwa kukubali hoja ya Mhe. Hija Hassan HIja kufanyiwa kazi na *PAC* na baadae kuridhiwa na Baraza lako tukufu. Aidha, nawapongeza kwa dhati Mwenyekiti na Wajumbe wote wa Kamati ya *PAC* kwa kazi kubwa na nzuri waliyoifanya ya kuchunguza utendaji wa Shirika la Umeme la Zanzibar na kuiwasilisha vyema kwa Baraza taarifa hiyo.

Aidha, niwashukuru Wajumbe wote kwa michango yao na kufikia mapendekezo yenye ufanisi kwa nia ya kuondoa ubadhirifu katika nchi yetu na kwa nia ya kuwatumikia wananchi

zaidi. Kwa kweli taarifa hii imetuonesha mambo mengi ambayo yanapaswa kufanyiwa kazi na serikali ili kuimarisha utendaji wa shirika kwa maslahi ya taifa letu. Muelekeo huu wa mashirikiano miongoni mwa mihimili ya serikali ndio hasa utakaosaidia katika kujenga mustakabali mwema wa nchi yetu na kuimarisha dhana ya utawala bora na kupambana na vitendo vyote viovu ndani ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa nia ya kuwahudumia wananchi wetu na kuhakikisha kuwa nchi yetu inapiga hatua kubwa kimaendeleo na kuweka misingi bora ya kujenga uadilifu ndani ya shughuli zote za serikali.

Mhe. Spika, napenda kulijuilisha Baraza lako tukufu kwamba serikali tayari imeshaanza kuyafanyia kazi mapendekezo yaliyotolewa na Baraza la Wawakilishi na kuchukua hatua stahiki katika baadhi ya maeneo yaliyopendekezwa na Wajumbe hao. Mhe. Spika, yako maeneo ya muda mfupi , muda wa kati na muda mrefu. Yale ya muda mfupi tayari serikali imechukua hatua na yale ya muda wa kati na muda mrefu yataendelea kufanyiwa kazi ili kuhakikisha kwamba yale yote ambayo yamependekezwa na Baraza hili tukufu yanafanyiwa kazi kwa maslahi ya nchi yetu. Niwapongeze sana Mhe. Spika, Wajumbe kwa kazi nzuri na kubwa ambayo wanaifanya kwa nia ya kuwatetea wananchi wa nchi hii na kuondosha kila maovu katika nchi yetu na ndani ya serikali.

Mhe. Spika, maelezo kuhusu hoja mbali mbali zilizotolewa na Baraza lako tukufu naomba niyaeleze kama ifuatavyo:-

Hoja nambari moja Wateja kupewa risiti zenye kiwango kidogo kuliko malipo halisi yanayolipwa. Mhe. Spika, katika ripoti ya Kamati ilioneshwa kasoro ya baadhi ya wateja wa shirika kupewa risiti zenye kiwango kidogo kuliko malipo halisi waliyolipa wateja hao, na hivyo kamati kupendekeza kuwa watendaji wote waliohusika wachukuliwe hatua za kinidhamu na kisheria.

Mhe. Spika, maelezo ya Serikali kuhusu hoja hii ni kwamba serikali inakubaliana na mapendekezo yaliyotolewa na Baraza lako tukufu na tayari hatua imeshachukuliwa na Shirika la Umeme kwa kuliarifu Jeshi la Polisi kuanza kuchukua hatua za kufanya uchunguzi wa malalamiko ya wateja waliolalamika kulipa fedha nyingi, lakini risiti walizopewa zimeandikwa zikiwa na fedha kidogo.

Aidha, serikali imelitaka Jeshi la Polisi liwatake wateja hao kuwabainisha watendaji waliohusika na suala hili ili liwachunguze, na iwapo itabainika kuwa wamekiuka sheria na taratibu basi hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yao.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa kifungu Nam. 44 cha Sheria ya Shirika la Umeme Nam. 3 ya Mwaka 2006, serikali imemuagiza Waziri anayehusika na Sekta ya Nishati kuunda kamati ya rufaa ya wateja ili kushughulikia malalamiko ya wateja. Napenda kuwaarifu kwamba hatua ya kuunda Kamati ya Rufaa ya Wateja inakaribia kukamilika na mambo ya msingi yanayozingatiwa katika uundaji wa kamati hii ni namna itakavyotekeleza majukumu yake. Hivi sasa Shirika la Umeme limo katika jitihada kubwa ya kushughulikia manung'uniko ya wateja na kutoa huduma zake bila ya upendeleo na kuepusha kuwepo hisia za mianya ya rushwa.

Mhe. Spika, kuhusu suala la fundi Salum Sadi Khamis. Naomba kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba, mfanyakazi huyo tayari amesimamishwa kazi ili kuruhusu hatua za uchunguzi ziweze kuchukuliwa dhidi yake.

Vile vile napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba Shirika la Umeme tayari limeshaiandikia Jeshi la Polisi kukumbushia kuhusu kesi yenye namba RB1250/2012 iliyopo kituo cha polisi Chake Chake na RB 302/2013 ya kituo cha Polisi Konde inayomuhusu ndugu Abeid Mohd Abeid, ili jeshi hilo liharakishe uchunguzi haraka iwezekanavyo, na upelelezi

utakapokamilika na kukidhi vigezo vya sheria. Hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya mtuhumiwa huyo. Aidha Kamishna wa Polisi Zanzibar ametakiwa kusimamia kwa karibu ili utekelezaji wa suala hili uende haraka.

Mhe. Spika, napende kuwajuilisha Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba tayari barua za onyo zimetolewa kwa Meneja Mkuu na Meneja wa Tawi la Pemba kwa kutokuwa makini katika kusimamia majukumu yao na kushindwa kuwasimamia vyema watendaji walioko chini yao. Barua hizi za onyo zimetolewa kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma namba 2 ya mwaka 2011, na bado serikali inaendelea kufuatilia kwa karibu mienendo ya watendaji hao ili kuona wanatekeleza majumu yao kwa mujibu wa taratibu, kanuni na sheria za utumishi wa umma. Iwapo ikibainika kwenda kinyume na yanayokubalika kufanyika kwa mujibu wa taratibu za sheria na za kiserikali hatua za nidhamu zitachukuliwa juu yao.

Mhe. Spika, serikali pia imetoa onyo la mwisho kwa maandishi kwa ndugu Ahmeid Said Yusuf kwa kitendo chake cha kujifanya wakala wa wateja na kutaka kuwaungia umeme wakati yeye ni mfanyakazi wa shirika. Aidha serikali haitomvumilia mtendaji yeyote wa shirika atakayekwenda kinyume na maadili ya kazi walizopewa.

Kuhusu hoja namba 2: Fedha za malipo ya kuungiwa umeme kuingizwa katika *account* ya mtendaji wa shirika ndugu Zakia Juma Azan.

Mhe. Spika, kuhusu hoja hii kamati ya *PAC* ilipendekeza kuchukuliwa hatua za kisheria. Kuhusu hoja hii Baraza la Wawakilishi lilipendekeza kuchukuliwa hatua za kisheria za kinidhamu kuhusu muhusika Zakia Juma Azan kwa kutokuwa muadilifu katika utekelezaji wa majukumu yake. Ndugu Zakia alijihusisha na Uwakala wa mteja kwa kuungiwa umeme wakati huo huo akiwa ni mfanyakazi wa Shirika la Umeme. Hatua hiyo

inapelekea kuwa na mgongano wa kimaslahi baina ya ndugu Zakia na Shirika la Umeme.

Kutokana na hali hiyo serikali ilikubaliana na pendekezo hilo la Baraza la Wawakilishi na tayari hatua za kumuhamisha ndugu Zakia kutoka Shirika la Umeme zimechukuliwa. Hatua hizo za kinidhamu zimechukuliwa kwa mujibu wa sheria ya Utumishi wa Umma namba 2 ya mwaka 2011. Mfanyakazi huyo amehamishiwa kutoka Shirika la Umeme kwenda Wizara ya Ardhi Makaazi Maji na Nishati na huku akiangaliwa utendaji wake ili kufuatilia kwa karibu nyendo zake.

Hoja namba 3 na 6: Kuwepo kwa makisio ya aina mbili kwa wakati mmoja. Mhe. Spika, kuhusu hoja hii serikali inalishukuru Baraza la Wawakilishi kwa kazi kubwa waliyoifanya kwa kugundua mapungufu haya ambayo yalichangia kulikosesha Shirika la Umeme mapato kutokana na udanganyifu wa baadhi ya watendaji wa Shirika kutoa makisio ya aina mbili kwa mteja mmoja.

Serikali imelitaka Shirika la Umeme kuwa makini katika utendaji wake na kuzingatia sheria na taratibu za kazi. Na wizara husika imetakiwa kuwa karibu zaidi kulisimamia shirika hili ili mapungufu kama haya yasitokee tena.

Aidha Shirika limetakiwa kuanzia sasa kuwa wazi kwa kuweka bayana vigezo na viwango bila ya kuwepo mwanya wa ubabaishaji ili kila mteja anayetaka kuunga umeme aweze kujua gharama zake. Vile vile Shirika limetakiwa kuwa makini katika kufanya tathmini ya gharama za wateja wakati wa kuungia umeme na kutoa matukio ya maelezo sahihi ya aina na sifa za vifaa vinavyotakiwa kwa mteja ili kuepuka wateja kununua vifaa visivyokuwa na viwango vinavyotakiwa au visivyohitajika.

Mhe. Spika, hatua kali zitachukuliwa kwa wale wote watakaokwenda kinyume na maadili yao ya kazi ikiwa ni pamoja

na kufukuzwa kazi au kupelekwa katika vyombo vya sheria ili haki iweze kutendeka kwa kila mmoja wetu.

Mhe. Spika, kuhusu hoja namba 4, 17 na 18: Mhe. Spika, nasema hivi kwa sababu hoja hizi zinakuwa zinalingana mshiriki *Mohammed & Bashir* kwa niaba *ya Sana Express* katika zoezi zima la uungwaji wa umeme katika Hoteli ya Misali.

Mhe. Spika, kuhusu hoja ya Baraza juu ya Ushiriki wa duka la *Mohammed & Bashir* ambalo halimo katika orodha ya maduka au makampuni yaliyopewa kibali cha shirika cha kuuza na kusambaza vifaa vya umeme. Shirika tayari imeiandikia rasmi kampuni ya *Mohammed & Bashir* kusitisha mara moja biashara ya uuzaji wa vifaa vya umeme na kwamba shirika halitosita kuchukua hatua za kisheria dhidi ya kampuni yoyote itakayoendesha biashara inayohusu masuala ya umeme bila ya kibali rasmi kutoka Shirika la Umeme.

Aidha serikali imeliagiza Jeshi la Polisi na Bodi ya Mapato Zanzibar *ZRB* kufanya uchunguzi wa kina katika kampuni hiyo *ya Mohammed & Bashir* kuhusu kutumia risiti za kampuni ya Sanaa, kwa kufanya hivyo kuna uwezekano wa muhusika kukwepa kulipa kodi. Vile vile serikali imelitaka shirika kuanzia sasa kuhakikisha linajiandaa kuwa na vifaa vya kutosha vinavyokidhi mahitaji ya wateja wanaotaka kuungiwa umeme, sambamba na kuhakikisha kuwa vifaa vya umeme vinavyotoka nje ya nchi vinakuwa na viwango bora kwa kuvifanyia ukaguzi unaostahiki kabla havijaanza kutumika kwa kushirikiana na taasisi inayohusika na ubora wa viwango; *Zanzibar Bureau of Standards (ZBS).*

Mhe. Spika, hoja namba 5: Namna ya upatikanaji wa vifaa vya uungwaji wa umeme katika hoteli ya Misali.

Mhe. Spika, kuhusiana na hoja hii ya vifaa vilivyotumika kuunga umeme kwenye Hoteli ya Misali vilivyochukuliwa kutoka katika

ghala la Shirika umejitokeza mgongano wa maelezo yaliyotolewa. Hivyo serikali imemuagiza Mdhibiti na Mkaguzi wa Serikali kufanya uchunguzi zaidi katika suala hilo. Baada ya uchunguzi huo wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Serikali itachukua hatua muafaka kwa kuzingitia ushahidi utakavyopatikana.

Kuhusu hoja namba 7: Fundi Abeid Mohammed Abeid si mfanyakazi wa Shirika lakini anafanya kazi za Shirika kinyume na utaratibu.

Mhe. Spika, tunakubaliana na hoja ya Baraza lako Tukufu kuwa fundi Abeid Mohammed Abeid si mfanyakazi wa Shirika la Umeme na kwa kutambua hilo serikali imelitaka shirika kuwa makini na watu kama hao ambao wanafanya kazi za shirika lakini si waajiriwa wa shirika hilo na kupelekea kulihujumu shirika. Shirika tayari limeiandikia Jeshi la Polisi na kulitaka kufanya upelelezi wa kina kuhusu suala hili na kwa wahusika wote na kuchukua hatua muafaka za kisheria dhidi ya wale wote watakaobainika kuhusika na makosa hayo, ikiwa ni pamoja na kupelekwa mahakamani.

Hoja namba 8: Kukiukwa agizo la Bodi ya Wakurugenzi kuhusu mgongano wa maslahi kati ya ushiriki wa ndugu Hamidu Saidan Ali na ndugu Ali Abeid Haji katika *ZECO* na *GECCO*.

Mhe. Spika, suala la kuwepo kwa mgongano wa maslahi kuhusu baadhi ya wafanyakazi wa *ZECO* pia na kwa kampuni binafsi ya *GECCO* ni jambo ambalo halikubaliki hata kidogo. Ili kuondoa mgongano wa maslahi serikali imechukua hatua ya kuwahamisha wafanyakazi hao na kuwapeleka sehemu nyengine.

Hoja namba 9: Watu walioungiwa umeme kinyume na utaratibu na baadhi ya wateja kutumia huduma hii bila ya kusajiliwa na hivyo kutumia umeme bure ambao watu hao hawamo katika orodha ya wateja wa Shirika.

Mhe. Spika, serikali inakiri kwamba lipo tatizo la baadhi ya watendaji wa shirika ambao si waadilifu huwaungia umeme wateja kinyume na utaratibu uliowekwa na shirika kwa maslahi yao binafsi. Hivyo shirika tayari limeandikia Jeshi la Polisi kuanza uchunguzi wa kina kwa wale wote waliotajwa katika ripoti ya Baraza la Wawakilishi wameungiwa umeme kinyume na utaratibu na kuwataka watu hao kuwataja waliowaungia umeme huo. Baada ya uchunguzi hatua za kisheria zichukuliwe kwa watakaobainika wana makosa. Hakuna atakayevumiliwa katika wahusika wote ambao watahusika na jambo hili. Serikali itapambana nao na wote watapelekwa katika mkondo wa sheria.

Hoja namba 10: Mkurugenzi Mkuu wa *ZBC* aliruhusu kampuni binafsi ya *Zanzibar Datacom* kutumia umeme kutoka katika mnara wa *ZBC* kinyume na utaratibu.

Mhe. Spika, kuhusu hoja hii serikali inaendelea kufuatilia suala hili kutokana na kukosekana kwa taarifa zinazowezesha kutoa maelezo sahihi na hatua sahihi kuchukuliwa. Hivyo bado utaratibu unaendelea kufuatilia kwa kina jambo hili ili upatikane ufumbuzi muafaka.

Hoja namba 11 na 25: Ndugu Mohamed Hashim Ismail aliagiza kurudishwa umeme kwenye mnara wa kampuni wa *Zanzibar Datacom* kinyume na utaratibu. Mhe. Spika, Baraza la Wawakilishi lilimuona aliyekuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugezi wa Shirika la Umeme ndugu Moh'd Hashim Ismail kuwa ameliingiza shirika katika hasara kwa kuagizwa kurudisha umeme katika mnara unaotumiwa na Kampuni ya *Zanzibar Datacom* kinyume na utaratibu.

Mhe. Spika, serikali imefuatilia hoja hii na kuona kwamba hakuna hasara iliyopatikana kutokana na amri ya Mwenyekiti wa Bodi kwa sababu ya kurudishwa umeme huo shirika liliwawekea kampuni hiyo mita ya Tukuza na deni lake la nyuma liliingizwa

katika mita hiyo. Kwa sababu hiyo serikali imeona hakuna sababu ya kumchukulia hatua za kisheria Mwenyekiti huyu wa zamani wa Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika kwa vile fedha za malipo zinatokana na mita iliyowekwa kwa ajili ya kulipa gharama hizo ambazo zimejitokeza.

Hoja namba 12: Bodi wa Wakurugenzi *ZECO* ikiongozwa na Mwenyekiti wake ndugu Mohamed Hashim Ismail ilichagua kampuni ya *CRJE* badala ya *SALCON* iliyoshinda zabuni katika ujenzi wa msingi wa majenereta 32 na baadaye kuvunja mkataba na kampuni ya *CRJE* iliyopelekea shirika kulipa fidia ya dola za kimarekani 20786 na kulitia hasara shirika.

Mhe. Spika, ni kweli Bodi ya *ZECO* iliichagua kampuni ya *CRJE* badala ya kampuni ya *SALCON* iliyoshinda zabuni ya ujenzi kwa misingi ya ujenzi wa majenereta 32 na baadae kulazimika kuvunja mkataba na kampuni hiyo ya *CRJE*. Hata hivyo fedha zilizolipwa hazikuwa za fidia ila ni malipo iliyowahi kufanywa na *CRJE*.

Aidha Serikali baada ya kulichunguza suala hili pia iligundua kwamba Kampuni ya *MANTRAC* walilipwa fedha za ujenzi huo wakati kwamba kampuni ya barabara ya *CRJE* haikulipwa kabisa. Hivyo serikali imeliagiza Shirika la *ZECO* iwaandikie *MANTRAC* kulipa fedha za *CRJE*.

Hoja namba 13: Tofauti ya malipo kwa kazi iliyofanana au wakati mwengine kazi kubwa kuwa na malipo madogo katika uungwaji wa umeme.

Mhe. Spika, kuhusu shirika kutoza malipo tofauti kwa kazi zinazofanana. Serikali imelitaka shirika liwe makini katika kufanya tathmini za gharama za wateja wake wakati wa kuwaungia umeme. Vile vile shirika limeagizwa kuweka viwango vya bei vinavyoeleweka kwa ajili ya uungaji wa umeme, ili kila anayehitaji huduma ya umeme aweze kujua

gharama halisi, ili kuepuka mwanya wowote wa upendeleo kwa wateja na kuepuka ubadhirifu unaoweza kujitokeza.

Hoja namba 14: Upendeleo katika uungwaji wa umeme ambao baadhi ya wateja walioomba mwisho wanapewa kipaumbele kuliko wale wanaoomba mwanzo.

Mhe. Spika, kwa kuwa dhamira ya shirika si kufanya kazi kwa upendeleo, hivyo shirika litajitahidi kuepuka manung'uniko na litoe huduma bila ya upendeleo na liepushe hisia za kuwepo mianya ya rushwa. Hivyo wafanyakazi watakaogundulika kupendelea wateja wengine na kuacha kufanya taratibu zinazotakiwa kwa mujibu wa kazi yao watachukuliwa hatua za kinidhamu na za kisheria ili kukomesha jambo hili.

Hoja namba 15: Malipo yaliyolipwa na baadhi ya wateja bila ya kupewa risiti kabisa na baadhi ya wateja kuuziwa vifaa vya shirika lakini hakuna risiti za mauzo hayo mfano ni *Atlas Hotel*.
Mhe. Spika, serikali imelitaka Shirika la Umeme litoe elimu kwa wananchi kwamba kamwe wasikubali kulipa pesa mikononi kwa mtu yeyote kwa ajili ya kupata huduma za umeme. Malipo yote yalipwe katika shirika na walipaji wapewe risiti zinazolingana na kiasi cha fedha zinazotolewa.

Shirika liwe makini katika kuhakikisha kwamba watu wote wasio waaminifu na watendaji wasiokuwa waaminifu hawatumii jina la shirika kujinufaisha binafsi. Programu ya kutoa elimu kwa wananchi tayari imeanza na itaendelea kwa kutumia njia ya redio, *television* na kwa maofisa wa shirika kutembelea maeneo mbali mbali ya wateja.

Aidha serikali imeona hakuna haja ya kuchukua hatua kwa Hoteli ya *Atlas* kwa vile upo ushahidi wa risiti ya kwamba hoteli hiyo imelipa gharama ya vifaa vilivyotumika kuungiwa umeme huo.

Hoja namba 16: Kazi kubwa ya kuunga umeme kwenye minara ya simu za mkononi kupewa kampuni binafsi badala ya shirika kufanya kazi hizo.

Mhe. Spika, kuhusu hoja hii ya kazi kubwa kupewa kampuni binafsi badala ya kufanywa na shirika lenyewe, serikali imeliagiza Shirika la Umeme kuhakikisha kwamba kazi ya kuunga umeme katika maeneo yote inafanywa na shirika lenyewe isipokuwa pale inaposhindikana ndio shirika liidhinishe kampuni binafsi kufanya kazi hizo.

Aidha shirika limetakiwa lihakikishe kuwa sheria na taratibu zinafuatwa kikamilifu katika kuteua kampuni binafsi na kwamba hakutakuwa na mgongano wa kimaslahi baina ya *ZECO* na kampuni hizo. Viongozi au watumishi wa shirika lazima wachukue kila hatua kuhakikisha taratibu zinafuatwa. Shirika limetakiwa kujipanga vizuri ili kuhakikisha kwamba kazi zinafanywa na shirika lenyewe badala ya kufanywa na makampuni binafsi.

Hoja namba 19: Shirika kuendelea kuruhusu *GECCO* kufanya biashara ya *Transformer* wakati kuna agizo la Bodi ya Wakurugenzi ya shirika kufuta kibali cha biashara hiyo kwa kampuni ya *GECCO*. Mhe. Spika, serikali imeshangazwa sana na kitendo cha *ZECO* kuwakataza *GECCO* kuuza *Transformer* huku shirika hilo kuzikubali *Transformer* za *GECCO* zinazoletwa na wateja na pia kutoheshimu maamuzi wa bodi iliyokataza shirika hilo kupokea *Transformer* kutoka kampuni ya *GECCO*.

Kutokana na hali hiyo serikali imelitaka shirika la umeme Zanzibar kuheshimu maamuzi ya Bodi ya Wakurugenzi yaliyotolewa kwa shirika hilo. Serikali tayari imeshamuonya Meneja Mkuu wa *ZECO* kuhusiana na suala hili na kuliagiza shirika kuchukua hatua za kinidhamu kwa wengine wote waliohusika na suala hili ili mambo kama haya yasitokee tena.

Hoja namba 20: Upotevu wa kumbukumbu za mteja Wasi Kichanga. Mhe. Spika, serikali imeliagiza Shirika la Umeme kufanya uhakiki kwa wateja wake wote wakubwa na wadogo ili kujua idadi halisi ya wateja na kuweka kumbukumbu zao.

Aidha serikali imeliagiza Shirika la Umeme kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya wafanyakazi waliohusika na kitendo cha kuyaacha majalada ya wateja wa shirika hilo kuroa. Pia agizo limetolewa kwa shirika hilo kuwachukulia hatua za kinidhamu wafanyakazi wote waliohusika na upotevu wa majalada ya wateja wakubwa wa shirika pamoja na wateja wa vituo vya minara ya simu. Shirika tayari limeanza kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya wahusika wote kwa kutaka kutoa maelezo kwa nini shirika lisiwachukulie hatua kwa makosa waliyoyafanya.

Mchakato wa kuchukua hatua unaendelea kwa kufuata taratibu za Utumishi wa Umma na wizara husika itaendelea kusimamia kwa karibu jambo hili ili lifanikiwe kama maagizo ya serikali.

Hoja namba 21: Kutochukuliwa hatua za kisheria dhidi ya *Residence Hotel* ambayo ilivuta umeme kwa kutumia kampuni ya *CRJE* badala ya *ZECO* na kuiruhusu kampuni ya *GECCO* kufanya kazi za uungaji umeme huku ikieleweka wazi kuwa sheria inakataza suala hili.

Mhe. Spika, kuhusu hoja hii serikali imebaini kuwa kazi ya uungaji wa umeme katika hoteli za *Residence* imefanywa na *ZECO* na kampuni ya *CRJE* imeilipa *ZECO* gharama za kazi za uungaji. Kampuni ya *GECCO* imeiuzia kampuni ya *CRJE* vifaa vya umeme uliotumika katika kazi hiyo. Hivyo kwa undani utaona taratibu zimefuatwa.

Hoja namba 22: Kuhusu uungwaji wa *Kendwa Beach Resort, Docrim Hotel* na *The leisure* bila ya kufuata utaratibu.

Mhe. Spika, katika kuhakikisha kwamba masuala kama haya hayajirudii, serikali imelitaka Shirika la Umeme kuhakikisha kwamba linawahakiki wateja wote wakubwa na wadogo ili kujua idadi halisi ya wateja na kumbukumbu zao. Kazi ambayo tayari shirika imeanza kuitekeleza kwa kuandaa mfumo wa kumbukumbu za wateja (*Data Base)* ambao utakuwa unafanyiwa mapitio mara kwa mara.

Aidha serikali imelitaka shirika kuhakikisha kwamba kila mteja anayetaka kuungiwa umeme ajaze fomu ya maombi ya kuungiwa umeme na taarifa zake zihifadhiwe uzuri ili ziweze kupatikana zinapohitajika. Serikali imeitaka wizara husika kusimamia kwa karibu utekelezaji wa mfumo huu wa kuweka kumbukumbu kwa wateja.

Hoja namba 23: Kushindwa kuthibitisha wapi zimenunuliwa nguzo za *Transformer* katika nyumba za kupumzikia ya ndugu Shumbana Amani Karume. Kushindwa kuthibitishwa wapi imenunuliwa *Transformer* ya '*The Sayyida Hotel*' na wapi wamelipwa gharama za uungwaji wa umeme wa hoteli hiyo na taratibu zipi zilitumika, aidha kusamehewa kodi ya *VAT* kwa hoteli hiyo.

Mhe. Spika, serikali ililifanyia ukaguzi eneo linalohusika na hoja hii na kubaini kwamba nguzo zilizotumika katika kupeleka umeme huo ni 20 na Shirika la Umeme ndio lililopeleka nguzo hizo.

Aidha serikali ilipeleka umeme kwa kuelewa kwamba eneo hilo ni eneo la uwekezaji na tayari hoteli mbili zimeshajengwa katika eneo hilo. Hasa ukiona kwamba serikali ina wajibu wa kupeleka miundo mbinu katika maeneo ya uwekezaji.

Mhe. Spika, kwa upande wa hoja inayohusu *The Sayyida Hotel*. Napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba hoteli hiyo ililipa

kodi ya *VAT* kama inavyohitajika. Aidha hoteli hiyo haikuunga umeme kwa kutumia *Transformer* yake.

Kuhusu hoja namba 24: Upatikanaji wa *Transformer* ya Hoteli ya *Larosa Deivent* na kwa nini taratibu za kawaida hazikufuatwa.

Mhe. Spika, serikali imelifuatilia suala hili na kubaini kwamba *Transformer* iliyowekwa katika hoteli ya *Larosa Deivent* imenunuliwa na mmiliki wa hoteli hiyo kutoka kampuni ya OSAJU.

Hoja namba 26: Kampuni za *Zanzibar Datacom* kwa mnara wa Mtoni inadaiwa kiasi gani na italipa kwa utaratibu gani. Mhe. Spika, kampuni ya *Zanzibar Datacom* ilikuwa inadaiwa dola za kimarekani 9600 na hadi kufikia mwezi wa Oktoba 2013 kampuni hiyo ilikuwa imeshalipa dola za kimarekani 3600 na kubakia deni la dola za kimarekani 6000. Shirika la Umeme limeingia makubaliano na Kampuni ya *Zanzibar Datacom* ambapo utaratibu ni kufanya malipo kila mwezi ambayo inatarajiwa kukamilika ndani ya kipindi cha miezi 24 kuanzia mwezi wa Machi mwaka 2013.

Hoja namba 27: Suala la kuhamishwa *Internal Auditor* kutoka Pemba na kwa nini kwa muda mrefu *account* za hesabu za Pemba hazijafanyiwa ukaguzi wa ndani wala wa nje.

Mhe. Spika, napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba ni kweli mchunguzi wa hesabu za ndani wa Shirika la Umeme Pemba alipewa uhamisho. Hatua za kumuhamisha mfanyakazi huyo zilichukuliwa kutokana na kutowajibika kwake ipasavyo. Kitendo ambacho kilipelekea kutotoa ripoti za ukaguzi hata moja kwa kipindi chote alichokuwepo katika nafasi hiyo.

Hivi sasa shirika tayari limeshampeleka mchunguzi wa hesabu za ndani mwengine wa kudumu huko Pemba, na pia serikali

imeagiza Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuzifanyia ukaguzi hesabu za shirika hilo huko Pemba ili kuona hali halisi ilivyo.

Hoja namba 28: Hakuna ruhusa iliyotoka kwa Bodi ya Wakurugenzi kuhusu ajira ya wafanyakazi 16 walioajiriwa mwaka 2008.

Mhe. Spika, serikali inakubaliana na hoja ya Baraza la Wawakilishi na kulitaka shirika kutotafautisha baina ya kuidhinishwa kwa bajeti na kuidhinisha kwa ajira. Hivyo shirika limetenda kosa la kuajiri wafanyakazi 16 mwaka 2008 bila ya kupata idhini ya Bodi ya Wakurugezi, na hivyo serikali tayari imempa onyo Meneja Mkuu wa Shirika la Umeme na kumtaka awe makini zaidi katika utelekezaji wa majukumu yake na kufuata sheria na taratibu zilizowekwa.

Hoja namba 29: Kasoro zilizotajwa kuhusu uajiri kuanzia 2008 mpaka 2012.

Mhe. Spika, kuhusu kasoro zote zinazohusiana na masuala ya uajiri zilizotajwa katika hoja hii serikali imeliagiza Shirika la Umeme kufuata kwa ukamilifu sheria na taratibu zote za ajira kwa mujibu wa sheria ya Utumishi wa Umma namba 2 ya mwaka 2011 ikiwemo kuzitangaza nafasi za kazi, kuweka vigezo sahihi, kufanya usaili na kuwepo kwa mikataba ya ajira.

Aidha shirika limetakiwa kuandaa mpango wake mkubwa wa mafunzo utakaotekelezwa bila ya upendeleo ili kuhakikisha kwamba taratibu zilizowekwa zinafuatwa.

Hoja namba 30: Uuzwaji wa gari *land rover* SLS 1023 na *toyota Pick up* SLS 1045 ambazo ziliuzwa bila ya idhini ya Ofisi ya Rais Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Spika, kuhusiana na hoja hii naomba kulieleza Baraza lako tukufu kwamba barua iliyotoka Ofisi ya Rais Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo kuidhinisha kuuzwa kwa mali za Shirika la Umeme haikuidhinisha uuzwaji wa gari namba *land rover* SLS 1023 na *toyota Pick up* SLS 1045.

Mhe. Spika, gari hizi ambazo hazikuidhinishwa aliuziwa ndugu Shaib Hassan Kaduara, hivyo serikali imeagiza kufanyika uchunguzi wa kina na kubaini mazingira yaliyopelekea ndugu Kaduara kuuziwa gari hizo. Serikali tayari imemuandikia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kulishughulikia suala hilo.

Aidha hatua za kinidhamu na kisheria zitachukuliwa kwa aliyehusika iwapo itabainika kuwa gari hizo ziliuzwa bila ya kufuatwa taratibu.

Mhe. Spika, hoja namba 31: Uuzaji wa mali za shirika ambazo ziliuzwa na uongozi wa shirika badala ya kitengo cha manunuzi kama sheria inavyoelekeza. Kifungu namba 175(3) cha kanuni za sheria namba 9 ya mwaka 2005.

Mhe. Spika, kuhusu hoja hii serikali inakubaliana na pendekezo la Baraza la Wawakilishi na hivyo imeiagiza Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika hilo kuwachukulia hatua za kinidhamu kwa kupewa onyo wote waliohusika na kuuza mali za shirika bila ya kufuata taratibu zilizowekwa na serikali.

Hoja namba 32: Tafauti kati ya orodha ya vitu vinavyoidhinishwa na bodi na vitu halisi vilivyouzwa na shirika katika mnada wa tarehe 18/12/2011.

Mhe. Spika, katika hali ya kawaida tungetarajia kuwa kwa vile Shirika la Umeme tawi la Pemba liliorodhesha idadi ya vitu walivyotakiwa kiviuza, Ofisi Kuu ya Unguja ilipaswa kuorodhesha vifaa vyote vilivyoruhusiwa kuuzwa na mauzo

yafanywe kwa mujibu wa ruhusa hiyo. Hivyo kwa kuwa kuna vitu vimeuzwa bila ya kufuata taratibu, serikali inaendelea kufanya uchunguzi na hatua za kinidhamu na kisheria zitachukuliwa kwa wahusika wote watakaobainika na makosa kwa mujibu wa Sheria za Utumishi wa Umma na Sheria ya Manunuzi.

Hoja namba 33: *Transformer KVA* 1500 ambayo haimo kwenye vifaa vilivyopigwa kwenye mnada iliondolewa katika eneo ililokuwepo na haijulikani ilikopelekwa.

Mhe. Spika, kuhusu hoja hii serikali imeagiza Ofisi ya Mdhibiti Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kulifanyia uchunguzi ili kubaini uhalisia wa suala hili. Hatua za kisheria na kinidhamu zitachukuliwa kwa wale watakaobainika kuhusika na upoteaji wa *Transformer.*

Hoja namba 34: Kukodi gari kwa mtu binafsi kwa ajili ya kazi za shirika na kutumia pesa nyingi badala ya kununua gari yake kama hiyo.

Mhe. Spika, ni kweli muda wa miezi tisa ni mrefu kwa kukodi gari ya mtu binafsi kwa kufanya kazi za shirika. Hivi sasa Shirika la Umeme tayari limeshapata gari zake na hivyo limeachana kabisa na utaratibu wa kukodi gari za mizigo za watu binafsi.

Aidha shirika limetakiwa wakati wote kuweka mawazo ya kibiashara ili kuepuka kulitia hasara. Hivyo watendaji wote wanatakiwa kuwa makini katika kutekeleza wajibu wao.

Hoja namba 35: Licha ya kuwepo na mkataba baina ya shirika na mtu binafsi kwa nini alikuwa anatiliwa mafuta kutoka katika vituo vya mafuta vya shirika? Fedha alizokuwa akikatwa zilikuwa zinakwenda wapi?

Mhe. Spika, serikali imefuatilia hoja hii na kuona kwamba ni kweli baadhi ya siku gari iliyokodiwa ilikuwa inatiwa mafuta na shirika baada ya kukosekana mafuta katika vituo vya mafuta. Gharama za mafuta aliyokuwa akitiliwa zilikuwa zinakatwa katika malipo ya mwenye gari hiyo na fedha kurudi katika shirika kwa faida, kwa vile shirika lilikuwa linanunua mafuta hayo kwa bei ya jumla ya kumtaka mwenye gari kwa bei ya reja reja. Hivyo hakukuwa na upotevu wa fedha za shirika katika suala hili la utiaji mafuta kwa utaratibu huo.

Hoja ya 36 na 37: Majenereta 32 yaliopo Mtoni yalipatikana kwa fedha za *MDRI* au mfadhili? Na taratibu gani zilizotumika katika kuyanunua.

Napenda kutoa ufafanuzi kuwa majenereta haya hayakununuliwa kwa fedha za *MDRI* bali yalinunuliwa kwa fedha za wahisani na serikali. Aidha unuzi huu ulifanywa kwa mashirikiano baina ya wahisani na serikali chini ya mshauri wa mradi wa umeme vijijini aliyekubalika na wahisani hao. Ununuzi huo ulifanyika chini ya utaratibu wa manunuzi katika hali ya dharura ambao ulikubalika na pande zote mbili.

Hoja Nambari 38: Mpango wa Shirika la Umeme Zanzibar wa kuyatumia majenereta 32 ya dharura kwa ufanisi na kwa kutumia gharama nafuu. Mhe. Spika, kuhusiana na hoja kutakuwa shirika kuwa na mpango wa matumizi ya majenereta 32 ya dharura ya Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, tayari imeandaa mapendekezo kuhusu majenereta hayo dharura na serikali itayajadili mapendekezo hayo na itatoa maelekezo kwa wizara husika hivi karibuni.

Mhe. Spika, kuhusu mtizamo wa serikali kuhusu ripoti ya Baraza la Wawakilishi. Mhe. Spika, baada ya kutoa ufafanuzi juu ya hoja mbali mbali zilizotolewa katika ripoti ya Baraza la Wawakilishi, yapo mambo ambayo serikali imeona ni vyema

kutoa mtizamo wake ili kuwa na uchambuzi unaostahiki na kuweka mwelekeo mwema wa baadae.

Aidha, mtizamo huo wa serikali una nia ya kutoa ushauri juu ya masuala yanayojitokeza kwa kamati za kudumu wakati wakielezea majukumu yake kwa mujibu wa sheria. Hatua hii itatusaidia pale itakapotokea haja ya kuwa na kamati maalumu au Kamati Teule inayokwenda kuchunguza jambo ili kamati hiyo iweze kufanya kazi kwa uadilifu na bila ya kuonekana kuwa na upendeleo wa upande mwengine.

Mhe. Spika, serikali inashauri katika kazi zijazo za kamati za Baraza hili ni vyema ripoti zikaonesha kwa uwazi maelezo kamili yanayotolewa na watendaji ili watendaji wapate fursa ya kujieleza pale ambapo mbele ya kamati kutoa maelezo yake.
Aidha, serikali inashauri kwamba Baraza liangalie Kanuni 120 na kuona uwezekano wa kuifanyia marekebisho ili Mjumbe anayetoa hoja asiwe mjumbe katika kamati inayoundwa kuchunguza hoja hiyo. Maana hapa itakuwa unatoa tuhuma na wewe mwenyewe unachunguza, kitu ambacho kinaweza kutoa wasi wasi kwa upande mwengine.

Hitimisho:

Mhe. Spika, kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, naomba kwa mara nyengine tena kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa jinsi unavyosimamia kazi za Baraza kwa umakini na umahiri mkubwa na kuwezesha kuwasilisha taarifa hii ya serikali kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu.

Vile vile naomba kuchukua fursa kuwashukuru Wajumbe wote wa Baraza kwa umakini mkubwa wa kusikiliza hotuba hii. Vile vile naomba nimshukuru Mhe. Hija Hassan Hija Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Kiwani kwa ujasiri wake na uzalendo wake wa kuibua hoja ambayo kwa kweli imetuonesha

mapungufu mengi tuliyonayo ndani ya shirika, mapungufu ambayo serikali imeweka nia ya dhati ya kupambana nayo si kwa Shirika la Umeme tu, bali kwa kuhakikisha kuwa katika taasisi zake zote mapungufu haya yasiweze kujirudia na kujitokeza.

Mhe. Spika, nachukua fursa hii kuwashukuru na kutoa pongezi za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati ya PAC Mhe. Omar Ali Shehe na Wajumbe wote wa kamati hiyo kwa kazi kubwa na nzuri waliyoibua mambo mengi muhimu yenye mustakabali mwema katika kulijenga shirika letu na kuimarisha uchumi wa taifa letu.

Aidha, nirudie kuwashukuru tena Wajumbe wa Baraza hili tukufu kwa kuridhia maelezo ya Kamati ya PAC kufanya kazi hii ambayo sote kwa faida yake tumeiona kwa kufuatilia kwa karibu na kwa umakini mkubwa yale yote ambayo yametolewa.

Mhe. Spika, napenda sana niwashukuru sana Wajumbe wetu kwa kazi kubwa wanayoifanya kazi kubwa wanayoifanya kila wakati katika kuishauri serikali ili tuweze kuwatumikia wananchi kwa uadilifu na kwa umakini. Nataka nikuhakikishie Mhe. Spika, kazi hii imefanywa na serikali kwa kushirikiana na vyombo vyake mbali mbali ili kuhakikisha kwamba haki inatendeka na uadilifu unakuwemo serikalini na kuepuka mapungufu mengi ambayo mara nyingi yanajitokeza.

Baada ya maelezo haya, naomba Mhe. Spika, sote tushirikiane ili kuhakikisha tunatimiza wajibu wetu. Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.
Ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe hiyo ndio taarifa ya serikali juu ya utekelezaji wa hoja mbali mbali ambazo zilitolewa na Baraza hili, kutokana na kazi kubwa iliyofanywa na

Kamati ya PAC ambayo iliwasilishwa kipindi kilichopita, na serikali kuifanyia kazi na leo kutoa taarifa rasmi.

Hoja Waheshimiwa Wajumbe imetolewa na ninataka nimkaribishe Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya PAC anakuja kufanya kazi hiyo kwa niaba ya Mwenyekiti. Karibu Mhe. Fatma Mbarouk Said.

Mhe. Fatma Mbarouk Said (Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya PAC): Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (PAC) kuhusu utekelezaji wa ripoti ya Kamati juu ya Shirika la Umeme Zanzibar.

Mhe. Spika, jambo lolote linahitaji baraka na rehma za mwenyewe Mwenyezi Mungu kuanza kwa jina lake tukufu na mimi nianze kumtaja Mwenyezi Mungu Subuhana Wataala anayetupa uzima na afya njema tukaweza kufika katika Baraza hili na kujadili mambo mbali mbali kama tunavyotakiwa kufanya hivyo na Katiba ya Zanzibar na sheria ya nchi.

Nikiwa mbele yako Mhe. Spika, na mbele ya macho ya wananchi wa nchi hii, nasikitika habari hii kufika kwa wananchi wa mataifa mengine duniani. Sina budi kutoa shukurani zangu kwako na Wajumbe wa Baraza hili kwa moyo mmoja kuikubali ripoti ya Kamati ya PAC iliyopewa kazi ya kufanya uchunguzi maalumu kwa utendaji wa mambo mbali mbali ya Shirika la Umeme la Zanzibar, kazi ambayo tuliifanya kwa ueledi mkubwa na ugumu na changamoto nyingi zilizotukabili.

Mhe. Spika, shukurani za dhati ziwe kwa Baraza hili kwa kuipokea ripoti yetu ya Kamati baada ya kuiwasilisha kutokana na Wajumbe hawa kuifahamu vizuri na ndipo kwa kauli moja Baraza liliikubali ripoti hiyo na kuiagiza serikali iyatekeleze

mapendekezo ya ripoti hiyo bila ya kuipa ruhusa ya kufanya mapitio yaliyoelezwa na ripoti hiyo.

Mhe. Spika, nataka kulikumbusha Baraza lako tukufu kwamba wajibu wetu kama kamati kuhusiana na kazi tuliyopewa na Baraza hili kufuatia hoja binafsi ya Mhe. Hija Hassan Hija ya kuunda Kamati Teule kulichunguza shirika hilo na hatimaye Baraza kuamua kazi hiyo ilifanywe na Kamati ya PAC.

Wajumbe huo umemalizika tu mara kamati yetu ilipowasilisha ripoti yake mbele ya Baraza hili na baada ya hapo ripoti hiyo na kila kilichomo kilibadilika na kuwa ni ripoti ya Baraza, na maagizo yaliomo ambapo kabla ya kuwasilishwa yalikuwa ni mapendekezo ya kamati, yaligeuka na kuwa ni maagizo ya Baraza.

Mhe. Spika, kwa udhati huu hata leo nikisimama na kuitwa jina lile lile la Mhe. Omar Ali Shehe Mwenyekiti wa Kamati ya PAC na nikapewa tena hadhi na heshima ile ile ya Mwenyekiti wa Kamati, sitokuwa na uwezo wa kusema lolote juu ya ripoti hiyo dhidi ya maamuzi ya Baraza lako tukufu, kwani ninajua fika kwamba maamuzi ya chombo hichi yana heshima kubwa.

Mhe. Spika, wajibu wa Baraza lako pamoja na majukumu mengine ni kuisimamia serikali wajibu huu unaelezwa na kifungu cha 43 (5) cha Katiba ya Zanzibar, pia umeelezwa na kifungu cha 5 (a) (2) wa Katiba hiyo kinachohusiana na mgawanyiko wa madaraka na madaraka ya Baraza la Wawakilishi ni kutunga sheria na kusisimamia utekelezaji wa shughuli za umma.

Mhe. Spika, Baraza lako linapotunga sheria Serikali hii ya Mapinduzi inalazimika itekeleze shughuli zake kwa mujibu wa maelekezo ya sheria husika, na ni sawa na kusema tunapotunga sheria basi jukumu la serikali kuisimamia sheria hiyo kama ilivyotungwa na Baraza la Wawakilishi. Sambamba na hilo Mhe.

Spika, Baraza lako linalopitisha bajeti ya serikali na kuruhusu kukusanywa kwa mapato, kufanywa matumizi kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo, serikali hii inalazimika kufanya makusanyo hayo na matumizi kama vile Baraza hili lilivyoamua.

Mhe. Spika, nataka nisisitize kwamba Baraza lako tukufu linaporidhia ripoti yoyote kamati ya Baraza na likaagiza mapendekezo ya kamati hiyo yatekelezwe kama ilivyopendekezwa na kamati, ama hata yakifanyiwa marekebisho ya kuamuliwa na Baraza, serikali hii inalizimika kutekeleza maamuzi na maagizo ya Baraza kama yalivyo na sio kugeuka kuunda tume ama kamati nyengine ikapewa kazi ya kuichunguza ripoti ambayo tayari imeshaamuliwa na Baraza.(*Makofi*).

Mhe. Spika, Baraza kwa mantiki inayokusudia hapa linajumuisha Wajumbe wasiokuwa Mawaziri, Mawaziri na Manaibu Mawaziri, Mwanasheria Mkuu na hata wewe mwenyewe Mhe. Spika, na kwa kufahamu haja ya maagizo ya maamuzi ya Baraza utekelezwe ipasavyo Wajumbe wote hawa wa Baraza ikiwa ni pamoja na serikali wanapata fursa na nafasi nzuri ya kutoa maoni yao na maelezo kabla ya maamuzi ya Baraza kufikiwa wakati ripoti za kamati zetu zinapowasilishwa Barazani.

Mhe. Spika, kimsingi si sahihi utekelezaji wa maamuzi ya Baraza kuundwa tume nyengine kwa ajili ya kuchunguza maamuzi hayo. Wajibu pekee unaobaki kwa serikali kuyachukulia hatua maamuzi hayo kwa kuzingatia sheria; ikiwa ni pamoja na hatua za kinidhamu na hatua za kijinai, na hatimaye kutoa taarifa ya utekelezaji hapa Barazani. Taarifa ambayo itakuwa ni vielelezo vya uthibitisho na hatua walizochukua kama vile ambavyo ripoti zetu zinavyofanya na sio kuletwa pasipo na uthibitisho wowote.

Mhe. Spika, kamati yangu ilifanya kazi kwa umakini mkubwa. Iliwahoji wahusika wote wa shirika pamoja na mashahidi ikiwa

ni pamoja na kukusanya vielelezo husika, serikali katika kutekeleza mapendekezo ya Baraza haikufanya hivyo na badala yake ni sawa iliyotoa dudu mchuzini.

Mhe. Spika, kuanzishwa kwa utaratibu wa kinuni na kuitaka serikali kuwasilisha utekelezaji wa mapendekezo ya kamati mbali mbali za kudumu za Baraza hili, na kuzingatia mapendekezo ya kamati teule na maagizo ya Baraza ya kuitaka serikali ilete tena marejesho ya utekelezaji wa maagizo hayo hapa Barazani. Muda mwingi unatumika kutoa semina kwa serikali hii juu ya namna ya uwasilishwaji huo unavyotakiwa.

Mhe. Spika, serikali hii iliyojaa wasomi na viongozi wazoefu wenye uzoefu wa kusafiri mara kwa mara nchi za ng'ambu kwa kutumia fedha za wananchi wavuja jasho, haipaswi kuendelea kupewa semina ya namna ya utekelezaji wa maagizo ya Baraza na uwasilishaji wa taarifa hizo za utekelezaji, kwani tunaamini uwezo upo, ila uthubutu na utayari ni mambo yaliyokosekana katika serikali yetu kwa kipindi cha miaka mingi sasa.

Mhe. Spika, nilidhani serikali ingechukua hatua muafaka za kinidhamu kwa uzito wa makosa yaliyofanywa na watendaji wa shirika dhidi ya makosa kuhujumu uchumi. Aidha, kwa vile kamati ilifanya uchunguzi wa kina na kukusanya vielelezo vinavyojitosheleza kwa hatua hii, nilidhani serikali itachukua hatua ya kuwasilisha vielelezo hivyo kwa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ili Mkurugenzi huyu afuatilie taratibu za kufikishwa Mahakamani wahusika badala ya kuliachilia shauri hili Polisi kwa kufanya uchunguzi ambao tayari umefanywa na kamati yangu.

Mhe. Spika, wananchi wetu za Zanzibar pamoja na Wajumbe wako wa Baraza lako hili wa *back benchers*, tunaamini kwamba serikali hii bado haijawa tayari juu ya suala zima la kuwajibisha wale wote waliohusika na ripoti mbali mbali za Baraza, na matokeo yake kutafutwa namna yoyote ya kusema ili ionekane

bado wana hamu ya kutekeleza maagizo hayo huku muda ukipotea bila ya utekelezaji wa maagizo ya Baraza kama yanavyotakiwa.

Mhe. Spika, kwa mnasaba wa Shirika hili la Umeme na kwa kuzingatia maamuzi ya Baraza, baada ya ripoti ya kamati yetu na kwa kuzingatia maelekezo ya utekelezaji yasiyo na ushahidi wowote yanayokingiuka masharti ya utekelezaji wa maagizo hayo kama yalivyoagizwa na Baraza hili tukufu. Ni wazi kwamba serikali imeridhika kwa yale mapungufu yote yaliyobainika kwa kamati na kukukubaliwa na Baraza.

Sio vyema sana kwa hali hii inavyoendelea kama kwamba serikali hii ni stahamilivu sana kwa maovu yanayotendeka katika Shirika la Umeme, na mama mwema tu asiyeweza kukikata kingaja cha mwanawe bali kukikosha ijapo hakikosheki. Lakini pia amejizuia kumuadhibu hata kama mtoto huyo amekithiri katika utovu wa adabu na heshima kwa wazazi wake.

Ninataasafu kusema kwamba utaratibu huu wa serikali kwa utekelezaji wa ubabaishaji na maagizo ya Baraza sio tu yamevunjia heshima Baraza hili, bali hata hatua inayoviza maendeleo endelevu ya nchi yetu.

Mhe. Spika, naendelea kukushukuru wewe na kuwashukuru Wajumbe wote wa Baraza lako hili kwa usikivu wenu.
Naomba kuwasilisha. (*Makofi*).

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Bismillahi Rahmani Rahim.

Ninashukuru sana kwa Mwenyezi Mungu leo kwa kunipa pumzi Ijumaa ya leo na kuweza kuchangia ripoti hii ya serikali tuliyoletewa hapa katika meza.

Mhe. Spika, mimi nilishangaa na jambo moja na limenitia hofu kubwa sana jambo hilo na huwa ni kawaida yetu Mhe. Waziri yeyote anapotoa hoja basi Waziri wanakuwa wanasimama, lakini wote Mawaziri hawakusimama ilibidi nisimame mimi. (*Makofi*). Sasa hapa Mhe. Spika, hapa nilipata hoja nzito sana kuna nini? Na katika ripoti hii imetokana na miongoni mwao wao kwenye Baraza la Mapinduzi, ndio iliyotoka huko hukumu hizi kufika hapa.

TAARIFA

Mhe. Spika: Samahani Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Naomba kutoa taarifa kwamba hii si hoja, ilikuwa ni taarifa. Kwa hivyo ndio maana hatukusimama.

Mhe. Spika: Haya ni katika zile taarifa ambazo huwa tunazijadili. Kwa hivyo endelea na mjadala kwa maoni uliyonayo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, Kiswahili lugha yangu naomba kinukuu kipengee cha chini kabisa.

"Mhe. Spika, naomba kutoa hoja", ndio ilivyoandikwa humu. (*Makofi*).

Mhe. Spika, kama nimekosea kutamka Kiswahili cha Kaskazini naomba radhi kwa hilo lakini kama ilivyoandikwa humu, naomba kutoa hoja na ninavyofahamu mimi hakusema naomba kutoa taarifa, kasema naomba kutoa hoja. Kwa hivyo naomba Mhe. Waziri hoja hii bado inasimama pale pale Mhe. Waziri katoa hoja, na waliokuwa Mawaziri wasimame kuiunga hoja. Ndio hapo hoja yangu nilipoanzia hapo.

Mhe. Waziri wa Nchi (O) Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kusema kwamba hakuna haja ya mabishano, sisi ni binadamu wakati mwengine tuna mapungufu yetu. Kwa hivyo badala ya neno hoja lifutike na iwe neno taarifa. Sawa sawa.

Mhe. Spika: Ninarudia kusema tu kwamba hii ni taarifa ambayo kwa mujibu wa Kanuni zetu tunaijadili.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ninashukuru sana Mhe. Spika, kuwa kaka yangu hakuwa mbishi amekubali hoja yangu na kaunga mkono kwamba inaondoka hiyo na kuwa ni taarifa, na mimi ninakubaliana naye.

UTARATIBU

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, ninakushukuru naogopa sana chombo hiki tusije tukakigeuza badala ya Baraza kikawa baraza.

Mhe. Spika, mimi ni mwanagenzi sana katika chombo hiki, lakini kwa uelewa wangu katika kipindi hiki nilichoingia na kwa mafunzo mengi muliyotupa ni kwamba mjadala katika Baraza la Wawakilishi unaanzishwa kwa hoja na Kanuni zetu ndivyo zinavyoagiza.

Kanuni ya 48 (1) inasema

48 (1) "Isipokuwa tu kama Kanuni hizi zimeagiza vyenginevyo hakuna mjadala wowote utakaoendeshwa ila tu shughuli iliyoingizwa katika orodha ya shughuli za Baraza.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya Kanuni hii Mjumbe yeyote anaweza akatoa hoja kupendekeza kwamba suala lolote lijadiliwe katika Baraza na hoja hiyo itaamuliwa kwa kufuata Kanuni hizi".

Na Mhe. Spika, mara kadhaa kuna maneno mengine yanaendelea hapo lakini naomba niishie hapo, mara kadhaa umetuongoza

katika kujadili mambo humu ndani kwamba hatuwezi tu kuibua suala tukalijadili, kwa sababu lijadiliwe lazima lije na hoja baadaye yanakuja maamuzi.

Hakuwezi kupatikana maamuzi kama hakuna hoja. Sasa Mhe. Spika, mimi nadhani Mhe. Makame Mshimba Mbarouk alikuwa sahihi katika hoja yake ya awali. Lakini sasa serikali inapoghumiwa ikasema inaondosha neno hoja ambapo bila shaka wamekaa wakauandaa kwa makini wenyewe, sasa ikatwambia ni taarifa. Taarifa haijadiliwi Mhe. Spika, na wewe huwa unatwambia taarifa tuulize maswali, halafu tuondoke.

Sasa hapa panataka na maamuzi mwisho na muongozo wako mara zote huwa ukitwambia Mhe. Spika, ili tupate maamuzi panahitaji iwepo hoja mbele ya Baraza. Naomba muongozo wako Mhe. Spika, utwambie nini kiliopo mbele ya Baraza.
Ahsante sana.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe tumekubaliana hapa kwa mujibu wa Kanuni zetu, nikiangalia Kanuni ya 47 inaeleza mambo ya kujadiliwa kuanzishwa kwa hoja, lakini ukiangalia na Kanuni ya 44 inayohusu taarifa ya serikali inaeleza pale, kwamba taarifa ya aina hii ya serikali basi nayo tutaijadili.
Ni kweli kwa jambo ambalo tunategemea hatimaye tutoe maamuzi basi itakuwa ni hoja.

Sasa mimi ninadhani alichokisema Mhe. Waziri kwamba anatoa hoja kuhusu taarifa hii aliyoitoa madhumuni yake anaomba Baraza hili lijadili. Na ukiangalia Kanuni ya 44 ndio inatueleza sasa kwamba Wajumbe wajadili baada ya kumpatia nafasi Mwenyekiti ambaye Makamo Mwenyekiti amekuja kwa ajili hiyo, na Wajumbe wengine sasa wapate nafasi ya kujadili ambayo ndio kazi inayoendelea hivi sasa.

Basi mimi nadhani isilete matatizo, tuendelee kujadili kama inavyoelekezwa na Kanuni zetu na hatimaye tuone utekelezaji

huu wa serikali unatosheleza au laa, ambao mwisho nitawahoji Waheshimiwa Wajumbe namna mulivyopokea, mafungu yote au sehemu fulani kwamba utekelezaji wake unatosheleza au hautoshelezi, mutaelekeza serikali vyenginevyo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, ninashukuru kwa muongozo wako niliouomba na ninaelewa kuwepo Kanuni ya 44 inayozungumzia taarifa ya serikali ambayo tuliifanyia marekebisho kama sikosei mwaka juzi kuingiza kipengele hiki.

Lakini kama ulivyosema punde Mhe. Spika, kwamba mwisho utatuhoji kuhusu ama kuipokea yote hii au sehemu ya utekelezaji wa yale ambayo humu ndani. Sasa mara nyingi utaratibu unaotuuliza ni kwa msingi wa hoja, ndio ninapata matatizo kwamba kama hii si hoja ni taarifa, yale maamuzi yetu Mhe. Spika, mwisho yatakuwa yamejengwa kwa misingi gani? Kwa sababu ni tofauti na taarifa tu ambayo kwa jumla serikali imeamua kuja kutuarifu Wajumbe juu ya jambo fulani na mwisho tunaipokea taarifa ile, lakini linapotokea jambo ambalo limeanzia ndani ya Baraza likapelekwa serikalini, serikali sasa inaripoti juu ya utekelezaji wa maamuzi ya Baraza na Wajumbe wako tunategemewa tuafiki kwamba tumekubaliana na hoja kwamba tumeridhika na utekezaji wa serikali au laa.

Sasa katika hali kama hiyo kidogo Mhe. Spika, napata tabu wakati utakapokuja kutohoji tutakuwa tunaamua nini? Naomba bado muongozo wako Mhe.Spika, katika hili.

Mhe. Spika: Nafikiri sina muongozo mwengine zaidi ya kwamba tuendelee kujadili na hatimaye Wajumbe mutaamua jambo gani ambalo utekelezaji uliowasilishwa hapa umetosheleza na jambo lipi ambalo kwa maelekezo mutakayotoa linahitaji kufuatiliwa zaidi na hatua kuchukuliwa.

Mimi nafikiri tuendelee kujadili kama ilivyo na hatimaye nitawahoji Waheshimiwa Wajumbe namna gani munaridhika na

taarifa hii iliyotolewa na serikali juu ya utekelezaji wa maamuzi ya Baraza yaliyofanywa huko nyuma. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk endelea.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, mimi nakubaliana na wewe kwa vile nimegundua kifungu hapa cha Wajumbe wanaweza kujadili na kutoa maoni yao kuhusu yao kuhusiana na taarifa ya serikali iliyowasilishwa.

Mimi naondoka hapo sasa lakini naomba Mhe. Spika, *hansard* isomeke kama nikubalike kama ni mwanasheria na mimi vile vile katika wanasheria.(*Makofi*).

Mhe. Spika, nimeiona taarifa hii lakini taarifa hii siku zote hupiga kelele munatuletea *time* ambayo hapo kwa hapo, si tatizo wenye akili tutasukuma hivyo hivyo ili tumalize wakati.

Mhe. Spika, taarifa hii nimegundua kuna mambo mawili ya kisheria. Jambo la kwanza nimegundua kuwa sheria aidha PAC waongeze sheria, kama ingekuwa ni hivyo zipo sheria ambazo zingeongezwa basi leo tusingejadili taarifa hii. Nimeona hilo kwanza kwa mujibu wa sheria, mimi kichwa changu kimenieleza hivyo. Lakini kwa nini nikasema hivyo. Taarifa ya kamati iliyoundwa imeamua imeelekeza serikali na wao imepokea na imeamua na imetekeleza. Sasa hapo ndio ninaanza kuchanganyikiwa Mhe. Spika. Sasa nikamate vipi nina kitabu cha kamati na taarifa ya serikali.

Niseme serikali ndio yenye mikono mirefu kwa mujibu wa taratibu na ndio hasa yenye sheria serikali. Kwa kuwa PAC haina sheria ya mikono mirefu kiasi hicho na ndio maana ikabidi tukakaa tena na tukaletewa tena taarifa, naomba sana Mhe. Spika, maoni yangu kwa kupitia wanasheria wa Baraza hili waangalie sheria watakayowapa PAC itakapogundua mambo aina kama haya basi itafutwe sheria ya kuweza kutoa hukumu ya

kupeleka katika chombo ambacho kitamtia mtu hatiani moja kwa moja.

Naomba hilo Mhe. Spika, nipokewe kabisa kwa mawazo yangu na liangaliwe na wanasheria itafutwe njia hiyo ya kuweza kufanya mambo kama hayo. Tukiwa na sheria hizi Mhe.Spika, basi sidhani kama kutatokea na ubadhirifu mwengine wowote katika idara za aina yoyote ambayo husika. Hilo ndio katika maoni yangu.

Lakini la pili Mhe. Spika, nishukuru serikali na Wajumbe wanikubalie kwa sababu moja au mbili.

Ni ripoti ile ile yetu sisi kama hamjui basi nawaambieni, hii ripoti hii. Kuna kama maneno tu hapa yamebadilishwa tu, lakini ripoti ni ile ile tu nikiiangalia hasa na ndio maana asubuhi Mjumbe mwenzangu akaanza kupingana nayo hii, ikawa ripoti tulisemea kamati, lakini mfumo mzima ni ule ule. Kwa mana hiyo ina maana mambo yote yaliyotafutwa kwenye kamati ndio haya leo. Lakini serikali imefanya uamuzi mmoja, wao wametoa hukumu kwa mujibu wa sheria, kwa sababu serikali ina vyombo vyake vya sheria, imetoa hukumu ndio maana yake Mhe. Spika, ndivyo nilivyoona mimi humu.

Sasa mimi Mjumbe sina kifungu cha kukata rufaa, Mhe. Spika, sina kifungu cha kukata rufaa cha kuipinga hii, sisi tutapinga bure tu hapa, nawaambia Wajumbe wenzangu tutaipinga bure, kwa sababu hukumu tayari kwa mujibu wa sheria, wanasheria wapo wataniambia kwamba nakosea, naomba wanifahamishe sio vibaya.

Mhe. Spika, naamini Mhe. Spika, unakuna kichwa leo kwa sababu nakupa vitu vikali na ndio ilivyo Mhe. Spika, ndio kupea huko ni *UNDP* hiyo sio mimi. Mhe. Spika, hukumu imeshatolewa tayari na serikali mimi sipingani nayo kabisa, kwa sababu nikisema nipinge basi nitafute kifungu chengine cha

sheria, itakuwa tayari mimi naingia makosani, kwa sababu sio mkata rufaa mimi.

Kwa hivyo Mhe. Spika, niseme tu nilifikiria kuwa ripoti hii leo nitaambiwa hasara ambazo zilizoipata serikali kwa kupitia *ZECO* ningeainishiwa humu, lakini sikuona kabisa kama kuna kasoro kubwa iliyotokea katika *ZECO* hii sijaona mimi na ndio maana nikasema jamani nitakuwa mgumu sana mimi hii ripoti. Nitaikubali kiaina yake na nitaikataa kiaina yake.

Mhe. Spika, kuna mambo mengi tu tumetajiwa humu; waliopewa onyo mimi nakubaliana nalo ndio binadamu, makoseo yamo ya hapa na pale madogo, hilo mimi sina tatizo nalo. Lakini kuna mambo mengine utakuta anaachiwa askari. Mhe. Spika, katika kifungu hiki ambacho kilichoainisha hapa kesi za Pemba kuachiwa askari mpaka leo hii sijui ni muda gani na ndio maana nikawaambia Waheshimiwa Wajumbe tuwe makini sana katika kuchangia ripoti hii, kwa sababu tayari imeshatubana kwa upande mwengine kabisa, kama mwenye kichwa ataona basi ataungana na mimi. Kweli nakubaliana na Mheshimiwa katika ukurasa wa 3 kuhusu maelezo ya serikali kuhusu hoja hiyo ya kuwa serikali inakubaliana na mapendekezo yaliyotolewa na Baraza tukufu na imechukuliwa shirika kuliarifu Jeshi la Polisi kuanza kuchukua hatua. Ndio sheria hiyo nakubaliana nalo, ndio maana nikawaambieni itizameni vizuri hii taarifa ilivyo.

Mhe. Spika, mimi nakubaliana na hii taarifa kwa haya ambayo waliotoa hukumu nakubaliana nayo kabisa kwa asilimia 100. Babu Juma Duni usishangae kwa sababu wewe hujui hayo, ndio maana nikasema kwamba tutafute sheria ambayo ni ya kujenga vizuri katika kamati zetu ili tufike pahala pazuri.

Mhe. Spika, kuna mambo mengine sisi viongozi wa juu kuanzia Marais huko juu. Rais Mhe. Spika ana uwezo wa kumtuma meneja wake, mkurugenzi wake au katibu wake na akampa amri na ikabidi itekelezwe ile amri, hili suala tunalielewa. Sasa

ukitizama ripoti hizi na wao wamo Marais wetu wanawatuma hawa watendaji wetu, mameneja wetu, ikiwa wakurugenzi wetu, ikiwa katibu wetu wamo humu. Sasa mimi sioni hilo la kutoa amri Rais kuwa leo kanitilie umeme nyumbani kwangu likawa tatizo hata siku moja. Mhe. Spika, suala hili tuliangalie vizuri, tatizo lake linakuwa vipi litaonesha hapa.

Mhe. Spika, humu kuna watu ambao wanabadilisha risiti, hawa mimi sijakubaliana nao kabisa kwa sababu hizi risiti kuzibadilisha na ndio maana nikasema sioni *amount* ambayo inaonesha hii kasoro ya kupoteza fedha katika risiti hizi, basi ningeona raha sana Mhe. Spika, tungeoneshwa shirika hili hasa mapotezo ya fedha ya mabilioni kadhaa basi hii ingekuwa ni ripoti tamu sana leo hii. Hata na ile ripoti ya *PAC* baadhi ya maeneo mengine sijaoneshwa au pengine yamo lakini kwenye ripoti hii haikutiwa sijui sababu gani, lakini wenyewe wapo watakuja kuangalia.

Mhe. Spika, hukumu imetoka hapa kwenye hii hoja nambari 2 inasema, fedha za malipo kuingizwa na nani. Sawa huyu mwanamama keshachukuliwa hukumu hiyo na ndio imekuwa basi, kwa maana hiyo uchunguzi unaendelea kwa taarifa nilizopewa hapa, na hapa atatakiwa Mdhibiti kitu kama hiki naona. Mhe. Spika, ningeuliza kwamba hii ni kweli? Kwa sababu nani anayejua ni ukweli ni polisi, lakini hapa hakushirikishwa polisi. Naomba Mhe. Spika, anisaidie Mhe. Waziri hapa kwa nini sheria hiyo ya polisi ili kuona uhalali wa hili jambo linalofanyika kisheria, lakini onyo kapewa, sawa tunaendelea.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa sita hapa amesema kuwa kuwepo kwa makisio ya aina mbali mbali kwa wateja. Mhe. Spika, hili ni kweli lipo na linafanyika na nimwambie Mhe. Waziri kwa hapa azidi kuimarisha sana kwa sababu hiki kitu ni kweli kinafanyika, na ndio maana wananchi wanapiga kelele. Suala la uungwaji wa umeme kinyume na utaratibu. Mhe. Spika, suala

hili ni tatizo sugu sana, kwa sababu wanaonewa wale wanyonge, haonewi yule ambaye ameunga umeme. Aliyewaungia umeme haonewi, anaonewa mnyonge na kwenda kung'olewa mita zake na kalipa faini kubwa ya shilingi milioni 1 au sijui shilingi milioni 3 wanakuwa wanalipa. Mhe. Spika, naomba tuwakomoe hawa waungaji, kwa sababu yule haujui, kwa sababu yule aliyeungiwa kila anayemuona basi anamuona ni mfanyakazi tu wa shirika lile. Naomba sana Mhe. Spika, suala hili liangaliwe vizuri sana, hawa waungaji kwa kweli mimi sijafurahika nao.

Mhe. Spika, nikirudi tena hapa katika ukurasa huu wa 9, unasema;

"Serikali inakiri kwamba lipo tatizo la baadhi ya watendaji wa shirika ambao sio waadilifu huwaungia umeme wateja kinyume na utaratibu uliowekwa na shirika kwa maslahi yao binafsi. Hivyo, shirika limeshaliandikia Jeshi la Polisi kuanza uchunguzi wa kina kwa wale wote waliotajwa katika ripoti ya PAC kuwa wameungiwa umeme kinyume na utaratibu na kuwataka watu hao kuwataja watu waliowaungia umeme huo. Baada ya uchunguzi hatua za kisheria zichukuliwe kwa watakaobainika wana makosa".

Mhe. Spika, hapataki tochi hapa. Mimi naona kumuweka polisi hapo ni sawa, lakini naona tutachukua muda mrefu sana uhalifu unaendelea, wale wanakuwa wanawataja, kama mimi nimeungiwa na Juma au na fulani, hayo majina yapo wanakuwa wanatajwa. Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Waziri ni vizuri kuwapa polisi lakini tutachukua muda mrefu kwa suala kama hili, ubadhirifu unaendelea na unazidi kuendelea.

Mhe. Spika, kama nilivyosema mwanzo kuwa serikali imeshatoa hukumu ya mambo ambayo iliyoyaona, wengine wamepewa onyo na wengine wamebadilishiwa ofisi. Lakini sijamsikia mtu humu katika ripoti hii waliolipa fidia, kosa la mtu kufanya jambo ambalo limekubalika humu kupewa angalau kosa la kuwa arudishe aidha zile pesa au arudishe hizo gari zilizotolewa

kinyume na utaratibu, sijaona na ndio maana kwanza sheria inasema kuwa imepewa Mdhibiti ili aone uuzaji huo umefikia wapi.

Mhe. Spika, nilitegemea mimi kuwa ripoti hii itajaa sana hukumu ambayo kitu fulani tumeshafanya, kitu fulani tumenyang'anya, kitu fulani ambacho fedha zimerejeshwa na tumefanya hesabu ya risiti ambazo zimepunguzwa fedha tumefanya ni kiasi kadhaa ni bilioni kadhaa na hizo fedha nusu tumeshasema zilipwe na zimeshalipwa nusu. Ningefurahi Mhe. Spika, kama ningepata lugha kama hii. Lakini bado inaonesha ndio kwanza inaanza upya, ndio maana nikasema Wajumbe tuwe waangalifu sana na ripoti hii, ingekuwa mmeiangalia vizuri ripoti hii kwa utaratibu Mhe. Spika, inaonesha bado hukumu haijakamilika, iko katika utaratibu wa kutaka kukamilishwa hukumu hii.

Mhe. Spika, nimalizie kwa kuwashukuru sana mameneja wawili hawa wa umeme wa Pemba na wa Unguja nawashukuru sana. Nitoe ushauri wangu kwao kuwa wawe waangalifu sana. Kwa sababu unajua Mhe. Spika, lile shirika ni kubwa sana, lina majungu mengi sana na serikali mulione suala hili kabisa, kwa sababu mtu anavyofanya kazi vizuri hakosi kupewa majungu na lazima utapewa majungu tu, lakini kwa kazi nyengine ni nzuri na miradi imetekelezwa vizuri na ndio maana wafadhili wametuletea tena fedha na wameturudishia miradi iendelee. Hilo ni suala moja kubwa ambalo nilipongeze sana, ambapo ilikuwa ni lazima niliseme. Tumekwenda na awamu nyengine sasa hivi ya vijijini kufanya *service* na mambo mengine pamoja na kusaidia vijiji kuusogeza umeme, nilisifu sana suala hili Mhe. Spika, nizitoe shukrani zangu za dhati ni lazima nilisemee hilo.

Mhe. Spika, ndio maana mimi nilikuwa nasema kumbe hakukuwa na wizi wa mabilioni ya fedha, ni makosa madogo ya kibinadamu, sote binadamu tunakosea Mhe. Spika, mambo madogo madogo haya. Ndio, ni makosa madogo madogo ya

kibinadamu, ni lazima tuseme. Nawashukuru sana Wajumbe kumbe wananifahamu sana Kiswahili changu, wananifahamu sana tu. *(Makofi).*

Mhe. Spika, hata sheria vile vile ina uangalifu wake jinsi ambavyo lile suala ulivyolifanya dogo na kubwa na hatia ikakutia wewe na udogo wako ulilokuwa nalo lile kosa ulilolifanya, na kosa kubwa ukatiwa hatiani kwa ulilolifanya.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, niseme kwamba Waziri muhusika na eneo hili namuomba sana, pale kuna matatizo ya kiubinadamu ya kuchomeana utambi, fitina, majungu na kadhalika na ndio walivyo binadamu Mhe. Spika. Hata mimi Mhe. Spika, unafikiria wengi wananipenda katika dunia hii, wengine hawanipendi wananichukia wanasema wanavyotaka wenyewe, lakini kwangu mimi nafanya chuki mbolea. Kwa mimi nilivyojiwekea naona kama ni bustani tu, mtu aseme vyovyote wala sijali, najali kile nilichokizungumza mimi, ninachokifanyia kazi mimi kwa mujibu wa utaratibu. Hiyo imo na ndio shirika hili kulikuwa na mambo kama hayo.

Mhe. Spika, hebu tizama katika kipindi cha nyuma na hiki cha sasa hivi tizama hali halisi inavyokwenda kazi zinafanyika, wananchi wanasaidiwa umeme kwa njia za mikopo *Alhamdulillah* na vifaa vinasogea kwa wananchi, ndio ilivyo Mhe. Spika. Kwa hivyo, suala hili niliona niseme kwamba Mhe. Waziri anayo ndogo tu ya kusawazisha na kuweza kuifanya hali halisi na kuipanga mipango yake vizuri kwa kupitia bodi yake, vitengo vyake husika na kuifanya mahiri sana.

Mhe. Spika, muda wenyewe hautoshi, unajua leo Ijumaa watu wengine hapa wamewekwa waende wakahutubu, kwa hivyo nisichukue muda wako mrefu sana ili niweze kukuambia Mhe. Spika, kwamba taarifa hii mimi naikubali kwa asilimia 100 kama nilivyosema. Waliopewa adhabu hizi naziunga mkono kwa mujibu wa taratibu wa taarifa za serikali, na nimeamini

niliwaambia kuwa zimetoka wapi, ni kwenye Baraza la Mapinduzi kama nitakosea naomba radhi. Imeanzia hukumu kwenye Baraza la Mapinduzi likiongozwa na Rais, sasa siwezi kumkosoa Rais mimi hata siku moja, Dk. Shein kusema kuwa hafai kutoa hukumu. Mwanasheria siku hiyo alikaa kwenye kiti wakasema sawa, pitieni adhabu hizi, sasa mimi itakuwa vibaya sana Mhe. Spika.

Mhe. Mjumbe Fulani: Utaukosa Uwaziri wa Kilimo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Hapana, Uwaziri wa Kilimo nipewe tu. *(Vicheko/Makofi).*

Kwa hivyo, ndio nikasema Mhe. Spika, kuwa mimi niikubali tu. Tena namshukuru sana Mhe. Rais na *cabinet* yake yote ya Baraza la Mapinduzi kwa kuona hukumu hizi zinastahili sifa ya kupewa, na waliopewa onyo naomba sana wakubali onyo hilo, wasinune, wafanye kazi kwa umahiri kabisa, wasimamie kazi za watu, wasimamie kazi za wavuja jasho na kuweza kutekeleza lile jambo ambalo lililokuwa mbele kwa wananchi.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha ripoti hii.

Mhe. Asha Bakari Makame: *Bismillahi Rahmani Rahim*. Mhe. Spika, kwanza niipongeze sana serikali kwa kuchukua hatua ambazo baadhi yake zimeainishwa humu, lakini Mhe. Spika, nitaiomba sana serikali sisi ndio watetezi wa wananchi Mhe. Spika, sisi ndio tutakaoipeleka serikali pahala pabaya, kama hatukuwa wakweli katika mambo yetu ambayo yametupelekesha kuingia humu kwenye Baraza lako tukufu Mhe. Spika, pamoja na kwamba baadhi ya mambo serikali imechukua hatua lakini bado.

Mhe. Spika, ni lazima tuwe wakweli na ni lazima tuisaidie serikali, kama hatukuisaidia serikali sisi tutawajibika hata kwa Mwenyezi Mungu, kuikosoa serikali sisi ndio wajibu wetu, sio

kubabaisha. Mimi nashangaa sana, samahani sana Mhe. Spika, baadhi yetu ni wanafiki. Mimi nasema kwa *haqqi lillahi*, na siku zote nasema na katika Baraza hili siku zote nitasema kwamba uongo siusemi ukweli nitausema. Makusudio na dhamira kubwa ni kuisaidia serikali yetu anayoiongoza Rais wetu Dk. Shein, kama hatukusema ukweli ndani ya Baraza hili tukatia gati gati kwa manufaa ya mtu binafsi Mhe. Spika, basi hatutokwenda. Mimi nasema bado tuwe waadilifu, tuikosoe serikali kwa lengo la kutaka serikali yetu iendeshe shughuli zake kwa ufasaha na ufanisi, na wananchi wetu wajue kwamba serikali yao inawatendea haki. Tusikae Mhe. Spika, humu muna mambo mengi sana.

Mhe. Spika, kuna suala humu fedha za malipo ya kuingiziwa umeme, samahani Mhe. Spika, kuingizwa katika *account* ya mtendaji wa shirika ndugu Zakiya Juma Azani. Mapendekezo ya Kamati ni kwamba hatua za kisheria na za kinidhamu zichukuwe dhidi ya muhusika. Ukija kwenye mapendekezo kwa serikali kahamishwa sehemu ile kapelekwa wizara ile ile kule kule. *Are we serious?* Maana yake niseme hiki kipengele kimoja tu *are we serious*? Kamati imeona, imechunguza na imetoa mapendekezo. Jamani tuache udugu, tuache mapenzi na tuache mambo ambayo hayatoisaidia serikali. Mhe. Spika, nayasema haya kwa dhamira nzuri, mtu atakayekaa akatafsiri maana yake tunatafsiriwa vibaya huko nje, ni kwa sababu wao hawamo humu ndani hawajui taratibu na sheria tunazoziendesha humu kwenye Baraza. Kwa hivyo, naiomba sana serikali, nasema kwa uchungu.

Mhe. Spika, Kamati inapotoa maagizo basi lile la kuonekana kwamba kweli hili limekithiri Mhe. Spika, tusioneane haya kabisa. Mimi nasema tena kusema uongo mwiko, kusema ukweli daima ni kiapo changu cha Chama cha Mapinduzi. Mimi nimeingia humu kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi na ndio chama changu kinavyoniagiza hivi. Hebu tuwe wakweli Mhe. Spika. Kuna wengine humu humu wakimganda mtu hata kosa hana watasema, lile la ukweli hawalisemi. Mhe. Spika, naomba

sana tuwe na imani na tuwe tumeunda wizara ya utawala bora, miongoni mwa shughuli zetu ni lazima tuwe na imani na utawala bora ili wananchi wetu waone kwamba kweli Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanaitendea haki serikali yao pamoja na wananchi wao.

Mhe. Spika, mimi ndio ukaniona sijagusa nimekisoma kipengele kimoja tu. Mimi nasema kama tutakwenda hivi hivi *wallahi* Dk. Shein hatumsaidii. Tumsaidie Dk. Shein jamani, kuikosoa serikali na ukaiambia ukweli sio kwamba huipendi serikali yako, hebu tumsaidie Rais wetu jamani, hivi hatujamsaidia bado Mhe. Rais Mhe. Spika. Tumsaidie kwa lengo la kwenda sambamba katika mihimili mitatu tuliyonayo na muhimili mkubwa zaidi ni huu wa kuiambia serikali ukweli na kuchukua hatua. Hayo mamilioni ya fedha yaliyopotea kwenye taarifa hii ndio tunamsaidia Dk. Shein kweli, mimi naona bado hatujamsaidia. Nasema Mhe. Spika, nisieleweke vibaya, nasema kwa nia safi, na ninasema kwa kuipenda serikali yangu kwa sababu mimi ndio mtawala, hajatawala mwengine mimi CCM ndio mtawala katika serikali hii, sitokubali chama changu cha CCM ambacho kimeleta Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar katika utawala wake kuyumbishwa sitokubali. Mhe. Spika, tuwe wakweli, tumsaidie na tuwasaidie wananchi wetu.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naiomba serikali isitutafsiri vibaya, sisi lengo letu kubwa ni kusaidia na kutekeleza malengo ambayo tumejipangia kwa kila mwaka kutekeleza wajibu wetu katika Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar. Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, mimi siungi mkono hoja hii. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nichukue nafasi hii kuwashukuru kwa kuendeleza shughuli zetu kama zilivyopangwa. Dakika zilizobaki ni tano, hivyo hazitoshi kumuita Mhe. Mjumbe mwengine kwa ajili ya kuchangia.

Waheshimiwa Wajumbe, kuna tangazo moja. Mhe. Mwenyekiti wa UWAWAZA, ameniomba niwatangazie Waheshimiwa Wajumbe wanawake kwamba mara baada ya kuondoka humu ndani wakutane katika chumba chao cha kawaida, ili wakaendelee na mafunzo yao ya kujiongezea uwezo ambapo leo watakuwa na mtaalamu kutoka Marekani atapenda sana mtaalamu huyo kuonana na Waheshimiwa Wajumbe hao. Kwa hivyo, tunaombwa sana Waheshimiwa Wajumbe wanawake tusiache kuhudhuria mkutano huo na mtaalamu huyo.

Basi Waheshimiwa Wajumbe, baada ya hayo sasa niakhirishe kikao hiki hadi saa 11:00 jioni.

(Saa 6:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano Yanaendelea)

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii jioni hii ya leo ni kawa mchangaji wa mwanzo juu ya hoja iliopo mbele yetu ya maelezo ya serikali kuhusu hoja zilizotolewa na Baraza lako hili kwa serikali.

Mhe. Spika, kwanza nashangaa kidogo juu ya kuletwa kwa taarifa hii au hoja hii. Mhe. Spika, huko nyuma kulikuwa na Ripoti ya Kamati Teule, ripoti ile iliwasilishwa Barazani hapa na kamati yako na Baraza likatoa mapendekezo yake kwa serikali, ili yafanyiwe kazi na baadaye serikali ilete namna ilivyoyafanyiakazi.

Kwa bahati nzuri au mbaya ripoti ile ya serikali ilipowasilishwa Barazani hapa wajumbe wako au Baraza lako hili liliikataa na serikali iliahidi kwenda kuifanyia kazi na kukaa tena na kamati

ile, ili irudi itoe tena namna ambavyo sasa imeifanyiakazi kwa sababu pale mwanzo ilikataliwa. Lakini Mhe. Spika, jambo la kusikitisha hadi leo hii inaletwa taarifa hii nyengine ile ya mwanzo hakuna kilichoendelea.

Sasa Mhe. Spika, mimi napata tabu kidogo kwamba tutawezaje sasa kuamini kama kweli serikali huwa inakwenda kuyafanyiakazi yale mapendekezo ya Baraza yanayotolewa hapa. Hali hii inaoneshwa kwamba ikiwa ile ya mwanzo imeletwa na yametupiliwa mbali yale mapendekezo ambayo yaliletwa, yaani hatukuridhika na kile ambacho walikifanya kama Baraza, hivyo tuliitaka serikali irudi na ikafanye mengine na baadaye waje watueleze namna ambavyo wamefanya. Lakini hakuna ambacho kimeendelea hadi hivi sasa.

Kwa kweli hili ni jambo la kusikitisha sana Mhe. Spika, kwa serikali yetu hii kuwa inapewa agizo na Baraza inashindwa kuyafanyiakazi. Lakini leo inatuletea ripoti nyengine hii namna waliyoyafanyiakazi mapendekezo ya Baraza kuhusu Shirika la Umeme. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nadhani ni vyema serikali ikatuambia kweli iko *serious*, ikiwa kile ambacho tumeiagiza bado haijakitekeleza mpaka leo, badala yake leo inatuletea kitu chengine cha maajabu ajabu mimi nasema, hivi sisi tutaamini vipi kama kweli wanayatekeleza haya.

Kutokana na hali hiyo, ninaiomba serikali kupitia kwako Mhe. Spika, kwanza ingetuletea ile ripoti ya mwanzo ya Kamati Teule namna ambavyo wameyafanyiakazi, kwa sababu mapendekezo mengi ambayo yamo mule Mhe. Spika ah! Tunayaona humu hayo maagizo mengine ambayo yalikuwa yametolewa na wala watu hawana habari na wenye kujenga wanaendelea kujenga na wengine wanafanya mambo mengine na zaidi ni kulijejea Baraza ah! Nyinyi ni wapiga debe tu ndio kazi yetu na wala msituambie

kitu. Kwa hivyo, nendeni huko kajikusanyeni museme mukimaliza hakuna kinachofanyika.

Sasa kwa wakati mwengine tunaanza kuamini kwamba haya ambayo yanasemwa pembeni inaonekana ni kweli serikali haiyatekelezi na inaonekana kuna chembe ya dharau juu ya chombo chako hichi Mhe. Spika.

Mhe. Spika, mimi nasikitika sana na kwa kweli niwaombe Wajumbe wenzangu kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba hatuna haja ya kuchangia kwenye ripoti hii, nadhani ni vyema tukawaambia serikali wachukue wenyewe hii na badala yake watuletee ile ya kwanza tuone namna ambavyo wamefanyia, ili tupime na halafu tuangalie. Sasa hichi ambacho wanatuambia leo tuamini kwamba kweli wamekifanyia kwa hayo ambayo wameyaonesha wameyafanya na yale ambayo wanaahidi wataendeleza kuyafanya na hatimaye tuweze kukubali kwamba haya nayo watayafanya.

Kwa kweli Mhe. Spika, tukiendelea katika utaratibu huu sisi Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako hili tunaonekana kule kwa wananchi kama hatufanyikazi, yaani ile kazi yetu ya kuisimamia serikali kwa mujibu wa Katiba tunaonekana kwamba hatufanyi, kwa sababu kama kuisimamia serikali ni kuipa maagizo na kuyatekeleza, sasa kama serikali haitekelezi na kazi yake itakuwa inatuletea ripoti tu hizi juu ya meza na sisi tupokee ripoti hizi tuseme sawa na wala haiwezekani.

Vile vile Mhe. Spika, kama utakumbuka Waheshimiwa Wajumbe wako chombo hichi kilikataa yale maelezo ya serikali juu ya utekelezaji na hii ni aibu, lakini serikali inaonekana kama imekaa kimya haihisi kwamba hichi ni chombo cha wananchi kimekataa kile ambacho imekileta, maana yake irudi na ifanye haraka ituletee tena kwa ajili ya kuona ule utekelezaji ambao wameufanya, lakini jambo la kusikitisha Mhe. Spika, mpaka leo kimya.

Kwa hivyo, naiomba sana serikali kupitia kwako Mhe. Spika, kwanza itupe jawabu la lile la mwanzo wamefikia wapi, kwa sababu kwa mujibu wa makubaliano ambayo tulikubaliana kwa siku ile ni kwamba Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais aliahidi kwenda kukaa na Kamati, ili kwenda kupitia kifungu baada ya kifungu, kwa ajili ya kuona namna ya ule utekelezaji utakavyokuwa, kwa sababu anasema sisi katika ile ripoti tumewachanganya mno.

Ingawa wao wenyewe hiyo serikali ndani ya Baraza hili imo na tunapopitisha sote tunakuwa tunakubaliana kwa pamoja hapa, yaani tunaitikia kwa pamoja hapa na tunaikitia ndio. Lakini inasikitisha sana ikirudi inakwenda kukaa pembeni kama serikali tu peke yake na kusema aa! Hili halitekelezeki au halifanyiki ama hatuwezi, sasa hapa kwa nini wanakuwa wanakubaliana, kwa nini hapa ndani ya Baraza hili wakubali halafu watoke wakakae pembeni waseme hili hatuwezi kulifanya.

Mhe. Spika, nadhani ni vyema wangejenga hoja humu ndani ya chombo ambacho kimetoa agizo na wao wamo, kwa sababu tunaposema Baraza linajumuisha na serikali, yaani serikali imo humu kwani mawaziri wamo humu ambao ndio wenyewe serikali. Sasa wanaporudi wakenda wakakaa kama kikundi cha watu wawili au watatu na halafu wakatuambia hili halitekelezeki maana yake nini? Kukidharau chombo hichi au kitu gani.

Mhe. Spika, makubaliano ambayo tumekubaliana ni kwamba turudi tukakae pamoja. Lakini nakumbuka mimi ni mara moja tu tena muda wenyewe haizidi hata saa moja na ilikuwa ni siku ya Ijumaa, kwamba Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ametuletea maagizo kuwa tukutane na kamati na mimi ni mjumbe wa ile kamati, basi tulikutana ukumbi wa juu hapo nafikiri ilikuwa imeanzia kama saa 5 na siku ya Ijumaa unajua Mhe. Spika saa 6 lazima tukawahi kusali.

Kwa hivyo, tukaanza kujadili, lakini tumeanza ile hadudi rejea moja tu hatukuimaliza muda umekwisha na ikabidi tuondoke na tukakubaliana kwamba tutapanga siku nyengine, lakini mpaka hii leo Mhe. Spika kamati ile haijaitwa na nimejaribu kumuliza Mwenyekiti wangu nilifikiri labda mimi nimefichwa, kwamba kamati imeitwa lini na aliniambia hatujaitwa na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais yupo atasema kaita lini kamati kwa ajili ya kukaa na kujadili yale, ili tuone namna ya utekelezaji utakavyokuwa.

Kwa kweli ni jambo la kusikitisha sana Mhe. Spika, kwamba Baraza lako hili linakaa na kutoa maamuzi au maagizo kwa serikali, lakini serikali haiyatilii maanani inayatupa au inayaweka kando. Mhe. Spika, chombo ni cha wananchi na sisi tupo hapa kwa ajili ya wananchi na hii serikali ambayo ipo pia ni ya wananchi, sasa haiwezekani kwamba panatolewa maagizo wao wadharau kiasi hichi. Mhe. Spika, nasikitika sana kuhusu suala hili. Baada ya hayo, Mhe. Spika sasa nije kwenye hii hoja ambayo ipo hapa.

Mhe. Spika, nimeangalia kwenye haya maelezo nimepata wasi wasi mkubwa sana juu ya utekelezaji. Kwa kweli serikali kwa niaba ndio ameleta Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais inaonekana iliangalia yale maeneo ambayo inapenda iyafanyie kazi juu ya ile ripoti, kwa sababu kuna maeneo imeamua kwamba iyafanyie kazi na mengine imeyaacha kabisa hata kujibu haikujibu na kitabu ninacho cha Ripoti ya Kazi Maalum, mimi nimeangalia majibu pamoja na yale ambayo yalikuwa yamependekezwa na kamati.

Mhe. Spika, Baraza lako hili likaridhia kwamba sasa haya serikali kayafanyieni kazi na baadaye muje mutujibu. Lakini ndio yale ninayoyasema kwamba serikali inaangalia kile inachokitaka ndio imejibu na ambayo haitaki basi imeacha. Kwa mfano, ukiangalia hapa Mhe. Spika kwenye hichi ukurasa wa 145 kuna mapendekezo ya kamati kuhusiana na hadudi rejea

zilizohusika, mapendekezo yale yaliletwa kwenye chombo chako hichi Mhe. Spika na Baraza lako hili likaridhia na likaamua kwamba haya ndio mapendekezo ambayo yapelekwe serikalini na serikali iyafanyie kazi.

Sasa kama serikali iliamua kuchukua baadhi ya hoja kuzijibu na kuzijibu kwenyewe mimi naona ni kwa ubabaishaji, maana yake sioni ule utekelezaji wenyewe. Mhe. Spika, tunaposema kwamba huyu tumeshampa barua ya onyo huyu maana yake ushahidi wake atuletee tuone zile barua ambazo waliwaandikia kama ambavyo sisi kwenye ripoti ile tuliweka na viambatanisho vya kuonesha ushahidi wa yale ambayo tuliyafanya.

Kwa hivyo, hatuna kinachofanyika isipokuwa unapewa maelezo tu, basi sisi kazi yetu itakuwa ni kuitia tu hapa na wala hivyo haiwezekani, tutakuwa tunaisimamia vipi hiyo serikali bila ya kujua hicho ambacho wanachokifanya. Kutokana na hali hiyo, ni lazima watuoneshe kwamba hichi ndicho walichokifanya. Kwa maana hiyo, kama hawaoneshi kwa utaratibu huu Mhe. Spika, kila siku watakuwa wanatuletea ripoti na Baraza lako hili litakuwa linazikataa, kwa sababu ripoti hazikidhi haja na inaonekana kama ni kitu ah! Kwa lazima tu tufanye na wala haiendi hasa vile ambavyo inatakiwa.

Vile vile tukiangalia kwenye ukurasa wa 145 kuna maagizo ambayo yametolewa ni mengi sana yapo karibu 11 na ukiyachambua ndio unapata baadhi ya haya ambayo yanaonekana ndio yamejibiwa.

Lakini labda niulize kuna agizo Nam. 7 Mhe. Spika kwa ruhusa yako naomba kunukuu.

> Kitabu cha Ripoti ya Kazi Maalum ukurasa wa 145 Agizo Nam. 7 linaelezea hivi:-

> "Kwa kuwa kamati imepata wasi wasi kwamba kuna hujuma imefanyika ilipelekea kukosekana kwa umeme ndani ya miezi mitatu Unguja 2009/2010. Serikali ndani ya kipindi cha miezi mitatu baada ya kuwasilishwa ripoti hii iunde tume iliyohuru ya kuchunguza chanzo na sababu zilizopelekea kukosekana kwa umeme huo na ripoti yake iwasilishwe na kujadiliwa katika Baraza la Wawakilishi na hili lilikuwa ni agizo, lakini sikuona majibu yake".

Sasa sijui imefumba macho au kurasa zilichanika ambacho kitabu Mhe. Waziri alikuwa nacho siwezi kujua, kwa kweli haya ni miongoni mwa mambo ambayo yaliagizwa.

Pia kuna agizo Nam. 8 pia naomba kunukuu Mhe. Spika.

Kitabu cha Ripoti ya Kazi Maalum Agizo Nam. 7 linaelezea hivi:-

> "Kwa kuzingatia matakwa ya Katiba serikali kupitia Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ifanye ukaguzi wa fedha zilizotumika kurejesha huduma ya umeme Unguja baada ya kuzimika na kukosekana kwa kipindi cha miezi mitatu Disembe, 2009 hadi Machi 2010".

Mhe. Spika, kipindi ambacho kilikatika umeme na umeme ule ulirejeshwa kwa gharama kubwa sana na Baraza lako liliona ni fedha nyingi sana zilizotumika pale. Kwa hivyo, Baraza lako tukufu Mhe. Spika inataka kujua fedha zilizotumika ni kiasi gani na serikali imeagizwa itumie Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali tena ndani ya miezi mitatu na walete jawabu hapa, lakini Mhe. Spika hakuna kitu na majibu haya tuliyopewa mimi sikuona hili. Sasa sijui serikali ilisahau au

ndio yale tunayosema kwamba inachagua inachotaka kujibu na isiyotaka basi na huna cha kutufanya, kwa kweli hali hii inasikitisha sana Mhe. Spika.

Pia tukiangalia kwenye ukurasa wa 147 wa ripoti ile kuna agizo Nam. 9 Mhe. Spika naomba kunukuu kidogo.

> Kitabu cha Ripoti ya Kazi Maalum ukurasa wa 147 Agizo Nam. 9 linaelezea hivi:-
>
> > "Bila ya kuathiri masharti ya Katiba Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ifanye ukaguzi maalumu na wala si ule wa kawaida wa kupita mwaka mara moja, yaani ukaguzi maalumu wa hesabu za Shirika kwa kipindi cha miaka 2009 hadi 2012".

Mhe. Spika, hili lilikuwa ni agizo na wala majibu yake sikuona humu na wala hatujapata hiyo ripoti maana hii ilikuwa ni ukaguzi maalumu, kwa maana hiyo italetwa ripoti yake. Sasa Mhe. Spika, hivi ni vitu ambavyo viliagizwa na chombo chako na serikali kwa nini haikutuletea majibu haya hadi hii leo na tena imepewa muda miezi mitatu haikusema kama imeshindwa isipokuwa imekaa kimya tu na imeletwa hii ah! Munataka hicho chukuweni, hii itakuwaje Mhe. Spika.

Nadhani niwanasihi sana Waheshimiwa Wajumbe wenzangu kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba sisi tupo hapa kwa ajili ya kutetea maslahi ya wananchi wetu na tumetumwa kazi na wananchi na wala tusione aibu kuiambia serikali kama unachokifanya sicho, kwa sababu hizi ni fedha za walipakodi Mhe. Spika. Kwa hivyo, ni lazima hesabu yake ijulikane na namna ambavyo zimetumika na ndio maana kukawa kuna maagizo haya na serikali inachelea nini kufanya haya au nini tabu ama kizito, tuko katika kulindana kama tuko katika kulindana sawa, lakini kama ni kutenda kazi kwa uadilifu basi

hivi vitu ni muhimu kufanyika Mhe. Spika, ili wananchi wakaiona ile sura halisi ya lile shirika.

Kwa kweli lile shirika linakwenda kwa hasara Mhe. Spika, kwa sababu sisi tumekwenda kwenye lile shirika na tumelichunguza kweli na linakwenda kwa hasara, lakini ukitizama sababu zipo kwa nini linakwenda kwa hasara zipo sababu za msingi kabisa ni ubadhirifu mkubwa ambao upo pale. Kwa mfano, kuna baadhi ya watendaji ambao ni wabadhirifu sana na katika ripoti yetu Mhe. Spika imeonesha, ndio maana tukatoa mapendekezo kwa serikali kwamba ifanye hivi serikali kwa ajili ya kulirekebisha lile shirika na wala hatukuandika ripoti ile kwa kumkomoa mtu.

Mhe. Spika, maana humu inaonekana kama haya majibu ya serikali yalikuwa na upendeleo fulani kwamba kuna watu fulani *untouchable* hao, ukimtaja basi humu majibu ya serikali yalikuwa aa! Huyu hakugusa chochote au hamna chochote na hao wengine wenzangu mimi akina fundi Saad ndio tumesikia kwamba tumewachukulia hatua au tumemsimamia kazi hivi sasa na hawa wengine mbona hawakuguswa, basi itakuwa hii ripoti kazi yake imeonea wale wenzangu na mimi ambao hawana mtu, lakini wale wazito au wanene hawagusiki, haiwezekani hiyo Mhe. Spika. *(Makofi)*

Nafikiri huo si utaratibu mzuri na wala hatuwezi kufanya kazi katika utaratibu huo wa kwamba akiwa fulani huyu hawezi kuambiwa na akiwa fulani aa! Huyo funga au fukuza kazi itakuwaje sasa. Mhe. Spiaka, nadhani tusiendeshe kazi kibaguzi baguzi na hii ni aina ya ubaguzi Mhe. Spika na wala hatuwezi kwenda katika utaratibu huu. *(Makofi)*

Katika hili wanaomba Waheshimia Wajumbe kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba ripoti hii tuwaachie wenyewe serikali warudi nayo. Kwa hivyo, tuirejeshe wakakae tena na baadaye watuletee majibu ambayo ni sahihi yenye kufanana na ripoti yetu tuliyowapelekea kwa sababu tumewapa maagizo basi

watekeleze. Kwa kweli hatuwezi sisi tukawa kama *rubber stamp* tunagonga tu aa! Lazima tuangalie na ripoti hii haikidhi haja. Mhe. Spika, ripoti ya serikali iliyoleta haikidhi haja ni nyepesi mno hebu waangalie kilichomo kwenye ripoti yetu katika yale maagizo ya Baraza waangalie vizuri na waone na baadaye watujibu na wala sio wachague cha kujibu kwamba hichi twende au kiache haiwezekani hilo.

Mhe. Spika, ninashangaa sana kwamba huu utendaji wa aina hii sijawahi kuona, yaani kama huu ndio utendaji wa serikali basi kazi ipo Mhe. Spika, kwa sababu mambo tunakubaliana humu kwa pamoja tena serikali imo humu badala ya kufika na kuikabidhi vyombo husika wanaunda kikundi cha kujadili mambo yale tuliokuwa sisi kama Kamati pamoja na Baraza lako tumeshaamua.

Kutokana na hali hii inaonekana kutakuwa na kikundi ambacho ndicho kikubwa sana kuliko hata chombo hichi cha wananchi na wala haiwezekani hivyo. Kwa hivyo, watu wanatizamana sura huyo hapo nani aa! Hawa wanamchukia tu huyo weka huko na wala sitaki kupitia moja baada moja na haya Mhe. Spika nikianza kuyachambua moja baada ya moja majibu ya serikali tutafika asubuhi hapa maana ninahoja nyingi juu ya hili.

Ninachokiomba kwa Waheshimiwa Wajumbe wenzangu kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba tukubaliane ripoti hii tuwarejeshee wenyewe wakakae vizuri na baadaye watuletee majibu ambayo yenye uhakika yenye macho na miguu na haya ni majibu kipofu hamna kitu ni kiwete na wala hayaendani. Kwa hivyo, Mhe. Spika, sitaki niichambue ripoti hii, isipokuwa naichukua kwa ujumla tu niwarejeshee siwezi kuiunga mkono na hata kuikubali kama huu ndio utendaji wa serikali, isipokuwa huu ni udhaifu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, chombo chako kimeunda kamati tumekwenda kwa ushahidi kabisa na kila kitu kimeletwa na ushahidi wake, badala

ya serikali kuchukua hatua kupeleka kwenye vyombo husika kinaundia kamati tena kutujadili sisi Wajumbe wa Baraza namna ambavyo tumeyapeleka haya ah! Sidhani kama hiyo ni sahihi, kwa sababu serikali imo na yenyewe ilikubali kwamba ndio ripoti hii sasa ikafanyiwe kazi, maana yake sasa tunatoa hilo agizo likatekelezwe pelekeni kwenye vyombo husika kwa nini munaunda vikundi tena vya kuanza kujadili.

Mhe. Spika, mimi nimalizie hapa kwa kuikataa ripoti hii na ninakushukuru na ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, ahsante na mimi nikuchukuru kwa dhati kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia Ripoti ya Serikali juu ya Shirika la Umeme *(ZECO).*

Mhe. Spika, nitajaribu kuzungumza kwa ufupi sana na nitakwenda kwenye baadhi ya vifungu kama viwili au vitatu. Lakini na mimi kama walivyotangulia wenzangu nianze kwa masikitiko kabisa namna serikali ilivyojipanga na kuelezea hatua zilizochukuliwa kwa wale ambao wametajwa katika Ripoti ya Kamati ya *PAC*.

Kwanza kabisa naomba niitanabahishe serikali kwa kuwaeleza kwamba wamewapa wakati mgumu sana viongozi wetu au watendaji wakuu wa serikali hii, kwa nini nasema hivyo Mhe. Spika? Nasema hivyo, kwa ruhusa yako Mhe. Spika, nataka nimuelezee Meneja Mkuu wa Shirika la Umeme nathubutu kusema kwamba ninamfahamu tena ninamuelewa, ninamjua uaminifu pamoja na utendaji wake.

Lakini tuangalie mazingira aliyopewa majukumu katika Shirika la Umeme na dhoruba alizokutana nazo, dhoruba ambazo Baraza lako hili lilifikia pahala wakajua udhaifu wa wafanyakazi wa Shirika la Umeme na wamekwenda kufanya upekuzi kwa ajili ya kujua matatizo ambayo yako Shirika la Umeme. Mhe. Spika, leo katika hii ripoti meneja amepewa ovyo, nasema tutampa ovyo,

tutamkaripia, tutamkemea tumemuonea kwa sababu tumempa watu sugu ambao hawana uaminifu. *(Makofi)*

Sasa kama serikali imeshindwa kuwachukulia hatua watu ambao wameguswa kwa namna moja au nyengine kwa ushahidi tosha ah! Jamani Meneja Mkuu atakuwa na uwezo gani wa kuweza kuwasimamia watu ambao serikali yenyewe imeshindwa kuwachukulia hatua. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ndipo pale ninaposema kwamba kuna watu uzuri wao tutaupaka matope kutokana na kutokuwa makini katika kufanyakazi zetu. Kwa kweli kijana huyu tutampotezea sifa zake na tutamfanya arudi nyuma kufanya kazi kutokana na mazingira aliyonayo.

Mhe. Spika, Shirika la Umeme kuna matatizo makubwa sana na wenzetu wameona machache tu, lakini mengi hayakuonekana. Kwa mfano, kuna makundi yanafanyakazi kwa ufisadi kwa namna ya kutaka kuwaangusha viongozi wa juu, sasa kama yale makundi hayakuweza kudhibitiwa au kuchukuliwa hatua kwa matendo yao Mhe. Spika hii ni hatari.

Kutokana na hali hiyo, ndipo tunapofika pahala leo tutampa onyo Meneja Mkuu na kesho tutasema Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwamba hafai au hasimamii vizuri kwa sababu watu wa chini sio na tunawaelewa na tayari wameshakwenda kufanyiwa kazi. Mhe. Spika, hiyo ilikuwa ndio dibaji yangu.

Sasa naomba nijaribu kutoa mchango katika hii Taarifa ya serikali. Mhe. Spika, nasikitishwa na ukurasa wa kwanza kabisa juu ya wateja kupewa risiti zenye kiwango kidogo kuliko malipo halisi waliyolipa. Mhe. Spika, wenzetu walikwenda kufanyakazi wametumia fedha za wananchi matatizo yameonekana na risiti zimepatikana, lakini leo mapendekezo kwa serikali inakuja kusema kwamba mambo haya wanaachilia Polisi wachunguze

ah! Sasa mimi nabaki kujiuliza kinakwenda kuchunguzwa nini wakati vitu vipo na tayari vimeshafanyiwa kazi na hii ni sehemu moja. *(Makofi)*

Sehemu ya Pili udhaifu wa Ripoti ya Serikali, hapa kuna kifungu kuhusu ndugu yetu Ahmed S. Yussuf, kwamba serikali imetoa onyo la mwisho. Mhe. Spika, maana yake unapozungumza onyo la mwisho ni kwamba tayari huyu mtu ameshapewa maonyo mengi, sasa kama mtu anafanya mambo ambayo hayaelekei na sisi kazi yetu ni kutoa onyo tu.

Jambo la tatu Mhe. Spika kwenye ukurasa wa 3 suala la ndugu Zakia Juma Azan. Mhe. Spika, tunaambiwa kwamba ameondoshwa katika eneo na amepelekwa kwenye eneo jengine ndio aende akatumalize kabisa, maana yake alikuwa kwenye Shirika na sasa tunampeleka kwenye wizara na huko kuna kichwa aende akakikate. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ripoti hii imefanyiwa kazi, lakini mimi naomba ninukuu kifungu cha Sheria ya Utumishi (*GO*) kifungu cha 84.

Sheria ya Utumishi (*GO*) kifungu cha 84 kinaeleza hivi:-

> "Mfanyakazi yeyote ambaye kutakuwa na mashaka juu ya ubadhirifu, suala la mwanzo anatakiwa kusimamishwa kazi na akesha kusimamisha kazi anatakiwa alipwe nusu mshahara. Lakini yakeshakufanyika hayo mawili basi anatakiwa afikishwe kwenye vyombo vya sheria kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi".

Mhe. Spika, sisi ndio watunga sheria na mimi najiuliza tunafuata sheria au tunabadilisha sheria na kama hivyo ndivyo Mwanasheria Mhe. Makame Mshimba Mbarouk angeusaidia sana Mhe. Spika.

Lakini hii ndio *GO*, kwamba mfanyakazi ameonekana na matatizo baada ya kutumiwa *GO* kifungu cha 84 tunamuondosha katika eneo moja tunampeleka kwenye eneo jengine, wakati tayari kinaonekana *physical*. Kutokana na hali hii, maana yake tuambiwe zile fedha hazikuingia kwenye *account* yake, maana yake hilo ndilo tatizo ambalo liliopo hapo kama fedha za serikali mtu zimetiwa kwenye *account* yake mara mbili na halafu bado tunamuondosha kwenye eneo moja na kumpeleka eneo jengine baada ya kuchukua hatua za kisheria, ambapo sheria zenyewe tunatunga sisi. Mhe. Spika, tunasema kwamba huu ni udhaifu wa ripoti hii.

Nikiendelea na mchango wangu kwenye ukurasa wa tano namba nane kukiukwa kwa agizo la bodi Wakurugenzi kuhusu mgongano wa kimaslahi katika ushiriki wa ndugu Hamidu Saidani Ali na ndugu Ali Abeid Haji katika *ZECO* na *GECCO* na ripoti ilikuwa ni ukurasa wa 29.

Mhe. Spika, kuna aina nyingi za wizi kwamba mfanyakazi wa serikali kutoka serikalini na kwenda kufanyakazi katika kampuni wakati wa kazi na huo ni wizi, pia akawa anatumia vifaa vya shirika kwa ajili ya kampuni na hiyo ni sehemu ya wizi. Lakini katika maelezo tumeambiwa tu, kwamba imechukua hatua ya kuwahamisha wafanyakazi hao na kuwapeleka sehemu nyengine na yule Bi Zakia angalau tumeambiwa kwamba kapelekwa wizarani, lakini hawa hata wapi wamepelekwa hatujui. *(Makofi)*

Kwa hivyo, huyu kapelekwa kwenye Wizara lakini hawa watu wengine wamepelekwa wapi hatukuambiwa Mhe. Spika. Kwa hivyo inaonekana kwamba hii ripoti ilikuwa ni ripoti ya kubanabana tu ya kutaka kutuziba macho. Mimi huwa nasikitika sana na kwa kweli kwa hali hii hatuwatendei haki wananchi wa nchi hii. Serikali kupitia Baraza lako imetumia gharama kubwa sana kwa maneno yetu ya kishamba mapesa mengi sana, kuwapa Kamati kwenda kuchunguza kwa muda mrefu na hatimae kupata vitu ambavyo havieleweki.

Mhe. Spika, tuna safari refu sana. Wananchi wengi wa nchi hii ni masikini, itafika pahala wanaweza wakatuhukumu kutokana na hali kama hii kwamba watu wanakula mapesa sisi wasimamizi na wachukuwaji hatua tunawatizama, wananchi wanateketea. Hii ni hatari kubwa sana. Mimi nimesema nitazungumza baadhi tu ya maelezo ambayo na mimi yakuniridhisha, wenzangu wamesema mengi. Ndugu yangu pale Mhe. Mbarouk Wadi Mussa, yeye kasema hataki hata kuisoma. Mimi nimejaribu kuisoma na kuelezea ile hali halisi ya yale maeneo ambayo inaonekana kwamba kuna udhaifu katika utekelezaji wa uchukuaji wa hatua katika ile ripoti ambayo imeletwa hapa.

Mhe. Spika, nasema kwamba tuna kazi kubwa sana na hali hii ikiendelea maana yake kama tunawaambia watu kwamba endeleeni kula, chukua halafu waondoke hapa waende pahala pengine. Unamwambia chukua Shirila la Umeme ukishakushiba tunakupeleka Wizarani ukale feni na ac utulie utumie fedha zako. Hii hali inasikitisha sana, mambo yako wazi, watu mapesa wanachukua katika *account* zao wakati *account* za taasisi zipo. Watu wanaunda Kampuni juu ya Shirika, watu humu ndani ya taarifa hii wamejiuzia magari pasipo na utaratibu, tunaambiwa magari hayo yatafatiliwa, sijui tujiulize ilikuwaje, Wizara ya Fedha haielewi. Eh! jamani inataka ielewe nini Mhe. Spika? Mpaka tukae kiza.

Maana yake sasa hivi hali ndiyo hiyo, *shagh'ala bagh'ala* unatoka pale umeme unakatika, unatoa ripoti kwenye shirika kuna tatizo *transformer* inaungua unaambiwa gari hazina mafuta, tuna gari moja gari yenyewe imekwenda Magharibi, subiri itoke Magharibi au itoke Kaskazini ndio ije kwako. Karibu pacha mwenzangu Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, nilikuwa naye tumekwenda safari moja usiku. Yeye ndiye Mhe. Naibu Waziri mtu wa Serikali Kuu, msimamizi ndio maana hawasemi au wanasaidia watu huku. Palikatika umeme pale Mea kwa muda wa siku tatu, kama Naibu Waziri katoa taarifa haujaungwa. Siku

hiyo tuko njiani akasema hebu leo nende huko, maana ukifika pale matatizo matupu na haya matatizo yanatokana kwa sababu ya ufisadi mwingi, watu wanaiba sana, hata zile huduma zinashindwa kuendelezwa. Mhe. Spika, pakiliwa sana hata watoto watalala na njaa. Haya ndio matatizo kwa sababu watu wanashindwa na nyenzo.

Mhe. Spika, najua wachangiaji wako wengi sitaki nichangie sana nataka niwape nafasi watu wote. Mimi nasema siungi mkono ripoti hii naomba kukaa.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nichukue nafasi hii kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu jinsi alivyotujaalia uhai na uzima tukiwa katika Sikukuu hii adhimu ya Mfungo Tatu. Wawakilishi wako Mhe. Spika, washuhudie Kiongozi wa Serikali akiwa safarini Makka kwa ajili ya ibada ya Hijja, Mwenyezi Mungu amjaalie Balozi Seif Ali Iddi akamilishe ibada yake, iwe vizuri na Mwenyezi Mungu amjaalie ampeleke Peponi kwa ibada hiyo.
Mhe. Spika, naomba nikishukuru sana kiti chako kwa jinsi ambavyo umetupa nafasi ya mchango huu na mimi nitakuwa na mchango mfupi sana ili wapate nafasi na wenzangu waendelee kuchangia ripoti hii.

Mhe. Spika, kwanza niipongeze serikali kwa maeneo mawili muhimu; kwanza kwa kutambua wajibu wa Baraza la Wawakili kwamba wameona kwamba ripoti hii hatimaae ije Barazani sasa ipate michango ya wawakilishi. Lakini pili niishukuru serikali kwa mzaha na kejeli ya hali ya juu kwa Baraza la Wawakilishi. Mhe. Spika, serikali naishukuru sana kwa mzaha wao na kejeli kubwa kwa Wazanzibari wanyonge wa Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, kama sijasahau ripoti hii tuliwaagiza na wao walikuwa ndani na walikuwa wote hawaumwi walikuwa wazima kwamba ndani ya miezi mitatu watuletee ripoti ya utekelezaji. Tangu Machi 2013 leo ni Oktoba ni miezi saba. Hii peke yake

kwa mtu mwenye akili ni udhaifu mkbuwa wa serikali. Kama serikali wameshindwa kutuletea ripoti miezi mitatu ambayo tumekubaliana ndani ya Baraza hili na wao walikuwemo, labda safari nyingi au pengine mambo ya serikali mengi lakini wameshindwa kutwambia miezi saba imepita leo ndio wanatusomea ripoti hii.

Mhe. Spika, niwaombe sana wenzangu wawakilishi wajue kwamba serikali hii ya awamu wa Saba chini ya Dokta Ali Mohammed Shein ni serikali yenye asilimia fulani ya dharau. Na kama dharau ndani ya serikali hii imo maana yake maendeleo ya Wanzanzibari ni vigumu sana kuyapata.

Mhe. Spika, nadharia ya uwongozi, kuna uwongozi na utawala. Kuongoza maana yake ni kusimamia watu au taasisi kwa kushauriana na kwa kufuata sheria. Na kutawala maana yake ni kuongoza watu bila ya kufuata utaratibu wa sheria na kufanya mabavu. Sasa tujuliulize je, kwa mfumo huu wa SMZ tuliyonayo tunaongozwa au tunatawaliwa? Mimi kwa tafsiri yangu Wazanzibari wanatawaliwa. Mtu anayekutawala hazingatii sheria, hazingatii kanuni, huangalia lile apendalo kwa mabavu yake. Na ndiyo ambavyo SMZ ya awamu wa saba Mhe. Spika. Sheria wanazijua, wametembea sana, lakini kwa sababu wanatawala hawazingatii uwongozi umuhimu wake ndio wanaamua hivi. Mhe. Spika, mimi sisemei kwamba Wazanzibari kwamba wanatawaliwa, lakini wajue tu kwamba hawaongozwi kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Spika, tujikumbushe basi Baraza hili limefanya ripoti kama nne, ripoti ya mwanzo ambayo ililetwa Barazani hapa serikali wao walichukua hatua wakawahamisha baadhi ya watu siku mbili tatu leo watwambie watu wale wako wapi. Kumbe waliwahamisha watu kwenye serikali hatimaye wamewarejesha chini ya mwaka mmoja, wapo serikalini wale wale waliowahamisha. Kumbe walikuwa wanafanya vile ili kuwaziba macho Wazanzibari na Wawakilishi wasione. Wale sote ambao

walichukuliwa hatua katika ripoti iliyopita leo wamo serikalini wanafanya kazi bila ya wasi wasi na bila ya vitisho.

Mhe. Spika, hii ndiyo SMZ ambayo Wazanzibari wanategemea iwapeleke mbali katika miaka 50 ya Mapinduzi Zanzibar, ili eti tusonge mbele kimaendeleo. Mtu anaharibu anaambiwa jifiche kidogo hatimaye rejea kazini kufanya kazi yako. Mimi niwaombe Wazanzibari wenzangu Wawakilishi ambao wamechaguliwa kwa kura za wanyonge watambue kwamba Wawakilishi wanadhima kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu na mbele ya wananchi wetu waliotuchagua.
Mhe. Spika, kwa nini serikali imeshindwa kuwachukulia hatua watendaji ambao wanafanya ubadhilifu. Tafsiri yake ni mbili tu; ama itakuwa serikali inawaogopa hawa wabadhilifu au tumeshindwa kuchukua hatua kwa sababu na sisi viongozi tumejawa na matatizo mengi. Lakini mimi siamini kwamba serikali inawaogopa wafanyakazi, ninachoamini kwamba tumeshindwa kuchukua hatua kwa sababu na sisi tumejaa matatizo.

Mhe. Spika: Mhe. Hijja Hassan Hija, nikuombe radhi hebu ukae kidogo kuna wageni wametoka safari niwatambulishe kwenu halafu utakuja kuendelea.

Waheshimiwa Wajumbe mnaelewa kwamba kesho Mwenyezi Mungu akitujaalia kutakuwa na Semina ambayo tutakaa hapa hapa katika ukumbi wetu wa juu, semina ambayo ni maalumu iliyotayarishwa kwa ajili yetu na Ras Al Khaimah. Ujumbe ambao umekuja kwa ajili ya semina hiyo tayari umeshafika hapa Zanzibar na mara baada ya kutoka Air Port wamekuja moja kwa moja ili kuwasalimia Waheshimiwa Wajumbe. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe naomba niwatanbue *let me now recognize among others:*

1. Mr. Kamal Ataya *Chief Executive Officer*

2. Mr. Chris Tinkler V*ice President Exploration*
3. Mr. Joseph Haskell *Chief Operating Officer*
4. Mr. Protase Ishengoma *Director* Ras Al Khaimah Tanzania
5. Mr. Damascene Makatu *Country Manager*
6. Mr. Musa Tharia *Manager* wa Ras Al Khaimah hapa Zanzibar

You are all most well come and this is House of Representatives, we are now in session doing the work of the people of Zanzibar. You are most well come to Zanzibar, You most well come to the House. Thank you so much in did, thanks allot!

Mhe. Hijja Hassan Hija, sasa endelea na mchango wako.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, kwa niaba ya *back benchers* wenzangu basi wageni wako tumewapokea vizuri sana.

Mhe. Spika, nilikuwa nauliza kwa nini serikali imeshindwa kuwachukulia hatua watendaji wabadhirifu? Tafsiri yake ni mbili; moja kati ya hayo ni sahihi ama serikali inawaogopa watendaji. Kama hilo silo maana yake serikali mongoni mwetu itakuwa madhambiyetu makubwa zaidi kuliko watendaji. Kama mimi mwenyewe binafsi nimeiba shilingi mia lakini mtoto wangu ameiba shilingi moja ni vigumu sana kumchukulia hatua.

Sasa siamini kama serikali inawaogopa watendaji lakini inaandaa mazingira ya kufanya kwamba Wazanzibari hawana haki ya kusema. Sasa Mhe. Spika, nimejaribu kuzitafuta zile barua za wale waliohamishwa, nimepata barua mojatu. Nimeangalia sheria ya kazi kama alivyosema mwenzangu Mhe. Ali Shehe, kumuhamisha mfanyakazi ndani ya Wizara ni utaratibu wa kawaida sio adhabu. Mtendaji kumuhamisha katika wizara hatua hiyo ni hatua nyengine si adhabu ni utaratibu wa kawaida. Leo serikali inatwambia imetoa adhabu. Mtu ametoka ZECO Pemba

amekwenda Wizara ya Maji Pemba ni adhabu kwa taratibu za SMZ.
Mhe. Spika, ikiwa miaka 50 serikali haijajua adhabu ni nini basi ni hatari kubwa na ni aibu kubwa. Kwamba eti mimi ukinihamisha hapa ukinipeleka ndani ya Baraza la Wawakilishi ni adhabu. Uhamisho ndani ya wizara moja ni wajibu mbali ya wizara kwa serikali nzima si tatizo. Lakini kwa SMZ ni adhabu kubwa kwamba umemtoa ZECO unampeleka Wizara ya Maji Pemba, hiyo ni adhabu kubwa.

Wazanzibari wajue kwamba zikipotea mamilioni ya fedha adhabu yake ni kuhamishwa Idara. Mhe. Spika, ni aibu kubwa na mimi niwaombe Wawakilishi wenzangu kwamba ripoti hii tusiikubali. Kwenye nchi zenye demokrasia na utawala bora, mawaziri wote walioshindwa kufanya kazi za Baraza wajiuzulu. Mhe. Spika, narejea, kwenye nchi zenye utawala wa sheria na utawala bora, Mawaziri walioshindwa kutekeleza maagizo ya Baraza, maagizo ya Bunge maana yake wajiuzulu.

Mhe. Spika, naomba sana kwa heshima kubwa na kwa uungwana mkubwa mawaziri wetu ambao wameshindwa kusimamia maagizo ya Baraza wajiuzulu wakati wowote kuanzia sasa. Mhe. Spika, mimi naona aibu sana kwamba tumechambua mapato ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar fedha za walipa kodi wakapewa Wawakilishi kufanya kazi ya kuisaidia serikali leo hakuna hatua.

Mhe. Spika, niwashauri wenzangu Wawakilishi, tuzichukue ripoti zote nne za uchunguzi tuziandike kwa lugha nyepesi ya kitaalamu tuwapelekee mabalozi waangalie jinsi pesa zao za misaada zinavyotafunwa hapa Zanzibar. Mimi binafsi nakusudia kufanya *Press Conference* Jumatatu ijayo tukijaaliwa na nitaandaa hoja kupeleka UNDP kwamba Baraza la Wawakilishi wakisaidiwa na Wawakilishi wa Wafanyakazi lakini hakuna *impact* yoyote. Hatuoni Mhe. Spika, kutumia milioni 500 kuwafanyia serikali kazi yao, hatimaye majibu ukurasa 20,

kurasa hizi si zaidi ya shilingi elfu kumi gharama yake. Eti leo hii ndio majibu ya milioni 500 zilizopotea, ndio majibu ya serikali haya.

Mhe. Spika, tarehe 12 Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Mwakilishi Makini wa Mwanakwerekwe ambae pia ni Waziri wa Ulinzi, na Mjumbe wa PAC alifanya mkutano akasema kwamba ripoti za Kamati zetu sisi Baraza la Wawakilishi zaidi ya milioni 60 zimepotea na hakuna hatua yoyote. Mhe. Spika, huu ndio wajibu wa kiongozi, kwamba serikali imepoteza fedha za wananchi milioni 60 zitokanazo ndani ya mikono ya wananchi wanyonge, zimetafunwa hatimaye majibu ya serikali ni mepesi yenye kurasa 22. Maana yake ni Shs 22,000 + *photocopy* Shs 6000 finish, kwa sababu wanajua kwamba hakuna hatua.

Mhe. Spika, mimi siwalaumu watendaji wa ZECO, watendaji hawa walitupa ushirikiano mkubwa, wakajieleza, wakatupa ushahidi, tatizo ni serikali. Kwa msingi huu Mhe. Spika, serikali kumbe inaandaa mazingira kwamba watu waibe. Na mimi nasema kila mwenye nafasi aibe kwa sababu hili ni shamba la bibi. Shamba la bibi kama mwenyewe hayupo liibiwe kwa hivyo kwa msingi huu serikali wanahalalisha kwamba kumbe ukiiba huna adhabu, kumbe unahamishwa tu. Kama Ofisi yako ni Dunga utapelekwa Mwanakwerekwe, utapelekwa Kiembesamaki au Wete au Mkoani.

Mhe. Spika, kwa dhati ya nafsi yangu siungi mkono hoja hii na naomba Wawakilishi wenzangu makini waliochaguliwa na wananchi wanyonge wakatae hoja hii, tusipoteze muda. Serikali iendelee kulinda watu wao na sisi wajibu wetu wawakilishi tuwambie wananchi kwamba hii serikali ndivyo ilivyo na tuwambie Mabalozi kwamba fedha zenu ambazo mnawafadhili Wazanzibar haziwafikii zinatafunwa. Na mimi niwaombe Wawakilishi wenzangu tuandike hoja hiyo kwa Mabalozi tuwaambie kwamba kweli mnatusaidia lakini mtu wa Kiwani, mtu wa Makunduchi, mtu wa Wete, hafaidiki kwa msaada wenu.

Mhe. Spika, baada ya mchango wangu huo mfupi naomba niseme kwamba siungi mkono hoja hii na wawakilishi wenzangu waliomakini anayehisi kwamba mnyonge alimpigia kura kutwa nzima basi hoja hii asiiunge mkono naomba sana irejeshwe serikalini wafanye mambo yao.

Mhe. Abdalla Mohamed Ali: Mhe. Spika, na mimi nashukuru kunipatia fursa jioni hii ya kusema kwamba hoja hii au taarifa hii na mimi siiungi mkono.

Mhe. Spika, kwa maneno yako leo asubuhi uliisifia sana taarifa kwamba kamati yako imefanya kazi kubwa sana kiasi kwamba ikaleta taarifa iliyo na picha halisi ya utendaji wa mashirika yetu. Lakini pia Mhe. Waziri na yeye katika ripoti yake amesema kwamba ripoti hii iliyoletwa na kamati yako imetoa picha halisi ya namna gani mashirika yetu yanavyofanya kazi zake. Lakini pia labda alikuwa amesahau kwamba pia ripoti yake iliyokuja hapa Barazani nayo imetoa picha halisi na namna gani serikali inafanya kazi zake.

Mhe. Spika, nafikiri sijui nitumie lugha gani, lakini serikali zilizopita huko nyuma tulikuwa tunazilaumu kwamba zinatumia ule mtindo Rais aliyesema wa "*Business as Usually"* Sasa awamu hii nafikiri ile *"as"* tumeiondosha tunatumia *"is"* ambayo ki *verb* inakuwa ni *direct* moja kwa moja. Sasa baada ya kusema kwamba *"Business as Usually"* tunataka tuondoke tunasema sasa tunakwenda *"Business is Usually*" ndipo tulipo. (*Makofi*)

Mhe. Spika, sijui tunakwenda wapi? Mimi nilitarajia awamu hii kwamba tutakuwa tunabadilika hasa kwa kufuata zile *slogans* ambazo zinaletwa na viongozi wetu wakubwa. Lakini maskini tunarudi kule kule nyuma.

Mhe. Spika, labda mimi nimuulize Mhe. Waziri na mimi nisiwe na mengi sana ya kuzungumza hapa. Mhe. Waziri,

anatuthibitishiaje kwamba ripoti hii imekamilika, kwa sababu kila hoja inayokuja inaonesha kwamba litaamrishwa jeshi la polisi. Lakushangaza kwamba hii mihimili tofauti lakini pia serikali au mhimili mmoja umuamrishe muhimili mwengine ufanye kazi zake. Mimi sijayaonapo hayo kama ni muhimili wa polisi ulikuwa ufanye kazi zake moja kwa moja tu bila ya kupata amri kutoka serikalini muhimili mwengine. Sasa leo anatwambia kwamba ataliamrisha jeshi la polisi lifanye uchunguzi, baadaye taarifa itakwenda wapi Mhe. Spika?

Yeye aliwajibika taarifa yake atuletee sisi hapa ili tujekukubaliana nayo, sasa majibu ya polisi yatasema atakwenda nayo wapi? Atakuja tena Barazani? Kanuni hairuhusu. Mimi nasema kwa msingi huo hii ripoti Mhe. Spika, haijakamilika. Kwa hivyo kuna haja ripoti hii irudi tena ili ifanyiwe kazi, aje atwambie moja baada ya jengine kwamba ripoti hii sasa kama ni jeshi la polisi, gari iliyouzwa namba fulani, namba fulani ripoti yake 1, 2, 3. Ni jambo la aibu kusema kwamba serikali ilikwisha kataa na ikapeleka barua ZECO kwamba gari zisiuzwe. Leo unatwambia Mhe. Waziri kwamba tupeleke jeshi la Polisi likachunguze. Linakwenda kuchunguza nini? Wakati barua tayari imeshazuia kwamba gari isiuzwe. Hiyo ni hoja Nam. 30 inasema kwamba barua ilitoka Wizara ya Fedha kwamba gari isiuzwe, lakini leo unakuja kutwambia kwamba unatufanyia uchunguzi, uchunguzi wa nini Mhe. Spika?

Lakini kuna hoja nyengine ya kwamba kuna uchunguzi wa hii Kampuni ya Muhammed na Bashir, tunachunguza nini? Muhammed na Bashir wanajulikana wamefanya kosa yeye hakupewa leseni. Sheria tumeipitisha, tunazo ya mambo ya leseni, leo tena tunakwenda kukaa itachukua mpaka lini Muhammed *and* Bashir kuchunguzwa Mhe. Spika, tuje tuwaambie wananchi Muhammed *and* Bashir alikuwa hana leseni ya kuuza nguzo ya umeme, miaka mingapi tuchukue. Hii tayari ripoti ni mwaka wa pili unapita. Mhe. Spika, tunataniana.

Serikali inatakiwa iwajibike moja kwa moja kuhusu masuala haya, uthibitisho upo, hakuna tena haja ya kufanya uchunguzi.

Mhe. Spika, kuna mfanyakazi anaitwa Abeid na yeye pia tunaambiwa anatakiwa achunguzwe, wakati tunajua fika kwamba Shirika la Umeme ndilo lenye wajibu wa kuunga umeme sehemu zote. Huyu anajulikana si mfanyakazi wao, kama si mfanyakazi wao vifaa alivipata waji vya kuwa aungie umeme. Tukachunguze nini, tupoteze tena wakati na fedha na shirika kupoteza wakati kwamba tunakwenda kumchunguza. Mhe. Spika, inatakiwa serikali ituletee ripoti kamili. Hii mimi nasema siungi mkono.

Mhe. Spika, naona nisiendelee kusema mengi kwa sababu kila ninachokisema hapa Waziri wameshakisikia na hoja nilizozisema ameshazisikia. Mimi nasema siungi mkono hoja. (*Makofi*).

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Muumba wetu Mwenyezi Mungu (SW) kwa kutujaalia kuwa hai na wazima na laasiri hii tukiendelea na shughuli zetu katika chombo hiki cha wananchi wa Zanzibar.

Pili Mhe. Spika, nikushukuru na wewe kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia sijui niseme hoja au taarifa ya serikali kuhusu Hoja mbali mbali za Kamati ya PAC ya Baraza la Wawakilishi iliyochunguza utendaji wa Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO).

Mhe. Spika, mimi nataka nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais (Mhe. Muhammed Aboud Muhammed) nampongeza kwa sababu sitaki kusahau historia. Siku ilipokuja hoja hii ya kutaka kuundwa Kamati Teule kwanza yeye hakuwa mzito kwa niaba ya serikali kukubali suala la kuchunguza utendaji wa ZECO kwa hiyo nampongeza sana. Na nakumbuka muongozo wake au ushauri wake ndio ulipelekea kuunda Kamati ya Teule kuiomba kamati ya Kuchunguza Hesabu za Serikali (PAC) ikafanye kazi hii ikimjumuisha na mjumbe ambaye alikuwa ametoa hoja. Kwa hivyo hilo kwangu

mimi ni sifa kwa Mhe. Muhammed Aboud kwa sababu imeonesha utayari wake wa kuona kwamba mambo ambayo hayaendi sawa katika serikali yanachunguzwa na chombo hiki kinatekeleza wajibu wake wa kikatiba.

Mhe. Spika, nimeipata taarifa hii nimeisoma, lakini kidogo nimeshtushwa na muelekeo wa mjadala wetu. Mimi kawaida yangu ni mtu muwazi kwa yale ambayo nayaamini. Naomba kidogo ili kulifahamu hili ninalotaka kulizungumza tujiulize kwa sababu suala hili kila wakati limekuwa likileta mkanganyiko katika Baraza hili Mhe. Spika. Ni nini matokeo ya Kazi za Kamati Teule, kwa sababu baraza letu ni wanachama wa Jumuiya ya Mabunge ya Jumuiya ya Madola *(Commonwealth Parliamentary Association*), ninafurahi kwamba niliazimwa kitabu hiki na swahibu wangu Mhe. Omar Ali Shekh aliporudi safari yake ya Uingereza kinaitwa *HOW PARLIAMENT WORKS* toleo la 6 kimeandikwa na waandishi Robert Rogers na Rhodri Walters.

Mhe. Spika, katika kitabu hiki kunazungumziwa muundo wa uendeshaji na kazi za Bunge la Uingereza ambalo linaambiwa katika dunia ndio *mother of parliament.* Sasa katika sehemu ya kazi zake pamezungumzwa suala la kuhakikisha uwajibikaji kwa serikali na vyombo vyake. Na katika maeneo mbali mbali imezungumzia namna tofauti ya kuiwajibisha serikali, iko sehemu Mhe. Spika, katika kitabu hiki inazungumzia *select committee* yaani kamati teule. Na katika hilo ikaelezea mtiririko wa shughuli zinavyofanyika. Kuna sehemu inazungumzia majibu ya serikali kwa kamati teule, hiyo ndio ambayo ninataka niinukuu Mhe. Spika, iko katika ukurasa 368/369 ya kitabu hiki na naomba niisome kama ilivyo kwanza kwa kingereza.

The government reply inasema:

"Reports are made to the House, although the intended audience included everyone concerned with the subject, the media and

crucially the government. Every select committee report should receive a formal government reply within two months. Hii kwa mfumo wao *This is a convention rather than a formal rule, but committee have found that asking the minister concerned to appear to explain a delay often means the rapid appearance of the reply.*

No one expects a government to put on the sackcloth and ashes in this formal reply. If the committee is has been highly critical the government is more likely to be defensive and to restate its case than to say 'it's a fair cop'. If the committee has put forward challenging recommendations, the government is likely to be cautious rather than right away but the 'delayed drop' effect of select committee reports should never be underestimated. Ambitious recommendation may change the whole public debate on a subject, they may be taken up by public bodies and pressure groups; and months (or sometimes two or three years) later they may contribute substantially to a major shift in government policy. Similarly the effect of justified criticism may not be immediately apparent; but a department may be quietly changing its procedures to avoid making the same mistake again.

Whatever the contents of the government reply, committees are more influential if they follow up on their reports. Most departmental select committees have a 'continuous agenda' in which major policy issues recur, but returning to the detail of previous recommendations, and pursuing vague promises or non-committal responses through further inquiries, maintains the pressure and keeps the subject in the public eye". Mwisho wa kunukuu.

Mhe. Spika, sitaki nitafsiri neno kwa neno kwa sababu naweza kuchukua muda wangu zaidi. Lakini cha msingi kinachoelezwa hapa ni kwamba njia moja ya kuiwajibisha serikali ni kupitia ripoti hizi za uchunguzi. Na inaonesha kwamba ni kawaida ya

serikali pengine kote kwamba ikiwa ripoti ni kali na inayojielekeza katika kuibana serikali basi serikali itakuwa inajitetea. Lakini nasema athari ya ripoti kama zile inakuwa kubwa kwa sababu inapelekea kubadilika kwa utendaji wa serikali, ama chombo kile kinachozungumzwa kinaweza kisirejee makosa yale kwa sababu hakitaki kuzungumzwa tena, lakini pia inaweza ikabadilisha mtazamo wa jamii nzima. Na katika zile hoja kubwa na nzito nasema hata zinaweza zikachukuliwa na makundi ya jamii na makundi yale yanaitwa *pressure groups* ili kusaidia kubadilisha muelekeo wa nchi na jamii kwa jumla. Nadhani ni hayo Mhe. Spika, kwa ufupi.

Sasa Mhe. Spika, nimeona nikisome kifungu hiki kwa sababu leo kidogo nataka kuwaombawenzangu kwamba mara nyengine na hili naona mara nyingi tumeliamini hivyo, kwamba kuamini kwa sababu kuna ripoti ya Baraza kupitia kamati ipelekee mtu moja kwa moja katika vyombo vya sheria kwa maana ya mahkama hilo ni kosa Mhe. Spika. Kwa sababu katiba yetu imeweka mgawanyo wa madaraka na mamlaka ya utoaji haki kwa mujibu wakifungu cha 5 (a) cha Katiba yetu ni ya mahkama. Kwa hivyo nadhani hilo moja ni vizuri tukalielewa ili tusije tukajitwika jukumu na chombo hiki kuweza kutoa tuhuma na kuhukumu na kuadhibu. Kwa sababu moja katika misingi ya kitu kinachoitwa *natural justise* ni kwamba huwezi kuhukumu kesi yako mwenyewe kwa hivyo hilo nilikuwa naliomba Mhe. Spika, lakini baadae watanifahamu wajumbe, nataka kulitolewa ufafanuzi naomba nianze hapo.

Sasa Mhe. Spika, baada ya kuondoka hapo nije katika ripoti hii ya serikali, pamoja na mtazamo niliouzungumza kuhusu shughuli za kamati, ukitizama kama nilivyosema mtazamo wa kidunia ni kwamba ripoti za kamati zipelekee mabadiliko serikalini. Lakini hilo naungana na wajumbe wenzangu wote kusikitika sana na kuhuzunika kwa niaba ya wananchi wa Zanzibar kwamba ripoti hii ni ripoti ya tatu na ya nne tunaisubiri hakuonekani kuna mabadiliko katika utendaji wa serikali.

Mhe. Spika, nimeipitia kwa kina wakati tumepata kipindi cha mapumziko hapa kati kati hii ripoti ya serikali. Na mimi niseme kuna maeneo machache nataka kuipongeza serikali na naomba nianze na hayo kwa sababu hayo ni machache. Kuna sehemu Mhe. Spika, humu ripoti ya kamati hoja namba 12 ilizungumzia suala la Bodi ya Wakurugenzi ya ZECO kuchagua Kampuni ya CRJE badala ya SALCON, lakini baadae wakavunja mkataba na Kampuni ya TCJE na kupelekea kulipa fidia ya dola za kimarekani 20,786 na kulitia hasara Shirika.

Maelezo ya serikali yamesema kwamba baada ya kufuatilia wamegundua kwamba haikuwa fidia bali ilikuwa ni malipo ya gharama za ujenzi ambao ulikuwa umeshafanyika hadi wakati ule. Kwa sababu inaonekana CRJE walianza kazi. Lakini serikali ikenda hatua moja zaidi ambayo Kamati pia haikuwa imegusa, ikasema walipofuatilia walichogundua ni kwamba Kampuni ya MANTRAC ambayo iliyoonekana ndio waliomalizia hiyo kazi walilipwa fedha zao za ujenzi kama kwamba Kampuni ya CRJE haikulipwa kabisa. Kwa hivyo akasema hivyo serikali imeliagiza Shirika la ZECO liiandikie MANTRAC kulipa fedha za CRJE yaani ile fedha ambayo CRJE walikuwa wameshalipwa kwa kufanyakazi ile ya awali. Kwa hivyo hili nalipongeza kwa sababu inaonekana Mhe. Spika, kwamba kuna maeneo ambayo kamati haikuyaona, serikali imefatilia imeona zaidi na imechukua hatua,

Lakini ninasikitika Mhe. Spika, na yako mengine ambayo nimefuatilia na nimegundua kwamba kamati labda haikuweza kupata taarifa zinazojitosheleza, lakini kuna maendeo ambayo ndio mengi serikali yenyewe imekiri kwamba kamati imekuwa sahihi na imeipongezwa, lakini utekelezaji wa hatua ni wa kubabaisha.

Mhe. Spika, moja limetajwa hapa tukilifanya marejeo ya ripoti ya kamati ile ya PAC ilipokuwa ikifanya kazi maalumu, kuna

watendeji kadhaa wametajwa kwa majina na vielelezo vikionesha kwamba wameshiriki mimi sisemi ubadhirifu maana yake ubadhirifu ni matumizi mabaya, kuliibia Shirika, kuiibia serikali. Mara nyingi Mhe. Spika, tunatumia neno ubadhirifu, ubadhirifu ni matumizi mabaya pengine linakaribiana karibiana na israfu. Lakini Mhe. Spika, ukiwa umefanya kazi ya Shirika ukatoa account yako binafsi utiliwe fedha huo ni wizi. Ikiwa Shirika mtendaji wake hajui viwango vya kumtoza mteja katika kumuunganishia umeme iwe mwengine kazi kubwa analipa malipo kidogo, na mwengine kazi ndogo malipo makubwa huo wizi Mhe. Spika, si ubadhirifu wala si uzembe.

Na katika hili, ripoti ya PAC ilijikita na ikatoa vielelezo vya kina kabisa. Sasa mimi nilitegemea leo Mhe. Spika, kwamba kwa watendaji wale serikali ingekuja kuturipotia kwamba ni sawa ichukuwe ripoti ya PAC kwa sababu kama nilivyosema mwanzo Baraza hili halifanyi kazi ya Polisi iwafikishie Polisi, lakini baada ya hapo tuone hatua zimeendelea, majadala sasa yapo kwa Mkurugenzi wa Mashtaka DPP. Mhe. Spika, Katiba yetu imetoa mamlaka hayo kwamba DPP kwa mujibu wa kifungu cha 56(a) ndio ofisi yenye mamlaka ya kufungua mashtaka kwa makosa yote ya jinai. Lakini ripoti hii imewasilishwa hapa mwezi wa Machi, 2013 leo tuko mwezi wa Oktoba, hii ni takriban miezi 7.

Hivyo Mhe. Spika, baada ya miezi 7 bado serikali inaripoti ndani ya chombo hiki kwamba Polisi wamekabidhiwa wanafanya uchunguzi, uchunguzi huu utakwisha lini? Na si uchunguzi kwamba unakwenda kuanza mwanzo, ni uchunguzi ambao chombo cha wananchi kimeshafanya kazi kubwa kwa sababu keshakuwekea kianzio na vielelezo vyake, kwa hivyo huna kazi kama ya kuanza kutafuta wapelelezi wakenda wakajificha wanatafuta mtu, hapana, tayari kuna pahala pa kuanzia tena na ushahidi na vielelezo. Kwa hivyo kazi ya Polisi ni nyepesi sana Mhe. Spika, ni kuthibitisha tu vile vielelezo na yale maelezo na tuhuma ambazo zimetolewa pale ikiwa imeridhika ikamilishe jalada lake ipeleke kwa Mkurugenzi wa Mashtaka. Hilo

lichukuwe miezi saba Mhe. Spika, mpaka leo tunaripotiwa kwamba hatua zinaendelea. Hiyo Mhe. Spika, haioneshi umakini wa serikali.

Na kwa mimi Mhe. Spika, na naamini kwa hilo asilimia ya wananchi wengi wa Zanzibar wataishangaa Polisi hii, kuna kesi nzito nzito hapa ambazo wanakuwa wepesi wa kukamata na mpaka leo hazendi zimekwama mahkamani. Wengine watu wameendelea kukaa mahabusu unakaribia mwaka pengine lakini yale wamekamata, hizi ambazo kuna vielelezo vyake tayari kwa hivyo bado Polisi inachunguza. Sasa sijui kama tatizo ni Polisi au tatizo la serikali katika kusimamia Polisi kufanya kazi yake. Mhe. Spika, hili mimi nimesikitika sana sitaki kutaja moja moja kwa sababu yamo mengi yalikuwa yanahusu ubadhirifu, hilo ni moja ambalo sikuridhika.

Lakini la pili limetajwa na wenzangu Mhe. Spika, kama nilivyosema mwanzo kuna tofauti ya ubadhirifu na wizi. Mhe. Spika, ripoti ile ya PAC ilitaja vizuri sana kesi mbali mbali za wafanyakazi wa Shirika, kwa mfano, kwa sababu ni mfano ulio wazi ule ambao uko katika ukurasa wa tano waripoti ya serikali hoja nambari 2, fedha za malipo ya kuungiwa umeme kuigizwa katika *account* ya mtendaji wa Shirika Ndugu Zakiya Juma Azan.

Mhe. Spika, kama nilivyosema hii huwezi ukaiita ubadhirifu, sidhani mimi labda uwe kidogo una upungufu wa akili, kwamba uwe hujui tofauti ya *account* ya Shirika na *account* yako binafsi na kwamba uwe hujui kama mtendaji wa Shirika kwamba fedha za Shirika zinapaswa kwenda katika *account* ya Shirika na si katika *account* yako binafsi Mhe. Spika. Sasa huyu leo serikali inaturipotia kwamba imempa adhabu kali kweli kweli ya kuchukia wizi alioifanyia serikali na wananchi wa Zanzibar, imempa uhamisho kwenda Makao Makuu ya Wizara.

Sasa Mhe. Spika, wananchi watajiuliza kwa sababu leo nimemsikia Mhe. Waziri katika hili akijibu hapa kwamba tunapoambiwa serikali hii iko makini na Mheshimiwa Rais wetu akasema moja katika kauli mbiu yake ya mwanzo kwamba anataka kupiga vita mfumo wa kufanyakazi chini ya mfumo wa *business as usually*. Sasa tutajiuliza kwamba haya ndio mabadiliko ya mfumo ya miaka mitatu Mhe. Spika? Mtu aliyechukua fedha mamilioni akatia katika *account* yake binafsi kahamishwa na tumeambiwa kwa mujibu wa sheria ya utumishi wa umma nambari 2 ya 2011. Mimi Mhe. Spika, hebu naomba nisaidiwe wapi sheria ya utumishi wa umma nambari 2 ya 2011 inasema mfanyakazi wa serikali akiliibia Shirika au Taasisi ya Serikali apelekwe uhamisho katika Makao Makuu ya Wizara yake. Mhe. Spika, naomba niondoke hapo kwa sababu sitoweze kuyazungumza yote kwa sababu ya muda nataka na wenzangu wapate fursa, ninatoa kwa mifano tu.

Jengine Mhe. Spika, linahusu kwa mfano hoja nambari 4, 17, na 18 lipo ukurasa wa 7 ripoti ushiriki wa Mohammed *and* Bashir kwa niaba ya Sana Express katika zoezi zima la uungwaji wa umeme katika hoteli ya Misali. Mhe. Spika, tumeambiwa kwamba Shirika tayari limeiandikia rasmi Kampuni ya Mohammed *and* Bashir kusitisha mara moja biashara ya uuzaji wa vifaa vya umeme na kwamba Shirika halitosita kuchukua hatua za kisheria dhidi ya Kampuni yoyote itakayoendesha biashara inayohusu masuala ya umeme bila ya kibali cha Shirika. Aidha Shirika limeliagiza Jeshi la Polisi na Bodi ya Mapato kufanya uchunguzi wa kina kwa Kampuni hiyo ya Mohammed *and* Bashir kuhusu tuhuma za kutumia risiti za Kampuni ya Sana Express na kwa kufanya hivyo kuna uwezekano Mhe. Spika, kukwepa kulipa kodi.

Mhe. Spika, huyu kakiuka sheria za nchi kwa sababu mamlaka haya ya Shirika yametungiwa sheria na Baraza hili la Wawakilishi na ripoti ya PAC ilitaja hivyo, leo Shirika linalochunguzwa ambalo limejaa makosa haya linaambiwa

kwamba linaliarifu Jeshi la Polisi lichunguze. Lakini nilichokiona kioja cha mwaka Mhe. Spika, ni mwisho wa maelezo haya kuhusu vile vifaa vinavyotunmika, inasema "Shirika kuanzia sasa kuhakikisha linajiandaa kuwa na vifaa vya kutosha vinavyokidhi mahitaji ya wateja wanaotaka kuungiwa umeme sambamba na kuhakikisha kwamba vifa vinavyotoka nje ya nchi vinakuwa na viwango bora kwa kuvifanyia ukaguzi unaostahiki kabla havijaanza kutumika kwa kushirikiana na taasisi inayohusika na ubora wa viwango Zanzibar Bureau of Standard (ZBS). Mhe. Spika, sote tunajua kwamba ZBS mpaka leo imeundiwa maneno tu, haijaanza kazi kwa sababu haina hata kifaa kimoja cha kufanyia kazi. Sasa leo tunapoambiwa kwamba ati ZECO inatakiwa ifanye kazi kwa kushirikiana na ZBS Mhe. Spika, haya ni majibu ya kuondosha njiani.

Mhe. Spika, naomba nitoe mfano wa mwisho kwa sababu kama nilivyosema mifano iko mingi na muda ni mchache. Mfano wa mwisho nnaotaka kuuzungumzia Mheshimiwa ni huu unaohusu ZECO NA GECO. Mhe. Spika, hii imetajwa katika hoja nyingi humu lakini cha msingi ni kwamba kuna wafanyakazi wawili ambao ni wa ZECO lakini wakati huo huo wanafanya kazi ya GECO, wamefungua Kampuni yao binafsi. Wametajwa Mhe. Spika, katika ukurasa wa 8 hawa ni ndugu Hamidu Saidani Ali na Ndugu Ali Abeid Haji. Sasa hawa Mhe. Spika, serikali imetwambia imechukua hatua ya kuwahamisha wafanyakazi hao na kuwapeleka sehemu nyengine.

Hawa Mhe. Spika, wamekiuka msingi wa maadili ya utumishi serikalini, kwamba wanatumikia mamlaka inayotoa huduma fulani halafu wao wenyewe wakiwa wafanyakazi wameunda kampuni yao binafsi wanayojipa kazi. Halafu serikali imeona adhabu ya kuwapa ni kupeleka sehemu nyengine na wala hatukutajiwa sehemu gani, kama wameongezewa cheo, wamepunguzwa hatujui Mhe. Spika. Kwa hivyo Mhe. Spika, ninavyosema ukitizama maelezo mengi ukiondoa yale machache nasema ninaipongeza serikali lakini bado hayaridhishi.

Mhe. Spika, nimalize kwa nukta moja ya uajiri iko katika ukurasa 16 hapo nina suala. Mhe. Spika, hoja nambari 28 inasema hakuna ruhusa iliyotoka kwa Bodi ya Wakurugenzi kuhusu ajira ya wafanyakazi 16 walioajiriwa 2008. Na serikali imekubaliana na hoja ya kamati na imethibitisha kwamba menejimenti ya shirika haikuwa na ruhusa ya Bodi kuajiri watu hao 16 lakini la ajabu maelezo ya serikali inasema, serikali tayari imempa onyo Meneja Mkuu wa Shrika la Umeme la kumtaka awe makini zaidi katika utekelezaji wa majukumu yake na kufuata sheria. Yale yaliyopita sawa wewe umevunja sheria basi mara ya pili tu kuwa makini zaidi.

Sasa Mhe. Spika, mimi kama nilivyosema yapo humu ya kujiuzia mali za Shirika na mambo mengine kinyume na utaratibu.

Mhe. Spika, mimi nasema ripoti hii bado katika maelezo ya hatua iliyochukuliwa baada ya kipindi chote hiki hairidhishi. Mhe. Spika, baada ya kuiweka ripoti nimalizie mchango sasa kwa maelezo mawili tu katika maelezo ya jumla nifungie mchango wangu Mhe. Spika.

La kwanza, mimi nasema pamoja na hatua nyingi nimeona kila hatua Mhe. Spika, Meneja wa hapa na yule wa Tawi la Pemba wamepewa onyo. Mimi Mhe. Spika, naona na naomba nifahamishwe kama sheria yetu ya utumishi wa umma inakataza, lakini naona kwa uzito wa tuhuma na ambazo nyingi serikali imezikiri za kushindwa kulisimamia shirika, huyu Mhe. Spika, alikuwa si wa kuonywa ilikuwa wa kuondoshwa, kuwajibishwa katika nafasi yake ile. Na Mhe. Spika, nataka kusema wananchi wa Zanzibar tutamstaajabu sana Mhe. Rais kwamba yeye alikuwa akiongoza kusema hataki *business as usually*, lakini mtu aliyetuhumiwa kwa makosa kama yale ambayo mengi yao serikali iliyakubali na imekiri katika ripoti hii kwamba inakubaliana na ripoti ya kamati, halafu ikaona adhabu yake iwe

ni kumpa onyo mimi ninastaajabu Mhe. Spika. Mimi nilikuwa nadhani yule alikuwa ni mtu wa kuajibishwa na Meneja wake wa Tawi la Pemba chini ya ubadhirifu huu. Hilo lilikuwa moja katika mawili ya jumla Mhe. Spika.

Lakini la pili, ni kwamba kuna suala vile vile limejitokeza na hili limewahi kuripotiwa katika kamati ya mwanzo kabisa ilipokuja hapa. Suala la watoa taarifa kwa kamati kuadhibiwa, hao Mhe. Spika, katika mfumo wa kupiga vita ufisadi huwa wanaitwa kwa kingereza *Whistle blowers* yaani wapiga firimbi. Sasa kumekuwa na malalamiko katika nchi nyingi duniani kwamba mara nyingi watu huogopa kutoa taarifa kwa sababu anajua akitoa taarifa ya ufisadi yeye anakuja kuwa *victim* (majeruhi). Sasa kuna mtendaji mmoja alitajwa hata katika ripoti lakini tunaambiwa kwamba huyu ni mmoja aliyekuwa katika mashahidi wakubwa aliyetegemewa na kamati kwa upande wa Pemba. Mhe. Spika, huyu anaitwa Shaibu Kaduara Hassan.

Mhe. Spika, huyu hata katika kamati yako ya mawasiliano na ujenzi ilipokwenda kuanza kazi mapema Pemba alianza kuonesha wasiwasi kwamba atachukuliwa hatua kwa sababu tu aliisaidia Kamati kwa taarifa. Na imethibitika kwamba kasaidiwa mpaka barua yake ya uhamisho wa kikazi, katika waliohamishwa katika shirika kupelekwa katika Wizara. Sasa serikali imeona hii ni adhabu, vipi imemtia adabu mtu ambaye ndio aliyekuwa chanzo cha kutoa taarifa hatimae wananchi wa Zanzibar wakaweza kujua ufisadi na utendaji mbovu unaofanyika katika Shirika la Umeme. Mhe. Spika, hili tukio naomba tulikemee sana kwa sababu likiendelea hivi litapelekea maana yake tuna *institutionalize corruption (*tunaihalalisha rushwa) kwa sababu itakuwa mtoa taarifa wa ule ufisadi atashindwa kuja kumfikia mjumbe wa chombo chako Mhe. Spika, au mtu mwengine yoyote ikiwa Polisi, ikiwa DPP yeye atakakaa hatakuwa shahidi mahkamani. Kwa sababu ataona kwamba akifanya hivyo Mhe. Spika, atakuwa mwisho yeye ndie mkosa.

Mhe. Spika, nimeeleza mengi kama nilivyosema mimi tofauti na wenzangu sipendi chombo hiki kionekane kama chenyewe kinatuhumu na kinahukumu lakini hapo hapo naamini kifanye kazi yake ya kuisimamia serikali kama Katiba yetu inavyosema na maana yake serikali iwajibike kwa chombo hiki kama Katiba yetu inavyosema. Na kuwajibika kwa serikali Mheshimiwa maana yake ni kuyachukulia kwa umakini mapendekezo yanayotoka hapa kwenda kuyafanyia kazi na hatua wanazochukua zionekane kwamba zimekidhi haja kwa mujibu wa Katiba, kwa mujibu wa sheria zetu lakini zionekane kwamba serikali kweli nayo inachukia. Kama si hivyo Mhe. Spika, wananchi hawana haraka 2015 tukijaaliwa watatuhukumu.

Ninakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kupata fursa kutoa maoni yangu machache juu ya taarifa hii ya serikali ilioko mbele yetu. Pia nimshukuru Mwenyezi Mungu subhanahu wataala kwa kuniwezesha kusimama hapa na nimshukuru Mhe. Waziri kwa kiasi fulani kwa kuandaa ripoti hii ya serikali na kuiwasilisha kwa umakini sana na nadhani wajumbe wote tumeipitia na tumeifahamu.

Mhe. Spika, mimi sitakuwa na mengi kwa sababu siiwafiki na kwa kuwa siiwafiki nitakuwa sina mengi ya kusema. Lakini katika hoja ya mwanzo niseme kuwa kuna risiti zilizotolewa ambazo zinaonesha viwango tofauti ya malipo. Sasa risiti ni ushahidi na risiti imetolewa na Shirika wenyewe lakini bado serikali inatafuta ushahidi, mimi ninawaambi ushahidi mmoja ni hii risiti iliyotolewa kama mnapeleka Polisi pelekeni. Sasa Polisi ikafanye nini na uchunguzi umefanywa, pelekeni hii risiti kule Polisi ikafanyiwe kazi sio Polisi ikachunguze. Ama kama hii risiti hamuiamini ni suala jengine, inawezekana ikawa hii kazi iliyofanywa na kamati hamuiamini.

Halafu Mhe. Spika, Kamati ilileta taarifa yake makini hapa Barazani tukaijadili na hatimaye ikawa serikali ikapewa iyafanyie kazi. Matokeo ya kazi hii serikali imekaa mfano kwa wacheza bao, bao lina kete zake, wachezaji wawili wanakaa, wanasafiri huku wamekaa kitako, wanatoa kete moja wakiitia hapa wanatoa hapa wakitia pale, lakini kete ndio zile zile na kila mmoja anakula, ana mtaji na anasafiri na anatua hapa. Sasa hoja ya pili na hoja ya nane kuna watu eti wamechukuliwa hatua kwa kuhamishwa walipokuwa na kupelekwa sehemu nyengine huku nikucheza bao kete ndio ile ile umeitoa kishimo hiki umeitia kishimo chengine.

Uhamisho si adhabu, kama ni adhabu itakuwa mimi maana ya adhabu siijui. Kwa hivyo leo nipewe nini maana ya adhabu kwa sababu kutoka sehemu moja ya kazi kwenda nyengine kwa taratibu za nchi hii ni kawaida. Lakini leo kuwa serikali inatafsiri kumtoa mtu hapa na ikamuweka pale kuwa imemuadhibu mimi nadhani Mhe. Spika, katika ripoti hii walioadhibiwa na sijui kwa nini wakaadhibiwa ni Meneja Mkuu, na Meneja wa Pemba. Kwa sababu onyo ni adhabu tena kubwa, kwa sababu onyo linabakia katika faili la mfanyakazi na kama pana utendaji makini wa serikali hawa tayari wamewadumaza, wamewadumaza kwa nini? Hoja ya serikali kuwa wameshindwa kusimamia majukumu yao ndio maana wakaonywa lakini hawa mmewaonea. Kwa sababu hawa waliofanyiwa kama ni wizi au ubadhirifu wao mmewafanya kama mnavyocheza bao tu kutoa kete hapa ikaishia pale sasa huyu unamuadhibu kwa nini?

Sasa Mhe. Spika, kama hawa wameadhibiwa kushindwa kusimamia serikali itaadhibiwa na nani kushindwa kutekeleza maagizo ya Baraza sio ya Kamati, nani ataionya serikali, kama uhamisho ni adhabu nani ataihamisha serikali.

Mhe. Spika, mimi huko nyuma nilikuwa mwalimu wa skuli za msingi na ilifika pahala ikawa nina uongozi mdogo huko skuli, kuna baadhi ya walimu huwa hawachukui zile *marks* za watoto

lakini mwisho wa *term* pale anakaa tu anamtazama Juma Ali akiwa hodari anamtilia 10, anamtazama Maryam Saidi, hodari sana anampa 15, hivi ndivyo ilivyokaa serikali, imekaa aa, hatuna vya kuliambia Baraza lakini tutunge tunge kidogo tukawadanganye.

Mhe. Spika, serikali ya watu wazima na sisi ni watu wazima kuliko wao. Niungane na wenzangu kuwa serikali isifanye masihara, imepelekewa ripoti ya kweli, itafute ukweli, watekeleze ukweli. Kwa mawazo yangu mimi wamewaacha wenye hatia na wamewabandikiza hatia watu wengine, huku ni kuwaonea na serikali inataka iwe adilifu.

Hapa Mhe. Spika, nilipokuwa mwanafunzi siku moja kwenye *debate* kulikuwa na *motion* iliyosema, *'mass should sat a side, so as to maintain justice*'. Kama serikali hii ni makini na kama ilikusudia kutekeleza sheria lazima huruma aziweke upande watekeleze sheria. Wasione tu kuwa Mohamed Haji Khalid yuko hivi aa, Mhe. Abubakar Khamis Bakary yuko hivi ndio, kila mtu atendewe haki sera yangu mimi ni haki sawa kwa wote. Kwa hivyo, serikali Chama cha Mapinduzi nao wana haki tunatofautiana tu wao hawako sawa kwa wote, lakini na wao wanayo haki. Kwa hivyo, sera mbili hizi ziunganishwe ili serikali itende haki isimuonee mtu lakini kadhalika isimpendelee yeyote.

Mhe. Spika, kama hali ya serikali ndio hii kwa kweli tuko pabaya sana. Serikali badilikeni kitu kinapotoka hapa kinatoka katika chombo kikubwa sana na nyinyi ni wakubwa sana mkae mujadili na mkileta kitu iwe mjadala wetu ni mfupi tuone haya, aibu na fedheha kuleta ripoti ya serikali mara kwa mara ikawa inarudishwa. Hivyo jamani hamuoni vibaya nyinyi kuwa kila siku ripoti zenu tunazirudisha, hamtanabahi angalau? Hatari hii tena hatari sana.

Mhe. Spika, nimesema sitaki nichangie kwa sababu sina la kuchangia, nikichangia itakuwa naikubali na nitakuwa nakubali ambalo silikubali. Kwa hivyo, nimalizie kwa kusema ripoti hii siungi mkono. Ahsante sana.

Mhe. Mohamed Mbwana Hamad: Mhe. Spika, awali ya yote na mimi nachukua nafasi kumshukuru Mwenyezi Mungu (*S.W*) kutujaalia jioni hii kuwepo hapa katika kukamilisha au kutekeleza majukumu yetu ya kitaifa. Lakini la pili natoa shukurani zangu za dhati kabisa kwako kunipa nafasi hii ya magharibi haya angalau na mimi nikachangia mawili matatu juu ya Ripoti ya Serikali iliyoko mbele yetu.

Mhe. Spika, ripoti hii kwa kweli ni muhimu sana kwetu Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi pia ni muhimu kwetu na wananchi wetu kuisikia. Vile vile ni muhimu serikali na wao kusikia kile ambacho kinajadiliwa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika ripoti hii iliyoko mbele yetu.

Mhe. Spika, wakati Kamati ya *PAC* ilipokuwa ikihojiana na baadhi ya watendaji basi kuna watendaji wa Shirika la Umeme walisema hivi, “ah! Kwa kweli kamati zinapita kila siku hapa lakini hakuna matokeo yoyote yanayofanywa nyinyi mnachukua pesa zenu mkijaa matumbo tu basi, laini hakuna ambacho kinaendelea cha utendaji wa serikali”.

Kwa kweli Mheshimiwa watendaji hawa walikuwa na wasi wasi wa kwamba kamati hizi zinapita lakini hakuna hatua yoyote ya serikali ambayo inachukuliwa baada ya matokeo ya kamati kumaliza kazi yake. Na leo watendaji hawa wa serikali ambao walieleza suala hili wanatusikiliza. Naiomba serikali iwe makini sana katika kutoa ripoti kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi itakapokuwa ripoti si makini kama iliyoko mbele yetu kwa kweli wananchi wetu wana masuala mengi ya kujiuliza.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo niseme kwamba na mimi niungane na wenzangu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Chambani kutokuiunga mkono ripoti iliyopo mbele yetu.

Mhe. Spika, mimi maeneo yangu nitakayoyachangia ni machache, kwanza nitachangia kwenye utangulizi ukurasa wa pili nanukuu unasema hivi:

> "Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imepokea Ripoti ya Kamati ya *PAC* ya Baraza lako kuhusu Shirika la Umeme Zanzibar (*ZECO*) kwa moyo mkunjufu na kulifanyia kazi kwa umakini mkubwa na uadilifu wa hali ya juu ili kuona mapungufu yaliyooneshwa katika ripoti hiyo yanafanyiwa kazi kwa maslahi ya nchi yetu na vile vile wale walioguswa wanafanyiwa haki na uadilifu kufuatana na matakwa ya sheria za nchi yetu".

Mhe. Spika, sentensi ni nzuri sana lakini utekelezaji wake uko wapi, kwamba kwa moyo mkunjufu na kuifanyia kazi kwa umakini hivyo umakini Mhe. Spika, ni mtu kupoteza mamilioni ya shilingi akatolewa katika ofisi hii na kuhamishwa katika ofisi nyengine huu ndio uadilifu wenyewe? Mheshimiwa hili ni tatizo.

Lakini nikienda katika *paragraph* iliyoko chini Mhe. Waziri alisema kwamba, 'kwa kweli taarifa hii imetuonesha mambo mengi ambayo yanapaswa kufanyiwa kazi na serikali ili kuimarisha utendaji wa shirika kwa maslahi ya taifa letu'. Mimi niseme kwamba sentensi hii iko kinyume chake, hii itafanyiwa kazi kwa maslahi ya watu binafsi kama tulivyoiona katika maelezo yaliyomo ndani ya ripoti hii.

Mhe. Spika, kwa kweli niiombe serikali iwe makini sana katika kutekeleza majukumu yake. Rais Ali Mohamed Shein amesema tusifanye kazi kwa mazowea. Mimi labda nimuulize Mhe.

Waziri, tumefahamu vipi suala la kuwa tusifanye kazi kwa mazowea. Kwa sababu tulikotoka ni haya haya watendaji kupoteza mamilioni ya shilingi hakuna hatua inayochukuliwa na hivi sasa yanapotea mamilioni ya shilingi hakuna hatua inayochukuliwa, nini maana ya kuwa tusifanye kazi kwa mazowea?

Mheshimiwa nikiendelea niende katika hoja nambari moja ambayo inasema hivi, "Wateja kupewa risiti zenye kiwango kidogo kuliko malipo halisi waliyolipa', ukienda katika kifungu cha chini yake hapo Mhe. Spika, maelezo ya serikali kuhusu hoja hii ni kwamba, serikali inakubaliana na mapendekezo yaliyotolewa na Baraza lako tukufu na tayari hatua imeshachukuliwa na Shirika la Umeme kwa kuliarifu Jeshi la Polisi kuanza kuchukua hatua za kufanya uchunguzi wa malalamiko ya wateja waliolalamikiwa kulipa fedha nyingi lakini risiti walizopewa zimeandikwa fedha kidogo.

Mhe. Spika, mimi nataka nikwambie kwamba, kamati imefanya kazi kubwa imeripoti vitabu vitatu. Kitabu cha kwanza ni ripoti iliyo na maelezo ya jumla, lakini kitabu cha pili kina vielelezo kuanzia nambari moja mpaka 50 na kitabu cha tatu kina vielelezo kuanzia nambari 51 mpaka 100; ina maana vielelezo 100 vimepatikana katika ubadhirifu pamoja na upotevu na wizi wa Shirika la Umeme hivyo leo tunataka ushahidi gani mwengine. Vielelezo vimetolewa ndani ya vitabu hivi, sasa ikiwa vielelezo hivi serikali haijaviamini tunawaomba viongozi wa serikali suala hili walifuatilie kwa haraka sana katika hiyo njia ambayo wao wanaiona ni sahihi ili mwenye haki apewe haki yake na anayelazimika kuwajibika awajibike ili nchi yetu iende vizuri katika uadilifu wa kazi.

Mhe. Spika, niende katika ukurasa wa 21 Hitimisho, hitimisho linazungumza katika *paragraph* ya kwanza kati kati hapo. Vile vile naomba nichukue fursa hii kwa mara nyengine tena kumshukuru Mhe. Hija Hassan Hija, Mwakilishi wa wananchi

Jimbo la Kiwani kwa ujasiri wake na uzalendo wake wa kuibua hoja ambayo kwa kweli imetuonesha mapungufu tuliyokuwanayo katika shirika, mapungufu ambayo serikali imeweka nia ya dhati ya kupambana nayo si kwa Shirika la Umeme tu bali kwa taasisi zote za umma. Mhe. Spika, katika sentensi hii mimi ningeiomba serikali kama Mhe. Hija Hassan alivyoonesha ujasiri wake juu ya kuibua haya basi na serikali ioneshe ujasiri juu ya kuwatendea haki wale ambao wamechezea mali ya serikali.

Mheshimiwa kutenda haki unapomchinja mnyama kama ng'ombe, mbuzi, kuku au kondoo miongoni mwa kumtendea haki ni kukinoa kisu kikawa kikali ili usimchikiche (kukata kwa kisu kisicho na makali). Kwa hivyo, serikali tunaiomba iwe makini inoe kisu isiwachikiche hawa, jamani tunawafumbia macho wabaya mpaka lini, tukija tukiwachinjia visu ambavyo havina makali tunapata dhambi ili upate thawabu makini ni kuwachinga katika kisi chenye makali ndio haki yao. Kwa hivyo, ujasiri aliyouonesha Mhe. Hija tunaiomba serikali ioneshe ujasiri huu huu juu ya kuwatendea haki wote wanaohusika na ubadhirifu na wizi wa mali ya umma.

Hivi sasa katika jimbo langu kuna maeneo mbali mbali hayana umeme kumbe uwezekano wa kufikishwa umeme katika maeneo yale, upo lakini ubadhirifu umekuwa mkubwa, wizi umekuwa mkubwa. Mhe. Spika, kwa kweli inasikitisha sana na inauma sana kila baada ya kipindi hapa tunapewa vitabu mbali mbali vinavyohusiana na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuna mabilioni yanapotea lakini hakuna hatua inayochukuliwa na leo ripoti hii imekuja tena katika Baraza la Wawakilishi, tunaiomba serikali ichukue hatua inayofaa ili mwenye haki apewe haki yake na anayestahiki kuwajibika awajibike.

Mhe. Spika, kwa kuwa wakati ni mkubwa na kuna miongoni mwetu wanataka kuchangia na mimi nilisema kwamba nitoe

maelezo yangu machache juu ya haya na mwisho niseme kwamba, kwa niaba ya Wananchi wangu wa Jimbo la Chambani siiungi mkono hoja hii hata kwa asilimia moja. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi angalau niseme mawili matatu yahusianayo na Ripoti hii ya Utekelezaji wa Serikali juu ya Maamuzi ya Baraza.

Mhe. Spika, tofauti na pale mwanzo maelezo yaliyotolewa humu katika karatasi baadae baada ya Mjumbe wangu kutoa hoja Mhe. Waziri alikubali kurekebisha, kwamba hii ni Taarifa ya Serikali au ni Hoja ya Serikali vyovyote utakavyoita juu ya utekelezaji wa maazimio au utekelezaji wa serikali juu ya maagizo ya Baraza la Wawakilishi. Hapa Mhe. Spika, tuna tatizo kidogo na sijui hili ni kutokana na uelewa au ni kutokana na kubabaisha, sijui ni kitu gani, kwamba suala hili katika suala la *PAC* lilizungumzwa wakati wa mjadala ule, *PAC* ilikoma wakati Baraza lilipolichukua suala hili sasa kama ni hoja ya Baraza. Kwa hivyo, nashukuru kwamba Mhe. Waziri baadae aliona baada ya kutanabahishwa na Mjumbe na kumbe vile sasa tunachangia hoja au taarifa ya serikali na kwa kuwa ni taarifa ya serikali sio ya wizara mana ingelikuwa ni ya wizara angelikuja Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati. Lakini kwa kuwa ni ripoti ya serikali ndio maana akaileta mchezaji maarufu hapa au mpikwa chano maarufu Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Na kwa kuwa yeye ni mpikwa chano basi mashetani yote leo yatamuelekea yeye. Mhe. Waziri katika hili kwa kweli astahamili sana kwa kuwa yeye ndiye mpikwa chano wa serikali katika Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, nakumbuka wakati kamati yangu ilipofanya kazi katika shirika kitu cha kwanza wakati ule ilikuwa ni kukutana na wafanyakazi wote wa shirika, tulikutana na wafanyakazi Pemba na wafanyakazi wa Unguja. Nakumbuka tulikumbana na

changamoto kali kutoka kwa wafanyakazi, kwa sababu tuliwaomba mashirikiano yao na wao wakatutanabahisha kwamba hivi Waheshimiwa hasa sisi mmetukusudia nini? Tukawaambia kulikoni, wakatwambia mnakumbuka huko kipindi cha nyuma ilishawahi kuja kamati kama hii lakini matokeo yake kwa kweli kilichotokea ni adhabu kwa wafanyakazi wale walioshirikiana na kamati ya Baraza sasa na leo mnatutafutia janga jengine. Kwa wakati ule mimi sikuelewa, lakini sasa ndio naanza kuelewa vile walivyokuwa wakitwambia. Maana nilishitushwa sana, naomba niseme kwamba wakati tulipokuweko Pemba alijitokeza mfanyakazi mmoja maarufu Kaduara, yeye akajitolea kinagaubaga kwamba mimi nitasema kweli daima na uongo kwangu mwiko, alisema hivyo kwa sababu hiyo ndio kauli anayoiamini kwamba atasema kweli daima na uongo kwake mwiko na kweli kipindi chote akakubali wakati mwengine kwa gharama zake kuisaidia kamati.

Sasa Mhe. Spika, nakumbuka kwamba tunazo kanuni zinazotulinda kama Waheshimiwa lakini vile vile sheria nakumbuka inawalinda mashahidi wanaokuja mbele ya kamati, nakumbuka mashahidi wanalindwa kwa mujibu wa sheria, sheria Nam. 4 ya mwaka 2007 kama sikosei sasa leo vyereje kwa shahidi aliyejitokeza katika kuisaidia kamati yako tukufu leo akakubwa na yeye na adhabu. Kwa sababu uhamisho huu unaambatana na adhabu kama waliyoadhibiwa wengine. Kwa hivyo, kwanza Mhe. Spika, naomba nitoe hoja kwamba vyovyote itakavyofanywa lakini kijana huyu alindwe kwa mujibu wa sheria zetu vyenginevyo itakuwa ni aibu kubwa sana na ni kukivunjia heshima chombo hiki kitu ambacho sisi wengine hatukubali hilo litokee. Kwa hivyo naomba hilo serikali i-*take note.*

Mhe. Spika, leo serikali nadhani isingelikuja na mzigo wote huu kwa sababu kwa mujibu wa hoja hapa zilizojibiwa ni hoja nambari 36, 38 na wakati ripoti iliyopitishwa na Baraza hili ilitoa mapendekezo 11 na mapendekezo mawili aliyoyaongeza Mhe.

Hamza Hassan Juma na Baraza likaridhia kwa kauli moja, jumla yalikuwa ni mapendekezo 13 kwa hesabu zangu za kishamba sasa ilikuwa serikali ije na hoja 13 tu zinazoji9bu namna serikali ilivyotekeleza hoja hizi 13, lakini serikali ikarudia tena kuzichambua zile ripoti za *PAC*. Hii maana yake ni kuichambua tena ile ripoti ya *PAC* wakati sisi tulishawarahisishia kazi kwa hoja 12 ambazo zote tulizijumuisha tukazitia kwenye hoja hizo 13. Sasa Mhe. Spika, nadhani tungelipata hoja hizo kwa ufupi namna serikali ilivyojibu hoja moja baada ya nyengine katika maeneo hayo 12.

Mhe. Spika, mimi leo sitaki niguse shirika nataka niguse tu yahusianayo na mamlaka ya chombo hiki pamoja na mamlaka ya serikali. Kwa sababu hapa inaonekana kidogo pana tatizo, pana mvutano au kutofahamiana licha ya semina elekezo iliyokuja kufanywa, lakini bado inaonekana somo hili halijaeleweka vizuri kwamba Baraza lina mamlaka gani na serikali ina mamlaka gani.

Mhe. Spika, Baraza la Wawakilishi ni sote Wawakilishi tuliochaguliwa ambao tunaingia katika chombo hiki kwa milango tofauti, lakini kwa mifumo yetu ndani ya Baraza hili na serikali imo ndani ya Baraza hili. Mifumo ya majadiliano Mhe. Spika, hujadiliana lakini mwisho wake hutoa maamuzi na kawaida tunapotoa maamuzi tumekuwa tukishuhudia katika Mabunge kadhaa duniani serikali ikiomba kwa Bunge au kwa Baraza ili kuakhirisha mjadala na kuipa nafasi zaidi serikali iende ikajitayarishe. Tumekuwa tukishuhudia mara nyingi serikali kuomba ipewe muda zaidi kama jambo likiwa halijaeleweka vyema au serikali haina majibu ya kutosha, serikali ipate muda wa kwenda kutafuta zaidi. Hayo tumekuwa tukishuhudia mara nyingi maana yake nini, maana yake tunapofika pahala sasa Baraza likaamua ikiwa ni pamoja na serikali ndani yake maana yake hilo sasa halina mjadala tena, tunapofika pahala Baraza kwa umoja wetu na nakumbuka kipindi kile Baraza kwa asilimia mia moja sikuona mkono uliokataa, kwa asilimia mia moja tuliunga mkono juu ya

maamuzi ya Baraza na juu ya mapendekezo 13 kwa ajili ya serikali kuyachukua na kwenda kuyafanyia kazi.

Mhe. Spika, tafsiri yangu nilidhani kwamba mapendekezo haya yatakwenda kufanyiwa kazi na serikali moja baada ya jengine kwamba tayari sote kwa pamoja kipindi kile tuliridhika na Ripoti ya *PAC* ndio maana yake. Tafsiri ni kwamba kipindi kile cha mjadala pamoja na serikali sote tulikubaliana kwamba yaliyomo katika ripoti ndio sahihi vyenginevyo serikali kama ingelikuwa na majibu ya ziada au kama ina tofauti kidogo ingeliomba muda kwenda kutafakari na baadae kuja na maamuzi mengine humu. Lakini kufika pahala tukakubaliana sote, nadhani Mhe. Spika, siku ile ulisema vizuri sana, bahati mbaya ile *hansard* sikuichukua lakini kwamba tunaiagiza serikali iende ikayafanyie kazi mapendekezo haya. Sasa leo kurudi tena hapa tukaambiwa hili linapelekwa polisi liende likachunguzwe, hili linapelekwa hapa likafanywe hivi, hili si kweli, kwa kweli Mhe. Spika, ni kuiaibisha kamati yako iliyofanya kazi lakini vile vile ni kuliaibisha Baraza hili ambalo siku ile tulikaa kwa siku nzima. Nakumbuka mwenyekiti wako wa Kamati ya *PAC* alisimama si chini ya masaa matatu katika ukumbi huu kuzungumzia na tulikuja na *volumes* ikiwa ni taarifa pamoja na vielelezo vyenye ushahidi hatimaye tukafika katika makubaliano.

Kwa hivyo ninachokusudia kukisema hapa Mhe. Spika, maamuzi yanayofanywa katika Baraza lako hili ni maamuzi ambayo yanahusisha Baraza ikiwa ndani yake kuna serikali na bahati nzuri serikali inaongozwa na Makamu wa Pili wa Rais katika chombo hiki. Sasa leo kurudi tena wakenda kuyaundia tume maamuzi haya kama vile ambavyo kamati ya kwanza Mhe. Spika, itakuwa bado hatujaelewana juu ya dhana hasa na mamlaka ya chombo hiki kama yalivyoelezwa katika Ibara ya Tano ya Katiba yetu ambayo imesema wazi wazi kwamba,

> "…Mamlaka ya Kutunga Sheria na Kusimamia Utekelezaji wa Shughuli za Umma…"

Inaelezwa wazi wazi katika Baraza hii na serikali nayo kwa umoja wake inawajibika kwa chombo chetu hiki.

Mhe. Spika, nataka niseme kwamba kazi iliyofanywa ilikuwa ni ya uchunguzi na tulifanya uchunguzi kwa kina sana, na kwa mara nyengine nataka niipongeze sana *management* ya shirika kwa namna walivyoisaidia hasa Meneja Mkuu, alivyoisaidia kamati yangu katika kutekeleza kazi zake Meneja Mkuu Unguja na Msaidizi wake aliyeko Pemba pamoja na wafanyakazi. Tulikuja na vielelezo vya kila aina ni kwa mara ya kwanza au mara ya pili vielelezo vilivyotungiwa buku kuna buku kubwa hapa la vielelezo tu. Sasa leo tunapofika pahala vielelezo vya kila aina maana yake wizi wa risiti na risiti ikishapatikana kuna uchunguzi gani tena, wizi ukishapatikana risiti yenyewe ni hii inatoka ***NNBC*** sijui kuna uchunguzi gani tena hapo kama si namna ya kutaka kuchakachua, mimi nadhani hilo si sahihi.

Katika mambo yote 13 yaliyoelezwa humu kama mapendekezo ya kamati Mhe. Spika, mimi niliyagawa katika sehemu tatu, kuna mapendekezo yaliyohusiana na makosa ya kinidhamu binafsi nahisi makosa ya kinidhamu yaliyochukuliwa kwa uzito wa makosa kwa kweli hatua zile ni ndogo sana. Kwa hivyo, hilo sina vya kulisemea lakini ninavyodhani kwa makosa ya kinidhamu kwa baadhi ya watendaji kwa kweli ni madogo sana, kwa sababu kuna wizi wa macho macho na wizi wa wazi wazi, watendaji wameliibia shirika.

Mhe. Spika, makosa ya kijinai vile vile katika mapendekezo 13 ni miongoni mwao, kuna makosa ya kijinai na makosa ya kijinai kwa sababu kamati yako ya uchunguzi ilishafanya kazi na kamati yako iliwasilisha ushahidi mimi sidhani kama ni sahihi kurudi tena ukaiambia polisi ichunguze sidhani kama huo ni utaratibu, kwa kiwango cha hatua yetu hii ilikuwa sasa ni jukumu la serikali kuchukua *package* yote na kumkabidhi *DPP* kwa sababu yeye ndiye mwenye dhamana sasa ya kupeleka kesi Mahkamani,

yeye *DPP* ana mamlaka ya kupima kama kuna ushahidi wa kutosha akapeleka kesi Mahkamani. Hakuna ushahidi wa kutosha ataachilia kesi, sisi hatuna lazima kwamba kila kitu kichukuliwe hatua, kipelekwe mahakamani hatuna ulazima huo. Tunachotaka sisi tujue kwamba haki imetendeka basi hilo tu na serikali imetimiza wajibu wake, hilo ndilo *interest* yetu kubwa na wananchi wa Zanzibar hiyo ndio *interest* yao si kitu chengine.

Mhe. Spika, jambo jengine la tatu ambalo ni miongoni mwa mapendekezo haya ya Baraza ni suala zima la uchukuliwaji wa hatua baadhi ya maeneo. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa kaeleza kwa vizuri sana. Lakini bahati mbaya humu hata katika ripoti iliyoletwa na Mhe. Waziri haya hayakuonekana, kuna maoneo ambayo mdhibiti kaagizwa afanye uchunguzi maalumu hakuna kitu chochote kilichogusa juu ya hilo.

Kuna ile taarifa juu *fault* ya umeme iliyokuja kutokea hakuna chochote kilichoelezwa katika hicho. Kwa hiyo, kwa ujumla Mhe. Spika, kwa lugha rahisi na nyepesi *nataasafu* kusema kwamba serikali bado haijataka hasa hasa kuwajibika kwa chombo hiki na yote hii ni kwa dhamira ya kutudhalilisha sisi Wawakilishi.

Mhe. Spika, nataka leo nikwambie kwamba sasa tunajisikia wazito sana katika kufanya maamuzi na mimi sishawishiki tena kwa Baraza hili kuunda Kamati. Na mimi nataka nisema kuanzia leo sitounga mkono hoja yoyote ile inayohusiana na uundwaji wa Baraza wa kamati Teule za Baraza kwa sababu ninavyodhani ni upotezaji tu wa fedha chache za wananchi wetu.
Tumeshaunda kamati nne teule, kuna Kamati ile ya kwanza ya kuchunguza mambo mbali mbali mpaka leo ripoti hiyo inapigwa danadana hapa haijafikia mwisho. Tuliambiwa itakuja mpaka leo hakuna kitu.

Kuna ripoti ya Manispaa Mhe. Salmin Awadh Salmin kasema mpaka kapata kabrasha moto moto sasa hivi linatoka jikoni sasa

ndio anakabidhiwa. Hii ilikataliwa na ile ya kwanza ilikataliwa na ya Manispaa nayo ikakatiliwa hii ni mara ya tatu inaletwa tena. Kabrasha moto moto analo Mhe. Salmin Awadhi Salmin analo mkononi.

Ripoti ya tatu ni ya *ZECO* ambayo nina hakika leo tutaikataa tutairejeshea serikali, nina hakika na sijui *allahu yaa alam* ripoti ile ya Kamati ya Ardhi sijui inayayukia wapi sijui.
Sasa Mhe. Spika, sisi tunaunda kamati tu tunafuja fedha za wananchi matokeo hakuna. Mimi sishawishiki tena kwa kipindi cha miaka miwili hichi kuunda kamati kama ikiwa ni kuyaachia mambo yaende kama yalivyo basi ndio hivyo hivyo.
Mhe. Spika, kwa maana hiyo basi kwa sababu ripoti tatu zimekuja na zikakataliwa, tafsiri yake nini?

Kasema pale Mhe. Mohd Haji Khalid, hii ni kufeli kwa serikali ndio tafsiri yake na kwa nchi ambazo zimeendelea sana katika demokrasia kwa kweli, Waziri moja kwa moja anatakiwa aachie ngazi tu. Lakini kwa sie ni kitu cha kawaida tu haina shida tuendelee tu. Lakini hii ni kufeli moja kwa moja kwa serikali mara tatu maana yake nini? Kwa hivyo, ndio tafsiri ya kwanza Mhe. Spika.

Tafsiri ya pili ni kukidhalilisha chombo hichi kama nilivyosema sasa Wajumbe wako tunajisikia shida sana maana yake si kamati hizi za *selected committees* tu. Lakini hata zile kamati nyengine za kawaida tunakwenda kufanya nini huko. Maana matokeo ya kufanya kazi ile ni kupata matokeo na kuja kuyapeleka hapa na serikali kuchukua hatua. Lakini inapofika pahala utendaji wenyewe ndio huu inakuwa ni shida na si shida tu, kwamba tunahangaika sie tunajuwa kwamba ni wajibu wetu kwenda kufanya kazi kwa kila kipindi kazi za kamati. Lakini matokeo yake kuna fedha zile za wananchi zinatumika hilo ni tatizo tunapaswa tuliangalie tena kwa mara nyengine pale.

Lakini Mhe. Spika, yote tisa kumi nchi zote zilizoendelea zimeendelea kwa sababu ya kuwajibika kwa serikali katika masuala mbele ya chombo cha wananchi. Ikiwa tutafika pahala hakuna uwajibikaji na hakuna uwajibishwaji tafsiri ya moja kwa moja kwamba tutachelewa sana kupiga hatua za kimaendeleo. Wale waliokuja juu kama wanakuja kuomba kazi kama wale wazungu sijui wamekuja kuomba nini.

Lakini wale wamekuja kwa ajili gani, sijui kama kutugaia pesa au vipi. Lakini fedha hizi tunaomba na tunakopeshwa, tunadhalilika kwenda kukopa, Mhe. Rais mzima anapotoka kwenda kupia magoti jamani kudhalilika! Rais anapotakiwa atoke na kwenda kutembelea sehemu nyengine. Lakini Rais wetu anapokwenda kupiga magoti masharti mengine magumu, tunawadhalilisha viongozi wetu kwa ajili ya umasikini wetu. Hebu tufike pahala hasa tuone huruma na kwa utaratibu huu tunaokwenda nao wa kwamba kila anaefanya kosa huyo ni mwenzetu Zanzibar sote tunajuana ndio kauli mbiu ilioko. Hiyo kauli mbiu kwa sote ni sie kwa sie, mwanashangazi na mjomba, kuna miaka mia mingine leo tunasheherekea miaka 50. Lakini hii ndio miaka 50 ya utendaji wa serikali.

Mhe. Spika, tutachelewa sana kupiga hatua za kimaendeleo, waliopiga hatua za kimaendeleo ni waliokuwa makini kwamba mtu yeyote anaecheleza fedha za umma anawekwa pembeni anakuja anafanya kazi. Lakini msamiati huo kwetu sie hatujui.
Sasa Mhe. Spika, kwa kuwa hizi ripoti zinaendelea kukataliwa tu hebu sasa tunaomba muongozo wako, kwa sababu mwisho wa siku sote tunakuangalia wewe. Hicho kiti uliochokalia ni kiti kitukufu na kina siri yake hicho. Mtu wa kawaida hakai hapo kina siri yake. Mhe. Spika, tunaomba muongozo wako hili likitokea kwamba ripoti wa kwanza imekataliwa, ya pili imekataliwa, na ya tatu itakataliwa. Sasa muongozo wako tufanye nini chengine?

Baada ya hayo Mhe. Spika, mwisho mimi nataka Mhe. Mohammed Aboud Mohammed, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa mara nyengine arudi na ripoti yake. Nakushukuru sana. (*Makofi*).

Mhe. Salmin Awadh Salimin: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kutoa maoni yangu au mchango wangu juu ya maelezo ya Serikali hii ya Umoja wa Kitaifa juu ya hoja mbali mbali za Baraza hili zinazohusu utendaji wa Sherika la Umeme.

Mhe. Spika, nimesimama hapa kwa unyonge sana tokea nipokee ripoti hii nimekuwa mnyonge kweli na kwa sababu inafika pahala ninakuwa hata sina la kusema. Kwa sababu mimi mmenipa madaraka hapa kwamba ndio Mnadhimu wa CCM katika chombo hiki nina masononeko makubwa sana juu ya utendaji huu wa serikali hii ya Umoja wa Kitaifa, mbayo wananchi walikuwa na matumaini makubwa sana kwamba katika kipindi hiki cha miaka mitano hii basi wangeterajia kuona mabadiliko makubwa. Jambo ambalo nadhani itakuwa ni ndoto.
Mhe. Spika, baada ya kupokea ripoti hii nilichokiona cha kwanza ni kwamba serikali haitaki kufanya kazi na chombo hiki. Hilo ni jambo nililoliona tu kwamba bado kuna nafasi tena kubwa kati ya serikali na chombo hiki cha wananchi na kwa kweli katika hali ya demokrasia na Utawala Bora hili ni jambo hatari.

Mhe. Spika, tumeshuhudia hapa Kamati Teule ambazo Mhe. Rais amekuwa akiziunda Kamati Teule iliundwa kwa kuzama kwa meli zile. Kamati Teule ya kwanza na ya pili na tumeshuhudia hatua zinazochukuliwa na serikali baada ya matoke ya ripoti zile na wananchi sote tunakuwa tunaridhika. Lakini inasikitisha sana kwamba chombo hichi cha wananchi ambacho kimepewa mamlaka ya kuisimamia serikali kinapounda kamati zake na kutoa ripoti basi hakuna hatua madhubuti zinazochukuliwa na baada yake ripoti zile zinakataliwa na

zinakataliwa si kwa sababu tu zinakataliwa lakini hazina yale matokeo yaliyotarajiwa ni ripoti za ubabaishaji tu.

Lakini ninachotaka kusema Mhe. Spika, wenzetu lazima wakumbuke kwamba chombo hiki ni chombo kikubwa ni chombo ambacho kina heshima kubwa katika nchi. Hufika pahala ikawa kama chombo hichi tunakidharau tutakuwa tunajidharau sisi weneywe. Hili lazima wenzetu wafahamu kudharau chombo hiki maana yake ni kujidharau wenyewe. Ni kweli serikali ndio yenye mamlaka ndio yenye uwezo, ndio yenye hatua na hakuna lolote litakalofanyika. Lakini ninachosema kwamba hii ni kujidharau sisi wenyewe, kwasababu chombo hiki ni chetu ni chombo cha wananchi kinasimamia serikali na kinatakiwa kiheshimike na kisidharaulike tunajidharau wenyewe.

Mhe. Spika, juzi nakumbuka katika taifa kubwa duniania Marekani, Rais wa Marekani Barak Obama umekwamishwa Mswada wake walioupeleka Bungeni juu ya kutaka idhini ya kukopa na Bunge lilikataa, alilazimika Rais Obama, alikuwa tayari ameshapanga ziara zake za kutembelea nchi mbali mbali na hatimae aliaakhirisha ziara zake. Mwenzangu hapa ananambia kuwa hata Balozi zilifungwa, hata wafanyakazi walizuiliwa kwenda makazini mpaka pale walipofikia makubaliano juzi na akashukuru akasema *alhamdulillah* huu ndio uzito wa chombo hiki.

Mhe. Spika, sisi hatutaki kwenda huko, sisi tunataka mashirikiano ya chombo hiki na serikali kwa sababu lengo letu moja na dhamira yetu moja sote tunawatumikia wananchi, sote ni waajiriwa wa wananchi. Katika hili hakuna haja ya kuoneshana umwamba wananchi wanatarajia kupata maendeleo katika nchi yao. Sisi tumechaguliwa na nyie mmechaguliwa, Rais amechaguliwa na wananchi na sote ni waajiriwa wa wananchi. Sasa kama tutafika pahala tuonekane kuna *gape* si dhani kama hiyo ni baraka katika nchi si baraka katika nchi.

Kwa hivyo, mimi niiombe sana serikali katika masuala kama haya yanapofikishwa mbele ya serikali lazima tuthamini na tuone umuhimu wa jambo hili ambalo tuko pamoja tusichukulie dharau tu, hata tukikataa/ hata wakikataa hakuna chochote, hili lina madhara mbele yetu. Hatutaki tutumie nafasi yetu ya kuwajibishana hapa serikali kwa pamoja inawajibika katika chombo hiki. Nyinye ndio wenye wajibu wa wakuwajibisha. Serikali ina wajibu, inawajibisha watendaji wake, tusingependa kufikia pahala tukawajibishana kwa kutumia vifungu vya Katiba kuwajibishana haipendezi hata kidogo. Kwa sababu sisi ni binaadamu tumepewa akili ni waungawa kwa nini tufikishane hapo?

Mimi nilikuwa najiuliza wakati Mhe. Mohammed Aboud Mohammed, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais alipokuwa akitoa hii ripoti ya serikali, mimi Mhe. Mohammed Aboud Mohammed, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais namfahamu sana na ni katika mawaziri waliokuwa makini sana. Sasa mimi nilikuwa najiuliza hii ripoti ameandikiwa au kaandika mwenyewe? Mimi nilikuwa napata maswali mengi hata nilipotoka hapa na Mhe. Mohammed Aboud Mohammed, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, wakati mwengine ripoti kama hizi usikubali kuzisoma hapa zitakushushia hadhi yako bure. Hizi sio ripoti katika jambo zito kama hili na ukakubali kuzisoma mimi naamini hizi hukuziandaa wewe, umesoma tu kwa naiba ya serikali, sijui kaandaa nani.

Lakini hii ni aibu Mhe. Spika, ni aibu kubwa kupita kiasi kwamba serikali ambayo ina viongozi tunaowatarajia, tunaowategemea wasimamie masuala ya utendaji katika serikali. Hatua zinakuwa kama hizi za kubabaisha babaisha. Kwa kweli Mhe. Spika, jambo hili ni baya kwa kweli na linakatisha tamaa.
Na mimi nikubaliane na Mhe. Omar Ali Shehe kwamba basi sasa iwe imetosha kuunda Kamati Teule, hii iwe ndio ya mwisho nikubaliane kabisa na Mhe. Omar Ali Shehe twende tunakokwenda, tutajua mwisho tutafikia wapi. Lakini hii iwe

ndio ya mwisho na imetosha. Kwa sababu inaonesha dhahiri kwamba hakuna mashirikiano katika vyombo hivi tunapoteza pesa za umma bure, licha ya pesa tunapoteza nguvu nyingi.

Tulipokuwa sisi tunasimamia Ripoti Teule ya Baraza la Manispaa tulipoteza nguvu nyingi tunafika mpaka usiku tukiwa na matumaini kwamba tunataka tutengeneza, tunataka kujenga chombo kilichokuwa imara. Lakini matokeo yake ni kama haya ubabishaji.

Mhe. Spika, mimi nataka kukwambia sisi Wajumbe wa Baraza lako tukufu tuna akili na tunajua tunachokifanya na wasifikiri wenzetu kwamba sisi hatuna akili kwa kuwa tuko huku nyuma wakaona labda wao ndio wenye akili kuliko watu wengine. Unapofanya kitu kwa uaminifu tunajua hiki unakifanya kwa uaminifu, na unapobabaisha tunajua kwamba hapa kuna ubabishaji hilo wajue na wasifikiri kwamba hatufahamu kwamba hapa pana ubabaishaji ni ubabaishaji tu.

Kwa kweli Mhe. Spika, mimi nina masikitiko makubwa juu ya ripoti hii na nitaeleza baadhi ya maeneo tu. Nilikuwa sitaki kusema mengi, nilikuwa nataka nimalizie. Lakini nitayaeleza juu ya baadhi ya maeneo tu ambapo jinsi gani inaonesha kwamba wenzetu hawa hawakuwa makini katika kuleta ripoti hii.

Kwenye hoja ya kwanza ambapo Mhe. Waziri ameieleza hapa hoja inayozungumzia wateja kupewa risiti zenye kiwango kidogo kuliko malipo halisi yaliyolipwa. Maelezo yote kwa ujumla hayana maana. Lakini niliposhika ni eneo moja tu na nyinyi mtaona jinsi gani serikali ilivyokuwa haiko tayari kushughulikia masuala haya.

Ukiangalia kwenye ukurasa wa 4 naomba kunukuu Mhe. Spika, inasema kwamba:-

" Kwa mujibu wa kifungu cha 44 cha Sheria ya Shirika la Umeme namba 3 ya mwaka 2006. Serikali imemuagiza waziri

anaehusika na sekta ya nishati kuunda kamati za rufaa za wateja ili kushughulikia malalamiko ya wateja, napenda kuwaarifu kwamba hatua za kuunda kamati za rufaaa za wateja zinakaribia kukamilika"

Mhe. Spika, sheria toka mwaka 2006 mpaka leo miaka mingapi? Leo serikali inasema hatua za kuunda Kamati za Rufaa ambayo sheria imemuagiza waziri amaehusika kuunda hii kamati baada ya sheria kufanyiwa kazi. Hii inaonesha jinsi tulivyokuwa hatuwajibiki mpaka yanatokea mambo kama haya tunapewa ripoti kama hii. Sheria namba 3 ya mwaka 2006 tunasema tunakaribia kuunda kamati ya rufaa kusikiliza malalamiko. Hichi ni kitu ambacho kwa kweli hakikubaliki.

Eneo jengine Mhe. Spika, ni hoja namba 2 ambayo wenzangu wameizungumzia. Waheshimiwa wengi wameizungumzia kuhusu fedha za malipo za kuungiwa umeme kuingia katika *account* ya mtendaji wa shirika ndugu Zakia Juma Azan ambapo wametwambia kwamba hatua za nidhamu zimechukuliwa kwa mujibu wa sheria ya Utumishi wa Umma namba 2 ya mwaka 2011. Mfanyakazi huyo amehamishwa kutoka Shirika la Umeme kwenda Wizara ya Ardhi Makaazi na Maji na huku akiangaliwa utendaji wake. Hivi ndio sheria inavyozungumza, ndivyo sheria inavyosema, sheria ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2011 akiibia mtu huku umuhamishe na umpeleke sehemu nyengine.
Eneo jengine ni hoja namba 23, nimenyokoa nyokoa tu kwa maneno ya kikwetu kidogo tu. Hoja hii inasema:-

"Kushindwa kuthibitisha wapi zimenunua nguzo na *Transformer* zilizotumika katika nyumba ya kupumzikia ya ndugu Shumbana Aman Karume na kushindwa kuthibitisha wapi imenunuliwa *Transformer* hiyo na mambo mengine"

Ripoti inasema kwamba:

"Serikali ilifanya ukaguzi wa eneo linalohusika na hoja hii na kubaini kwamba nguzo zilizotumika katika

kuupeleka umeme huo ni 20 na Shirika la Umeme ndilo lililopeleka nguzo hizo"

Mimi nataka kumuuliza Mhe. Mohammed Aboud Mohammed, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais huu ukaguzi wewe ulikwenda? Hizo nguzo kweli ni 20?
Mhe. Spika, kwa sababu wakati mwengine mnapoandikiwa haya mambo muangalie nguzo 20, hivi leo tukitoka hapa kama tunakwenda kwa kuhesabu hizo nguzo zikiwa zaidi ya nguzo 20 utakuja kukiambiaje chombo hichi?

Mhe. Spika, nguzo zaidi ya 40 zimeungwa wanasema hapa wezangu nguzo 49 zimehesabiwa moja baada ya moja, kutwambia nguzo 20 haya mambo vipi. Halafu unatwambia kwamba umeme umepelekwa kule kwa sababu kuna hoteli zimeshajengwa hoteli mbili, kuna muwekezaji. Wakati umeme haukupelekwa katika nyumba ya uwekezaji, umeme umepelekwa kwenye nyumba ya kupumzikia bure hakuna vielelezo vyovyote vinavyoonesha malipo juu ya nguzo zilizopelekwa kule. Halafu mnaleta ripoti hapa ya ubabaishaji.

Hoja namba 30 kuhusu uuzwaji wa gari *land rover*. Wenzangu wamezungumzia hapa ambapo Wizara ya Fedha imekataa kuidhinisha juu ya uuzaji wa gari hizi. Lakini gari hizi zimeuzwa hatua gani imechukuliwa, mtu kaonywa zaidi ya mara tano. Ndio Sheria ya Utumishi wa Umma ameonywa zaidi ya mara 5 huu ni wizi. Katika sheria ya Kiisilamu mwizi anatakiwa akatwe mkono. Nchi yetu hii si ya kiislamu tu lakini katika sheria ya kiisilamu wezi hawa wanatakiwa wakatwe mikono ikithibitika.
Hoja ya mwisho ambayo nilikuwa nataka kuitolea maelezo ni hoja ya 36 na 37. Mhe. Spika, mimi nina masikitiko makubwa sana. Nina masikitiko makubwa juu ya hoja hii ambapo naomba kunukuu Mhe. Waziri anatwambia hivi:-

"Napenda kutoa ufafanuzi kwamba majenereta haya hayakununuliwa kwa fedha za *NBRI* bali yalinunuliwa na fedha za wahisani na serikali"

Hayo majenereta 32 yanayolalamikiwa anaendelea kusema.

"Aidha ununuzi huu ulifanywa kwa mashirikiano baina ya wahisani na serikali chini ya mshauri wa mradi wa umeme vijijini aliekubalika na wahisani hao. Ununuzi huo ulifanyika chini ya utaratibu wa manunuzi katika hali ya dharura ambayo walikubalika na pande zote mbili"

Hiyo ndio ripoti ya Mhe. Mohammed Aboud Mohammed, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais aliyotueleza.

Mimi ninachotaka kusema Mhe. Spika, hivi serikali imeridhishwa na hali ile kwamba leo wanasema kwamba utaratibu umefatwa kwa manunuzi zaidi ya bilioni 7 ziko pale hazifanyi chochote, majenereta pale yamekaa hayafanywi kazi.

Mhe. Spika, juzi juzi tu hapa tulikuwa na mgao wa umeme kama ambapo majenereta yale yangetumika kwa niaba ya wananchi tungeyatumia majenereta zile kuondosha mgao wa umeme wenzetu wahisani wametupa pesa tumechanganya na pesa za walipa kodi wa Zanzibar wametukusudia kutuondoshea tatizo kuwe na *standby* ya jenereta kuondoa ikitokea matatizo. Leo hazina maana yoyote zile hazitumiki hazina faida haziuziki halafu mnatwambia aah maana yake utaratibu umefatwa, wahisani wamekubali ng'oma iko pale tunawaambia nini wananchi wa Zanzibar juu ya hali ile.

Hivi hakuna uwajibikaji katika nchi hii wale waliohusika na ununuzi wa majenereta yale mabovu hawawajibiki? Fedha zile zilizopotea pale hakuna uwajibikaji iwe ndio basi tu. Juzi tunasikia taarifa kwenye redio kwamba Shirika la Umeme limeiandikia serikali kwamba wanataka ziuzwe, nani anazitaka jenereta zile. Hivi serikali imeshindwa kuziendesha nani atanunua uoza ule, wizi ule nani ataununua? Tunanunua vifaa tunatumia fedha za serikali wizi mtupu!

Mhe. Spika, hapana manunuzi au taratibu zilizotumika kisheria pale palikuwa na njia ya ubadhirifu na wizi wa mali za serikali na fedha za wahisani. Na kama pangekuwa pametumika utaratibu uliokuwa bora wa kuisadia serikili, jenereta zile

tungekuwa sasa tunazitumia. Lakini pale pana hila zimefanyika katika ununuzi tunatumia njia ya kuwababaisha wananchi ya kuona kwamba zimenunuliwa. Lakini vitu vyengine havifichiki, viko pale wananchi wanajiuliza pesa zile zilizotumika pale zimekuwa ni *useless* hivi hakuna utaratibu wa kuwajibika.

Lazima Mhe. Spika, waliohusika na ununuzi wa majenereta yale wawabijishwe na isitoshe wapelekwe Mahakamani kwa uhujumu wa uchumi wa nchi hii. Itumike sheria ya uhujumu wa mali za nchi, wale ni wahujumu wa uchumi walionunua jenereta zile. Wananchi hawawezi kuvumilia kuona watu wanatumia mamlaka yao waliopewa kuharibu uchumi, tumeweka majenereta pale hayana faida yoyote halafu tunasema tuuze wala hatujayatumia, yamenunuliwa hayajatumika tunataka kuyauza maana yake nini? Halafu mnaleta ripoti ya ubabaishaji hapa, kwamba maana yake taratibu zimefuatwa washirika wamekubali wamefanya hivi tunaharibu fedha za serikali. Mimi nakubaliana na Mhe. Hija Hassan Hija tuwaambie Washirika wa Maendeleo fedha zao zinavurugwa hapa hazitumiki vizuri. Tunataka waliohusika na ununuzi wa majenereta yale wawajibishwe mara moja na isitoshe washitakiwe. Sheria ya Uhujumu wa uchumi lazima itumike, wale ni wahujumu wa uchumi wa nchi hatuwezi kustahamili.

Mhe. Spika, kwa kweli aibu na inasikitisha na inahuzunisha kwamba hakuna hatua zinazochukuliwa juu ya matendo ya aina hii, inasikitisha sana na kama tunaendelea na utaratibu huu masuala haya ya uharibifu yataendelea . Uchukuaji wa mali za umma utaendelea na hatuwezi tukaendelea hata siku moja. Kuendelea kwetu inakuwa ni ndoto, kama tunawasaidia wenzetu wanatusaidia lakini sisi hatu-*appreciate* ule msaada ambao tunapewa, tunaweka tamaa zetu, shida zetu mbele *milghairi* ya kuangalia maslahi ya wananchi.

Leo wananchi wanalazimika kununua umeme kwa bei ya juu, kisingizio kwamba Shirika la Umeme makusanyo yake hayakidhi madeni ya *TANESCO*. Si kweli tunawabebesha

wananchi wetu mzigo, tunawapandishia bei kila siku kwa sababu ya wizi wetu. Tunaziiba pesa za shirika halafu tunasema pesa tunazokusanya hazitoshi. Matokeo yake tunapandisha umeme kila siku, tunawaongezea ughali wa maisha wananchi wetu kila siku, hawana uwezo wa kulipa umeme. (*Makofi*).

Kwa kweli serikali ni lazima jambo hili walione kwamba wizi huu tunaoufanya katika shirika na tunaufumbia macho utawaweka pahala pagumu wananchi wetu. Tunapandisha bei za umeme kila kukicha wananchi hawana uwezo, mahitaji yamekuwa makubwa na vipato vyao vimekuwa vidogo. Lakini sisi huku tumefumba macho hatuoni. Hii ni aibu Mhe. Spika.

Mhe. Spika, mimi siungi mkono maelezo haya na ninamrejeshea mwenyewe Mhe. Mohamed Aboud Mohamed afahamu kwamba hayakubaliki. Huu ni ubabaishaji wa chombo hiki na nyinyi wenyewe munajua kwamba huu ni ubabaishaji ni lazima hatua madhubuti zichukuliwe juu ya ripoti hizi ambazo tunazoziwasilisha hapa ili wananchi wajenge imani na serikali yao. (*Makofi*).

Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*).

Mhe. Marina Joel Thomas: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii kuchangia taarifa hii.

Kwanza Mhe. Spika, ninaipongeza serikali kwa hatua ilizochukua. Ninaipongeza kwa sababu kuna hoja karibu 38 serikali imezifanyia kazi na kuna nyengine baadhi ya hoja serikali imetamka kama inazidi kuzifanyia uchunguzi na uchunguzi wenyewe upo katika vyombo vya Polisi.

Mhe. Spika, taarifa inapotolewa katika chombo kama hichi, serikali pia inatakiwa ijiridhishe na taarifa hii na zile ambazo inahisi zinataka uchunguzi zaidi ili serikali itakapotoa maamuzi itoe maamuzi ya uhakika. Kuna hoja mbali mbali Mhe. Spika,

humu nikiangalia kama hoja ya nambari 5 inayosema namna ya upatikanaji wa vifaa vya uungwaji wa umeme katika Hoteli ya Misali.

Serikali hapa pia ukiangalia imesema hivyo, serikali imemuagiza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya uchunguzi zaidi kwa suala hilo, baada ya uchunguzi huo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, serikali itachukua hatua muafaka ya kuzingatia ushahidi unaopatikana.

Mhe. Spika, hii nayo ni hatua kwa sababu jambo linalofanyika lolote linahitaji kufanyiwa uchunguzi wa kina. Kazi aliyopewa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili serikali ione inajiridhisha na ripoti ambayo iliyotolewa na endapo itakapotoa maamuzi itoe maamuzi ya uhakika.

Kuna hoja mbali mbali humu ambazo serikali kama hoja 10 hii pia, pia serikali imetoa tamko imesema kuwa serikali inaendelea kulifuatilia suala hili kutokana na kukosekana kwa taarifa zitakazowezesha kutoa maelezo sahihi. Ina maana hapa serikali kwa mtizamo wangu taarifa zilizotolewa pengine haijaridhika nazo. Kwa hivyo ina maana inaendelea kulifuatilia kwa kina ili pindipo itakapotoa taarifa yake itoe ya uhakika, si inatoa taarifa ambayo haina vielelezo ambavyo vinavyofaa.

Ukiangalia hoja nyengine Mhe. Spika, kuna hoja nambari 20 "Upotevu wa kumbukumbu za mteja". Pia serikali nayo imechukua hatua, serikali imeliagiza Shirika la Umeme kufanya uhakiki wa wateja wakubwa na wadogo ili kujua idadi halisi ya wateja na kuweka kumbukumbu zao.

Aidha, serikali imeliagiza Shirika la Umeme kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya wafanyakazi waliohusika na kitendo hiki. Serikali imechukua hatua Mhe. Spika. Hoja mbali mbali Mhe. Spika, imechukua hatua na zile ambazo serikali inahitaji kujiridhisha ndio inazipeleka Polisi, inapeleka katika vyombo

vya ulinzi na usalama ili iamue nini maamuzi ya busara itakayotoa kwa serikali. Serikali haikurupuki tu. (*Makofi*).

Mhe. Spika, hapa nilikuwa na ushauri kwa serikali kwa zile hoja ambazo zimeekwa kwenye uchunguzi kwenye vyombo mbali mbali vya ulinzi na usalama, ushauri wangu uchunguzi utakapokamilika tunaomba taarifa hii tuletewe Barazani ili turidhike na taarifa hiyo. Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi ninaunga mkono taarifa hii asilimia mia moja. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe ninafikiri inafaa tukapumzike na kuna wachangiaji wachache waliobaki ambao hawa ninategemea wamalize michango yao siku ya Jumatatu, penye maajaliwa kipindi cha asubuhi, na kama kutakuwa na Waheshimiwa Mawaziri mawili matatu wanaotaka kuchangia wanaweza pia nao wakaomba hiyo siku ya Jumatatu.

Lakini ratiba yetu inatuelekeza kwamba shughuli hii tuimalize siku ya Jumatatu kipindi cha asubuhi. Kwa hivyo Waheshimiwa Mahmoud Muhamed Mussa, Mhe. Hamza Hassan Juma na Jaku Hashim Ayoub pamoja na wale Waheshimiwa Mawaziri ambao watakaoomba baadae shughuli hiyo ifanyike siku ya Jumatatu.

Waheshimiwa Wajumbe ninawashukuru kwa kuendelea na shughuli zetu kwa mashirikiano makubwa. Baada ya hayo basi sasa niakhirishe kikao hiki hadi siku ya Jumatatu tarehe 21/10/2013 saa 3.00 za asubuhi.

(Saa 1.37 Usiku Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 21/10/2013 saa 3.00 asubuhi)